# UCHANGANUZI WA KIMOFOSINTAKSIA WA VIANGAMI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

**TASNIFU YA**

**KIMONYE NAOMI NDUMBA**

**C50/CE/25010/2014**

**TASNIFU HII INAWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MEI 2021**

ii

## UNGAMO

Tasnifu hii ya utafiti ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni yoyote katika chuo kingine.

MTAFITI

KIMONYE NAOMI NDUMBA

NAMBARI YA USAJILI C50/CE/25010/2014

Sahihi Tarehe

Naomi 9/11/2020

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

1. Daktari Leonard Chacha Mwita

   Sahihi Tarehe

   9/11/2020

2. Daktari Jacktone Onyango

   Sahihi Tarehe

   9/11/2020

## SHUKRANI

Shukrani zangu zimwendee Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kuanza na hatimaye kukamilisha utafiti huu. Ninawashukuru wasimamizi wangu, Daktari Chacha Mwita na Daktari Jactone Onyango, kwa kuniongoza vyema katika utafiti huu. Maarifa yao yalichangia katika kuimarisha kazi hii.

Ninatoa shukrani za dhati kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunipa fursa ya kuyaendeleza masomo yangu. Ninawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili: Profesa King'ei, Daktari Chacha, Daktari Onyango, Daktari Ngugi, Daktari Osore, Daktari Maitaria, Daktari Masinde na Daktari Wafula. Mafunzo yenu katika shahada ya uzamli yamenifaa sana. Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki.

Ninaishukuru familia yangu kwa kunishika mkono na kunipa matumaini kila wakati. Wazazi wangu Simon Kimonye na Bertha Kanyua walinipa moyo kila wakati. Ndugu zangu Ann, Isaac na Mary. Ninamshukuru mume wangu Simon Kiarie na watoto wangu Nicholas, Clara na Natalia kwa kunisaidia kukamilisha kazi hii.

# TABARUKU

Mume wangu mpendwa Simon Kiarie na watoto wetu Natalia, Clara na Nicholas.

Mungu awabariki sana.

Wazazi wangu wapendwa Simon Kimonye na Bertha Kanyua.

Mungu awabariki sana

Ndugu zangu Ann, Isaac na Mary. Mungu awabariki sana

## IKISIRI

Lengo la utafiti huu ni kushughulikia uchanganuzi wa kimofosintaksia wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulilenga kuthihirisha kuwa kuna aina tofauti za viangami katika lugha ya Kiswahili. Viangami ni mofimu zinazojisimamia kisintaksia lakini kifonolojia ni tegemezi. Viangami hutegemea neno kuu kifonolojia. Viangami huambishwa kwa neno kuu. Kiangami ni sehemu ya neno kamili inayochukua nafasi ya kiambishi. Utafiti ulilenga kuchunguza changamoto katika uainishaji wa maneno yenye viangami, tofauti zilizopo katika uambishaji wa viambishi na viangami katika lugha ya Kiswahili, sheria za uundaji wa viangami na sifa arudhi za viangami. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni Nadharia Boreshaji ambayo iliasisiwa na Prince na Smolensky (1993). Kila sarufi inaweza kushughulikia maumboghafi tofauti. kwa mujibu wa nadharia hii, kunafaa kuwa na mfanano kati ya umboghafi na umbotokeo. Nadharia hii inajikita katika sifa bia za lugha zinazotumika kuunda miundo rasmi ya lugha. Ni kwa misingi hii ambapo utafiti huu ulijaribu kuchunguza kuwepo kwa viangami katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Katika maktaba, mtafiti alisoma kwa undani tafiti zilizofanywa na wanaisimu mbalimbali kuhusu viangami katika lugha tofauti. Vitabu vingine vilivyochapishwa na vimeshughulikia viangami vilipitiwa kwa undani. Vipengele vya utafiti vilivyohusishwa ni kama vile; mbinu za usampulishaji, sampuli iliyotumika iliteuliwa kimakusudi. Katika uteuzi wa sampuli, mtafiti aliteua vitabu tofauti. Mbinu za ukusanyaji wa data zilizotumiwa ni kusoma kwa kina makala kutoka maktabani. Mtafiti aliwasilisha matokeo yake kwa njia ya maelezo. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali. Kwa mujibu wa utafiti huu viangami vya Kiswahili vinaweza kuambishwa mwanzoni na mwishoni mwa neno. Viangami vinaambishwa kwa nomino, vitenzi, vihusishi na pia vielezi. Utafiti huu utaweza kurejelewa katika siku za usoni kuendeleza tafiti za ziada za viangami. Utafiti huu uliazimia kuwanufaisha wanaisimu kwani utaendeleza lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa lugha ya Kiswahili na waandishi wa vitabu vitabu vya Kiswahili pia watanufaika.

## ABSTRACT

This thesis seeks to analyze the morphological and syntactical structures of clitics in Kiswahili language. The aim of this research is to prove that, there are different types of clitics in the Kiswahili language. A clitic is a morpheme that has syntactic characteristics. A clitic is phonologically bound to the host. In Swahili and other similar languages, clitics attach to the adjacent word or the host. A clitic is a part of a word which takes the position of a affix. This research analyzed the challenges of categorizing Kiswahili word that have been attached a clitic, comparison of clitics and affixes, rules that determine the attachment of a clitic to the host and the effect of a clitic to the prosody of the main word. This research was anchored on the Optimality Theory which was originally proposed by Prince and Smolensky (1993). According to Optimality Theory, there are two basic types of constraints in every language, the output and the input. Every grammar can handle every possible input. In Optimality Theory, constraint is universal. These constraints require identity between input and output forms. The principles behind this theory helped in analyzing the characteristics and use of clitics in the Kiswahili language. The researcher got data from the library. In the library, the researcher read different thesis and books that are related to clitics as it has been studied by different linguists. Publications that have touched on clitics were studied. The research methodology entailed sampling procedures whereby the researcher purposively sampled published materials on clitics. Pen and paper were the instruments used for note taking. The data was collected by reading books from the library. Finally, the data collected was analyzed and presented using descriptive method. The study found that there are proclitic and endclitic in Kiswahili. In Swahili, clitics can attach themselves in nouns, verbs, prepositions and adverbs. The findings of this study will be used as reference in the further study of clitics in Swahili language. The beneficiaries of this research will be the Kiswahili linguists, the students and the authors of Kiswahili language.

## MAELEZO YA ISTILAHI

| | | |
|---|---|---|
| Kilele | : | Kiini cha silabi. |
| Kiambishi | : | Ni kiungo cha kisarufi kinachoambatishwa kwenye mzizi wa neno ili kulipa neno maana mbalimbali. |
| Kiangami | : | Ni kipashio cha lugha kinachotokana na neno kuu na kinajiambatisha kwa neno huru. |
| Mofosintaksia | : | Tawi la isimu linalochunguza uhusiano uliopo kati ya mofolojia na sintaksia. |
| Maumboshindani | : | Maumbo tofauti yanayoshindana ili kufikia upeo wa kukubalika. |
| Neno kuu | : | Ni neno ambalo linaambishwa kiangami. |
| Umboghafi | : | Umbo asilia. |
| Umbotokeo | : | Umbo linalofikia kiwango cha kukubalika kulingana na nadharia ya umbo upeo. |
| Umajumui | : | Kupatikana katika sarufi zote za lugha. |
| Upangiliaji | : | Mpangilio wa mashartizuizi kwa kufuata nguvu na uhafifu wa mashartizuizi husika. |

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **FIKI-UKO** | : | Fikia ukomo |
| **HKODA** | : | Silabi haiwezi kuishia kwa koda |
| **MASHA-ZU** | : | Mashartizuizi |
| **Nsarufi** | : | Neno la kisarufi |
| **NArudhi** | : | Neno lenye sifa za kiarudhi |
| **TATHI** | : | Tathmini |
| **SHABI** | : | Shahibiana |
| **ZALI** | : | Zalishi |
| **K** | : | Konsonanti |
| **I** | : | Irabu |
| ***II** | : | Irabu mbili hazifai kufuatana |
| **KV** | : | Mfuatano wa konsonanti na irabu |
| ***KYK** | : | Kiyeyusho hakiwezi kutokea katikati ya konsonanti mbili halisi |
| ***KKKB** | : | Hakuna mfuatano wa konsonanti tatu halisi |
| **TEGE** | : | Tegemezi |
| **UU** | : | Umbo upeo |
| **LE** | : | Kilele cha silabi |
| **TA** | : | Tangulio |
| **FU** | : | Fungio |
| **CH** | : | Toni ya chini |
| **JU** | : | Toni ya juu |
| **KA** | : | Toni ya kati |

# ALAMA

| | |
|---|---|
| * | Alama ya kinyota imetumika kuonyesha makosa ya kisarufi |
| - | Alama ya kistari kifupi imetumika kutenganisha vipashio au viungo vya kisarufi kama vile viambishi. |
| // | Fonimu/sauti |
| → | Mchakato |
| [ ] | Uwakilishaji wa kifonetiki |
| σ | Silabi |
| ø | Kapa |
| $ | Mpaka wa silabi |
| # | Mpaka wa neno |

# YALIYOMO

**UNGAMO**------------------------------------------------------------------------------------**ii**

**SHUKRANI**---------------------------------------------------------------------------------**iii**

**IKISIRI**----------------------------------------------------------------------------------------**iv**

**ABSTRACT**--------------------------------------------------------------------------------**v**

**MAELEZO YA ISTILAHI**-------------------------------------------------------------**vi**

**MAELEZO YA VIFUPISHO**-------------------------------------------------------**vii**

**MAELEZO YA ALAMA**-------------------------------------------------------------**viii**

**YALIYOMO**--------------------------------------------------------------------------------**ix**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**-----------------------------------------------1

1.1 Usuli wa Mada----------------------------------------------------------------------1

1.2 Suala la Utafiti----------------------------------------------------------------------5

1.3 Malengo ya Utafiti -----------------------------------------------------------------6

1.4 Maswali ya Utafiti -------------------------------------------------------------------7

1.5 Sababu za Kuchagua Mada-------------------------------------------------------7

1.6 Upeo na Mipaka---------------------------------------------------------------------9

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada----------------------------------------------------9

1.7.1 Maana ya Kiangami---------------------------------------------------------------10

1.7.2 Utata katika Viangami vya Kiingereza----------------------------------------11

1.7.3 Tofauti kati ya Viambishi na Viangami---------------------------------------13

1.7.4 Mfanano kati ya Viambishi na Viangami-------------------------------------19

1.7.5 Tafiti kuhusu Viangami na Mbinu Zilizotumika------------------------------22

1.7.6 Maana ya Mofosintaksia-----------------------------------------------------------23

1.8 Nadharia Boreshaji-------------------------------------------------------------------24

1.8.1 Misingi ya Nadharia----------------------------------------------------------25
1.8.1.1 ZALI---------------------------------------------------------------------------25
1.8.1.2 MASHA-ZU----------------------------------------------------------------26
1.8.1.3 TATHI-------------------------------------------------------------------------26
1.8.2 Mihimili ya Nadharia--------------------------------------------------------27
1.8.2.1 Umajumui--------------------------------------------------------------------27
1.8.2.2 Ukiukwaji---------------------------------------------------------------------28
1.8.2.3 Upangiliaji--------------------------------------------------------------------28
1.8.2.4 Usambamba-----------------------------------------------------------------28
1.8.3 Mashrtizuizi ya Umbo Upeo-----------------------------------------------29
1.8.3.1 Mashartizuizi ya Uziada---------------------------------------------------29
1.8.3.2 Mashartizuizi ya Uadilifu-------------------------------------------------31
1.9 Mbinu za Utafiti --------------------------------------------------------------33
1.9.1 Mbinu za Usampulishaji----------------------------------------------------33
1.9.2 Uteuzi wa Sampuli-----------------------------------------------------------33
1.9.3 Mbinu za Ukusanyaji Data-------------------------------------------------34
1.9.4 Kusoma na Kunukuu--------------------------------------------------------34
1.9.5 Uchanganuzi wa Data-------------------------------------------------------35
1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo---------------------------------------------------35
1.10 Hitimisho----------------------------------------------------------------------- 36
**SURA YA PILI: UAMBISHAJI WA VIANGAMI NA VIAMBISHI-----37**
2.1 Utangulizi-------------------------------------------------------------------------37
2.2 Mofolojia ya Kiswahili-------------------------------------------------------37
2.3 Kuambatisha Viangami na Viambishi---------------------------------------42

2.3.1 Maumbo ya Viangami na Viambishi------------------------------------------43
2.3.2 Maumbo ya Viambishi----------------------------------------------------------44
2.3.3 Maumbo ya Viangami----------------------------------------------------------46
2.3.3.1 Viangami vya Irabu Moja-----------------------------------------------------49
2.3.3.2 Viangami vya Konsonanti Ikifuatwa na Irabu--------------------------------52
2.3.3.3 Viangami vya Silabi Mbili-----------------------------------------------------54
2.3.3.4 Viangami Funge--------------------------------------------------------------56
2.4 Uainishaji wa Viangami na Viambishi----------------------------------------58
2.4.1 Uainishaji wa Viambishi kwa Kuzingatia Nafasi----------------------------59
2.4.1.1 Viambishi Awali----------------------------------------------------------------60
2.4.1.2 Viambishi Tamati---------------------------------------------------------------64
2.4.2 Uainishaji wa Viambishi Kiuamilifu------------------------------------------68
2.5 Uainishaji wa Viangami ------------------------------------------------------73
2.5.1 Uainishaji wa Viangami kwa Kuzingatia Nafasi-----------------------------73
2.5.1.1 Viangami Awali------------------------------------------------------------------74
2.5.1.2 Viangami Tamati----------------------------------------------------------------76
2.5.2 Uainishaji wa Viangami Kiuamilifu-------------------------------------------77
2.5.2.1 Vimilikishi-----------------------------------------------------------------------78
2.5.2.2 Nafsi-----------------------------------------------------------------------------80
2.5.2.3 Viashiria ------------------------------------------------------------------------81
2.5.2.4 Viulizi----------------------------------------------------------------------------82
2.6 Tofauti ya Viangami na Viambishi-------------------------------------------82
2.6.1 Kuambishwa kwa Neno-------------------------------------------------------83
2.6.2 Dhana Inayowakilishwa------------------------------------------------------ 84

2.6.3 Viangami Kubadilika--------------------------------------------------------------84

2.6.4 Mabadiliko katika Neno Mpya------------------------------------------------- 85

2.6.5 Viangami ni Virai-------------------------------------------------------------------86

2.7 Hitimisho-------------------------------------------------------------------------87

**SURA YA TATU: UTARATIBU WA UUNDAJI WA VIANGAMI VYA KISWAHILI---------------------------------------------88**

3.1 Utangulizi-----------------------------------------------------------------------88

3.2 Sarufi ya Lugha ya Kiswahili---------------------------------------------------89

3.3 Vipashio vya Lugha ya Kiswahili----------------------------------------------90

3.4 Utaratibu wa Kuunda Viangami------------------------------------------------93

3.4.1 Viangami ni Aina ya Silabi--------------------------------------------------------94

3.4.2 Viangami huwa na Irabu Moja---------------------------------------------------99

3.4.3 Maana Halisi ya Neno Hubakia----------------------------------------------103

3.4.4 Maneno Yanayoathirika Hufatana--------------------------------------------104

3.4.5 Kiangami Kihusiane na Neno Kuu--------------------------------------------106

3.4.6 Neno Moja Hupachikwa Kiangami Kimoja----------------------------------109

3.4.7 Kiangami Huambishwa Neno Kamili-----------------------------------------111

3.4.8 Kangami Huambishwa Neno Moja-------------------------------------------112

3.4.9 Hakuna Viangami vya Konsonanti Pekee-----------------------------------113

3.5 Hitimisho---------------------------------------------------------------------116

**SURA YA NNE: MWINGILIANO BAINA YA SIFA ZA KIARUDHI NA VIANGAMI-----------------------------------------------**117

4.1 Utangulizi-----------------------------------------------------------------------117

4.2 Fasili ya Sifa za Kiarudhi-------------------------------------------------------117

4.2.1 Shadda katika Viangami--------------------------------------------------------119

4.2.2 Kiimbo katika Viangami---------------------------------------------------133

4.2.2.1 Kiimbo cha Kushuka--------------------------------------------------------136

4.2.2.2 Kiimbo cha Kupanda--------------------------------------------------------137

4.2.2.3 Kiimbo cha Kupanda na Kushuka-------------------------------------------138

4.3 Hitimisho--------------------------------------------------------------------142

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO---143**

5.1 Utangulizi-------------------------------------------------------------------143

5.2 Muhtasari--------------------------------------------------------------------143

5.3 Matokeo ya Utafiti-----------------------------------------------------------146

5.4 Umuhimu wa Utafiti---------------------------------------------------------147

5.5 Changamoto------------------------------------------------------------------149

5.6 Hitimisho--------------------------------------------------------------------149

**MAREJELEO---------------------------------------------------------------------150**

**VIAMBATISHO-----------------------------------------------------------------155**

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli wa Mada

Lengo la isimu ni kuchunguza, kuchambua, kuchanganua na kufafanua lugha. Taaluma ya isimu ni pana sana. Utafiti huu wa uchanganuzi wa viangami katika lugha ya Kiswahili, unajikita zaidi katika tawi la isimu linganishi. Kulingana na Lebman (1973), isimu linganishi huwa na dhima ya kuchunguza lugha mbalimbali ili kuzilinganisha na kuzilinganua. Hapa, lugha huchunguzwa katika viwango vyote ambavyo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kiangami ni kipashio cha lugha kinachopatikana katika lugha nyingi ulimwenguni. Katika utafiti huu, viangami vilichunguzwa katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki.

Mgullu (2001) anaeleza kuwa, wanaisimu linganishi wameweza kuainisha lugha katika makundi tofauti kwa kuongozwa na vigezo fulani. Vigezo hivi ni kama vile, uainishaji wa kinasaba, uainishaji wa kijiografia, uainishaji wa kimuundo na mwisho ni uainishaji wa kiuamilifu. Kigezo kinachotumika zaidi kuainisha lugha ni kile cha kimuundo. Kigezo hiki ni cha uhakika zaidi kwani kinatumia muundo wa lugha. Kwa kutumia kigezo hiki, wanaisimu wanapata vikundi viwili vya lugha, lugha tenganishi na lugha ambishi. Lugha tenganishi ni zile ambazo maumbo ya maneno yake hayaambishwi wala kunyambuliwa. Maneno katika

lugha hizi huwa ni mofu moja tu ambayo huwakilisha mofimu moja tu. Mifano ya lugha tenganishi ni kama vile Kichina na Kivietinamu. (Mgullu, 2001).

Kwa upande mwingine, lugha ambishi ni zile lugha ambazo maneno yake huambishwa viambishi mbalimbali ili kupata maana tofauti. Viambishi ni vipashio vya lugha vinavyofungamanishwa na mzizi wa neno ili kupata neno jipya au muundo mpya wa neno (Denham na Lobeck, 2010). Kunayo makundi matatu ya lugha ambishi ambayo ni, lugha ambishi mchanganyo, lugha ambishi bainishi na lugha muundogubi (Mgullu, 2001). Katika makundi haya matatu, lugha ya Kiswahili inaainishwa kama  lugha ambishi-bainishi.

Lugha ambishi bainishi ni kundi la lugha ambayo maneno yake huwa na viambishi vinavyodhihirika moja kwa moja. Katika lugha ambishi bainishi, maana ya neno huwa kwenye mzizi wa neno lenyewe. Mzizi wa maneno katika lugha ambishi bainishi hujitokeza waziwazi na mizizi yenyewe haijichanganyi na viambishi. Baadhi ya lugha za kibantu huwa katika kundi hili. Kiswahili ni mojawapo wa lugha ambishi bainishi kwa vile maneno ya lugha ya Kiswahili huweza kuwekwa viambishi mbalimbali bila kuchanganya mzizi wa neno na viambishi vile. Katika lugha ya Kiswahili, ni rahisi kuonyesha mzizi wa neno na viambishi pia. Viambishi vinaweza kuwa vya awali au tamati. Kwa mujibu wa Quinion (2008), viambishi awali huja kabla ya mzizi navyo viambishi tamati huja baada ya mzizi. Tazama mfano huu,

1. (a) Nomino *m* - <u>*tu*</u> (umoja)

umoja mzizi

*wa* - <u>*tu*</u> (wingi)

wingi mzizi

(b) Kitenzi *a* – *na* – <u>*som*</u> – *e* - *a*

Nafsi wakati mzizi kauli kiishio

Vimbishi awali Viambishi tamati

Kulingana na mfano huu, maneno katika lugha ya Kiswahili huwa na mzizi. Mfano 1. unadhihirisha uwepo wa viambishi awali na viambishi tamati katika maneno ya Kiswahili. Kiambishi kinachotangulia mzizi, kinajulikana kama kiambishi awali kama vile 1a, -*m*- na 1b, -*a*-*na*-. Ikiwa kiambishi kinatokea baada ya mzizi basi kitakuwa kiambishi tamati kama vile, 1b, -*e*-*a*-.

Lugha ya Kiswahili inavyo vipashio mbalimbali. Vipashio hivi ni muhimu kwani ndivyo vinavyounda sentensi. Vipashio hivi ni sauti, silabi, neno na sentensi. Massamba na wengine (1999) wanavieleza vipashio vya kisarufi kwa ruwaza ya tungo na vipengele vyake. Wanataja vipengele hivyo kama neno, kirai, kishazi na sentensi. Njia moja ya kuunda maneno ya Kiswahili ni ile ya kupachika viambishi katika mzizi/shina la neno husika. Kiswahili, kama ilivyo katika lugha zingine, huwa na maneno yanayoambishwa na yale yasiyoambishwa. Kwa mujibu wa Mgullu (2001), lugha ya Kiswahili ina maneno mengi zaidi yanayoweza kuambishwa kuliko yale yasiyoambishwa.

Katika utafiti wake Munguti (1989), mbinu tofauti za uundaji wa nomino za Kiswahili zimeshughulikiwa. Mbinu moja aliyoelezea ni ile ya kuambatanisha maneno. Kulingana na Munguti, maneno mawili au zaidi huweza kuunganishwa na kuunda neno moja. Mifano ni kama vile: *ufundimitambo, elimuviumbe, askarikanzu* na kadhalika.

Matundura (2016) ameshughulikia mbinu tofauti za uundaji wa istilahi katika Kiswahili. Ameshughulikia uambishaji wa maneno kama mbinu moja. Kulingana naye, viambishi awali na viambishi tamati hubandikwa kwenye mzizi wa neno na hivyo kupata neno lenye maana tofauti ingawa maana inahusiana na neno la awali. Kwa mfano, mzizi -lim- huweza kuzalisha maneno kama vile: *lima, limia, limisha, limiana* na *limika.*

Wakati mwingine kuna maneno ambayo ni kamili lakini yanatumika kuambisha maneno mengine. Kwa mfano, katika kirai *Baba yake,* neno 'yake' ambalo ni kimilikishi linaweza kuambishwa kwa neno 'baba' hivi kwamba neno moja, *babake* litaibuka. Kipashio *–ke-* hapa kinaitwa kiangami na wala si kiambishi. Kiangami ni neno la Kiswahili lenye maana sawa na neno la Kiingereza *clitic. Clitic* ni neno linalotokana na neno la Kigiriki *klitikos* lililo na dhana ya egemeza (Anderson, 2010).

Dhana za viangami na viambishi zinakaribiana sana kwani, zote mbili zinahusu kuambatanisha vipashio vya kusarufi. Tofauti ni kuwa, viambishi katika lugha ya Kiswahili hupachikwa kabla au baada ya mzizi (Massamba na wengine, 1999).

Kwa mfano: mzizi –*som*- huweza kuambatishwa viambishi na kupata neno, *a-na-ye*-**som**-*e-a*. Kwa upande mwingine, kiangami ni neno kamili ambalo linapodondoshwa baadhi ya silabi, linaambatishwa kwenye neno lingine kamili. Kwa mfano katika neno *yake,* silabi ya kwanza inadodoshwa na kupata kiangami –*ke*. Kiangami hiki kinaweza kuambishwa kwa neno kamili *baba* na kupata neno *babake.*

Suala hili la viangami si suala jipya na limeshughulikiwa katika lugha tofauti kama vile Kiingereza, Kiarabu, Degema, Kichina, Kiitaliano na kadhalika. Utafiti huu ulishughulikia viangami katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia vigezo vya mofolojia, fonolojia, sintaksia na semantiki.

## 1.2 Suala la Utafiti

Kwa mujibu wa Anderson (2010), kiangami ni kipashio cha lugha ambacho kinategemea neno lingine kimatamshi. Kama viambishi, viangami pia huambishwa kwa maneno. Sheria zinazotumiwa kuambisha viambishi ni wazi lakini sheria zainazotumika kuambisha viangami si dhahiri. Shughuli ya kuambisha maneno ya Kiswahili hufanywa kwa uangalifu mkubwa sana. Waandishi na wazungumzaji hawahitaji kufanya mambo kimakusudi. Mizizi au maneno makuu yanapoambishwa viungo vya kisarufi, inadhihirika kwamba kunazo sheria fulani zinazofuatwa. Kwa mfano ni sawa kusema *baba**ke*** ila si sawa kusema *shangazi**ke.***

Hata kama utafiti wa viangami umefanywa katika lugha zingine ulimwenguni, kuna haja ya utafiti huu kufanywa katika lugha ya Kiswahili. Muundo wa lugha ya

Kiswahili unatofautiana na ule wa lugha zingine zilizofanyiwa utafiti kama vile, lugha ya Kiingereza, Kiarabu na hata lugha ya Yoruba. Kulingana na Spencer na Luis (2012), ni vigumu kuthibitisha sura ya viangami kwa kusoma tafiti ambazo tayari zimefanywa na wataalamu wengine.

Maneno ya Kiswahili yanapoambishwa viangami, muundo wa neno asili hubadilika. Hii inapelekea pia kubadilika kwa aina ya neno. Hivyo basi uainishaji wa maneno baada ya kuambishwa kiangami huathirika na utata kutokea. Swali ni je, ikiwa baadhi ya maneno yataunganishwa na kuwa neno moja, kutakuwa na tatizo lolote lile katika uainishaji? Baadhi ya maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kibantu hutiwa mkazo katika silabi ya pili kutoka mwisho. Kwa mfano, katika neno *mama*, mkazo utatiwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho. Ikiwa neno ‘mama’ litaambishwa na kuongezewa kiangami hivyo kuwa na silabi ya ziada, je, mkazo utabaki ulipokuwa au utabadilika? Mtafiti atashughulikia hayo.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudia kutimiza malengo yafuatayo:

1. Kulinganisha uambishaji wa viangami viambishi katika lugha ya Kiswahili.
2. Kuchunguza sheria zinazofuatwa katika uundaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili.
3. Kutathmini mwingiliano uliopo baina ya sifa za kiarudhi na viangami vya Kiswahili.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

1. Je, kuna tofauti gani katika kuambisha viangami na viambishi vya lugha ya Kiswahili?
2. Je, viangami vya Kiswahili huundwa kwa kuongozwa na sheria gani?
3. Je, sifa za kiarudhi zinaingiliana vipi na viangami vya Kiswahili?

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu unachangia pakubwa katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Utafiti wa viangami umefanywa na wanaisimu katika lugha zingine. Baadhi ya sheria na taratibu za uundaji wa viangami hutofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Hivyo basi ni muhimu kushughulikia viangami katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia sheria za kisarufi za lugha ya Kiswahili. Utafiti huu utasaidia wanaisimu kuelewa viangami katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unalenga kukusanya data itakayochanganuliwa na hatimaye kufasiri matumizi ya viangami katika lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, utafiti huu utawafaidi wanaotumia lugha ya Kiswahili kimaandishi na kimaongezi katika shughuli zao za kila siku.

Pia, utafiti huu utawasaidia wanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Wataweza kutambua kuwa kunazo njia mbalimbali za ufupishaji wa maneno. Uundaji wa viangami ni mojawapo wa ufupishaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu utamsaidia mwanafunzi kutumia misamiati iliyo kamili na ile ambayo

imefupishwa na kuambishwa kwa maneno mengine. Hawatakanganyika wanapoyaona maneno yaliyoambishwa na yale yasiyoambishwa. Kwa mfano, wakiona maneno kama vile *twenzetu* na *twende zetu*, wataweza kutambua kuwa maana ni sawa hata kama muundo ni tofauti. Hii itawasaidia kutambua maneno ambayo yamefupishwa na kuwa viangami na hivyo kuwasaidia wasikanganyike hasa wanapohitajika kuunda sentensi ili kuainisha maneno ya Kiswahili.

Wengine watakaonufaika kutokana na utafiti huu ni waandishi wa vitabu vya Kiswahili pamoja na wanafunzi wa somo la Kiswahili wanaovitumia vitabu hivyo. Utafiti huu utawasaidia wanafunzi kutofautisha maneno yaliyoambishwa na yale ambayo yana viangami. Mara nyingi wanafunzi hutunga sentensi ambazo zinawatatiza kuainisha. Kunao waandishi wa vitabu vya kiada wanaochanganya viangami na viambishi. Jambo hili hukanganya wanafunzi hasa wa shule za upili. Kwa mfano, kwa maoni ya Ipara, na wengine (2010), kuna viambishi viulizi. Baadhi ya mifano iliyoelezewa ni kama vile, *wenda<u>pi</u>*. Hapa waandishi wanaainisha kipashio -pi- kama kiambishi kiulizi ilhali -pi- ni kiangami kinachotokana na neno kamili *wapi.* Jambo hili linawakanganya wanafunzi wanaokitumia kitabu hiki katika kudurusu au hata kujifunza upya mada hii ya viambishi. Inatarajiwa kuwa data itakayowasilishwa katika utafiti huu itasaidia pakubwa katika kuendeleza sarufi ya Kiswahili na ambayo itatumika na wanaisimu kuchanganua na kufasiri zaidi matumizi ya viangami katika lugha ya Kiswahili.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ni wa kiisimu. Hii ni kwa sababu kiangami ni kipengele cha kiisimu. Msingi wa utafiti huu ulikuwa ni uchanganuzi wa kimofosintaksia wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Mofosintaksia ni taaluma inayochunguza mwingiliano wa mofolojia na sintaksia (Donna, 2003). Utafiti huu ulishughulikia viangami katika kitengo cha mofolojia na sintaksia kwa undani. Utafiti huu ulishughulikia viangami katika neno, kirai na pia sentensi. Kuna viangami vya aina tofauti lakini katika utafiti huu, mtafiti alishughulikia viangami vinavyoambishwa kabla ya neno kuu na vile vinavyoambishwa baada ya neno kuu. Hii ina maana ya kuwa, viangami vya awali na vya tamati ndivyo vilivyoshughulikiwa. Utafiti huu ulishughulikia matini zilizoandikwa hasa vitabu vya Kiswahili.

Viangami vinaweza kupatikana kwenye usemi halisi na pia usemi wa taarifa. Utafiti huu haukushughulikia usemi halisi kwa undani. Baadhi ya data iliyokusanywa ilijikita katika usemi wa taarifa. Sababu ni kuwa, maandishi kuhusu viangami yalipatikana makatabani na pia mtandaoni. Kauli zilizochapishwa kwenye vitabu na pia kwenye mtandao hukubalika ikilinganishwa na usemi wa mtu halisi.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Hivyo basi, mtafiti alizingatia maandishi kuhusu viangami. Sehemu hii inaweka wazi na kueleza maoni ya wataalamu wengine kuhusiana na viangami. Maoni ya wataalamu hawa yalichangia pakubwa katika mada ya uchanganuzi wa komofosintaksia wa viangami katika lugha ya Kiswahili.

### 1.7.1 Maana ya Kiangami

Kwa mujibu wa Spencer na Luis (2012), kiangami ni kipengele ambacho katika sentensi huchukuliwa kama neno huru kimofolojia na kifonolojia. Kwa mujibu wa Alotaiby na wenzake (2010), kiangami ni kipashio cha isimu kinachotamkwa na kuandikwa kama kiambishi lakini kinajisimamia kisarufi. Katika maelezo ya Spencer na Luis (2012), kiangami kinaundwa kwa maneno mawili au zaidi, hata kama kinatamkwa kama neno moja. Hili ni neno ambalo kifonolojia huambatishwa kwa neno lingine lililo huru. Kiangami huonekana kama kiambishi cha neno kuu. Wanaeleza kuwa viangami huambatishwa kwa neno kuu lililo karibu.

Anderson (2010) anaeleza kiangami kama wazo la kimapokeo la kisarufi. Kwa maelezo yake, kiangami ni neno refu ambalo kilafudhi au kimatamshi si huru ila linategemea neno linalopakana nalo ili liweze kutamkwa. Kulingana na Spencer na Luis (2012), kuna aina tatu za viangami katika lugha ya Kiingereza. Viangami hivi ni:

1. Kiangami awali; Hiki ni kiangami ambacho hutokea upande wa kushoto wa neno kuu.
2. Kiangami tamati; hiki ni kiangami kinachoambatishwa kwa neno kuu upande wa kulia.
3. Kiangami cha kati/ndani; Hiki ni kile ambacho hujipenyeza ndani ya neno kuu.
4. 

### 1.7.2 Utata katika Viangami vya Kiingereza

Spencer na Luis (2012) wanaeleza utata unaozuka katika viangami vya maneno ya Kiingereza. Kuna maneno ambayo yanapoambishwa viangami huwa ni vigumu kuyaainisha. Wanatoa mfano wa neno *Pat* ambalo ni nomino na neno *is* ambalo ni kitenzi. *'s* inakuwa kiangami kinachoambatishwa kwa nomino *pat* na kupata neno *Pat's*. Ni vigumu kuainisha neno *Pat's.*

Ni vigumu kueleza viangami kupitia utafiti uliofanywa na wataalamu wengine kwani viangami na viambishi huwa na matumizi na sifa zinazofanana au zinazokaribiana (Spencer na Luis, 2012). Kwa mfano, Baker, na wengine (1989) wanazua mjadala wa kiambishi *–en-* ambacho katika lugha ya Kiingereza hutumiwa kuonyesha hali ya kuendelea. Kwa mfano,

*2. The vase was brok**en** by Tom*

(Jagi lilivunjwa na Tom)

Hapa, *en* inatumika kama kiambishi lakini waandishi wengine wanazua mgogoro hasa wanapoangalia *en* kwa mtazamo wa lugha zingine kama vile lugha ya Kihispania ambayo inakaribiana kimuundo na lugha ya Kiingereza. Kwa mtazamo wao, sifa muhimu za *en* zinadhihirisha kuwa ni kiangami.

Utata mwingine wanaoeleza Spencer na Luis ni kuwa, wakati mwingine viangami huchukuliwa kama vipashio au maneno yaliyokiuka kanuni za kisintaksia. Hivyo basi, viangami ni vipashio vya kipekee ambavyo ni vigumu kupewa nafasi katika

sentensi kama neno la kawaida. Spencer na Luis wamefafanua baadhi ya dhima ya viangami kama ifuatayo;

1. Viangami vinavyoonyesha tendo. Hivi huonyesha hali ya kitendo, mkazo, ukanushi na pia kuyakinisha, kwa mfano:

   (a) *Harriet's reading (Harriet is reading)*

   Harriet anasoma.

   (b) *Sue'd have complained (Sue would have complained)*

   Sue angelalamika.

2. Viangami vya vishazi. Hivi ni vile vinavyoonyesha vishazi. Kwa mfano:

   *She's.*

   Yeye ni

3. Viangami vya nomino (kiima). Hivi ni viangami vinavyoonyesha matumizi ya kiima kama vile nomino zilizo wazi, kuonyesha umiliki na pia idadi. Kwa mfano katika Hungarian.

   (a) *autó* (gari)

   (b) *autó**m*** (gari langu)

   (c) *autó**ja*** (gari lake)

Kulingana na mfano huu, kuna viangami viwili ambavyo vimetokana na vivumishi vimilikishi. Kiangami –*m*- na kiangami –*ja*-. Neno kuu ni nomino ambayo ni *autó*.

Katika maelezo ya Spencer na Luis (2012), sifa za viangami ni kama vile, viangami havitiliwi mkazo. Pili, viangami huambatishwa kwa neno kuu. Tatu,

viangami havichagui maneno ya kujiambisha kwayo na mwisho ni kuwa mpangilio wake kisintaksia ni tofauti ule wa na neno kamili.

Maelezo ya Spencer na Luis yalichangua sana katika utafiti huu. Baadhi ya mambo yaliyotajwa yalijitokeza katika utafiti. Katika lugha ya Kiswahili, ni vigumu kuyaainisha maneno ambayo tayari yameambishwa viangami. Katika lugha ya Kiswahili, huwezi kutegemea utafiti uliofanywa na watafiti wengine kuhusu viangami. Kwa mfano, kuna watafiti kama vile Spencer na Luis (2012) ambao wameainisha viangami mara tatu, viangami awali, viangami tamati na viangami kati. Katika lugha ya Kiswahili, mzizi wa neno hauvunjwi. Hivyo basi ni vigumu kupata viangami vya kati.

### 1.7.3 Tofauti Kati ya Viambishi na Viangami

Alotaiby na wenzake (2010) wameangalia viangami katika lugha ya Kiarabu. Kulingana nao, viangami katika lugha ya Kiarabu huweza kujiambatisha kwa viangami vingine au pia kwa neno moja kuu. Alotaiby anaeleza kuwa viangami katika lugha ya Kiarabu si vingi kama ilivyo katika baadhi ya lugha. Katika lugha ya Kiarabu kuna uwezekano wa kuwa na viangami hata vinne kabla ya neno kuu na vitatu baada ya neno kuu. Kumbuka kuwa lugha ya Kiarabu huandikwa kutoka kulia hadi kushoto. Mfano huu ni kwa mujibu wa Buckwalter 2004),

| | |
|---|---|
| (a) >f b Al bATI | (?then by false) |
| | Na kwa isiyo sahihi |
| (b) Whb t ny h | (you gave it to me) |

Ulinipa hiyo

(c) B ha (by it)

Kwa hicho

(d) tALLAH (swear by Allah)

Apa kwa jina la Allah

(e) >wstETwnyhA (?and will give you me it)

Na unanipa hiyo?

Tofauti kuu kati ya viangami na viambishi ni kuwa kiangami ni mofimu iliyo na sifa za kisintaksia za neno kamili lakini kifonolojia mofimu hii hutegemea neno jingine ambalo ni neno kuu. Kwa upande ule mwingine kiambishi ni mofimu inayoambishwa kwenye mzizi wa neno ili kuunda neno jipya au kupata maana tofauti. Anderson (2010) ametofautisha viangami na viambishi kwa njia zifuatazo.

1. Viangami vina kiwango cha chini cha uteuzi kutegemea neno kuu lakini viambishi vina viwango vya juu vya uteuzi. Kiangami kinaweza tu kuambishwa kwa neno linalofuata au kutangulia katika sentensi. Kwa mfano,

   Nimemwona mama yangu. Mamangu

   Mwana wangu ni mzuri. Mwanangu

   Kwa huo upande mwingine, si lazima neno linalowakilishwa lifuatane na fungu tenzi husika. Kiambishi huweza hata kutumiwa

kuwakilisha dhana ya neno ambalo haliko katika sentensi. Kwa mfano,

Mama ameleta kiatu - ame**ki**leta

Jana nilifika nikalala. - nili**po**fika nililala

2. Maneno yaliyoambishwa viambishi yana uwezo mkubwa wa kuwa dhana tata kuliko maneno yaliyofungamanishwa na kiangami. Hii ina maana ya kuwa, matumizi ya kiangami yanaeleweka moja kwa moja kaika sentensi ila kiambishi kimoja kinaweza leta utata katika sentensi. Kwa mfano.

    Mama ali**po**simama…

    Kiambishi –po- kinaweza leta dhana ya jinsi alivyosimama, mahali aliposimama au pia wakati aliposimama.
3. Maneno yaliyoambishwa viambishi yanaweza kuwa na muundo wa upekee ukilinganisha na maneno yaliyo na viangami.
4. Maneno yaliyoambishwa viambishi huweza kuwa na maana zaidi ya moja ukilinganisha na maneno yaliyo na viangami. Hii ina maana kuwa kiambishi kimoja kinaweza kuwa na maana nyingi lakini kiangami kinabaki tu kuwa na maana ile moja. Tazama mfano huu,

    Mchezaji alimpigi**i**a mpira.

Kiambishi –i- katika sentensi hii kinaleta maana tofauti. Inaweza kuwa ni mchezaji alipiga mpira kwa niaba ya mtu mwingine, au aliupiga mpira kwa sababu ya mtu mwingine, au iwe ni aliupiga mpira kuelekea kwa mtu mwingine au alipiga mtu mwingine kwa sababu ya mpira.

5. Sheria za kisintaksia zinaweza kuathiri maneno yaliyoambishwa viambishi lakini maneno yaliyo na viangami hayawezi. Viambishi huweza kuleta tofauti za upatanisho wa kisarufi. Nomino inayorejelewa katika sentensi huathiri viambishi vitakavyotumika katika sentensi hiyo. Kwa mfano,

    Pahali ha**pa p**etu ni **pa**zuri.

    Mahali hu**mu mw**etu ni **m**zuri.

    Mahali hu**ku kw**etu ni **ku**zuri.

    Shule hi**i y**etu ni nzuri.

    Soko hi**li l**etu ni nzuri.

    Kulingana na mfana huu, viambishi vinabadilika kutegemea nomino inayotumika.

6. Viambishi vinaweza kuambishwa kwa maneno mengine yaliyo na viambishi vingine tayari lakini katika lugha kama vile Swahili, viangami haviwezi ambishwa kwa maneno yaliyo na viangami vingine. Tazama mfano huu,

    Soma

Som**e**a

Som-**esh-**a

Som**e-a-n-**a

Som**e-sh-e-a-n-**a

Katika mfano huu, kitenzi soma kina uwezo wa kuchukua viambishi vya kauli mbalimbali kwa wakati mmoja.

Katika maelezo yao Akinlabi na Liberman (2000), viangami ni mofimu huru kisintaksia lakini kifonolojia ni tegemezi katika neno kuu. Wanasema kuwa viangami vimepungukiwa kiarudhi kwa njia moja au nyingine. Hii ndiyo maana viangami vinalazimika kutegemea neno kuu. Wameangazia aina sita za viangami katika lugha ya Yoruba. Viangami hivi ni:

1. Kiima kinachodhihirisha toni ya juu ya mofimu.
2. Vinavyotilia mkazo kishirikishi.
3. Kiima kilicho na kiwakilishi.
4. Vishirikishi vya mshangao.
5. Viwakilishi vimilikishi.
6. Vinavyoulizia swali.

Ifuatayo ni baadhi ya viangami katika katika lugha ya Yoruba vinavyoonyesha dhana ambazo tayari zimeorohdeshwa hapo juu,

(a) Viangami vya swali

| | |
|---|---|
| *Ngba;a wa*; | thibitisha, tulikuja? |
| *Aba; a wa;* | tulikuja? |
| *Ngbo;wa*; | thibitisha, alikuja? |
| *Abo;wa;* | alikuja? |

(b) Viangami vya mshangao

| | |
|---|---|
| *Emu o* | kinywaji gani! |

(c) Viangami vimilikishi

| | |
|---|---|
| *O ko o* | gari langu |
| *O ko o re* | gari lako |

Katika viangami vyote vilivyotajwa, silabi ya mwisho ya neno kuu na kiangami kinachochopekwa kwa neno hilo havina toni sawa. Katika lugha ya Yoruba, viangami hutokea pale ambapo irabu inadondoshwa katika kitenzi na kisha kuambatishwa kwa nomino. Njia nyingine ni pale ambapo kitenzi kinakuwa neno kuu nayo nomino inadondosha irabu na kuambatishwa katika kitenzi. Mifano ifuatayo ni ya ziada kwa mujibu wa Akinlabi na Liberman (2000).

| | | | |
|---|---|---|---|
| *3.* | (a) *wa* (T) | *eko* (N) | *Weko* |
| | Tafuta | elimu | tafuta elimu. |
| | (b) *wa* (T) | *ono* (N) | *wono* |
| | Tafuta | njia | tafuta njia |
| | (c) *ji* (T) | *obe* (N) | *jobe* |
| | Iba | kisu | iba kisu |

| | | |
|---|---|---|
| (d) *mu* (T) | *iwe* (N) | *Muwe* |
| Chukua | kitabu | chukua kitabu. |
| (e) *mu* (T) | *iwe* (N) | *muwe* |
| Chukua | kitabu | chukua kitabu |

Katika mfano 3, jozi zote zina mpangilio wa toni ulio sawa. Katika 3 (a) (b) (c), irabu ya kitenzi imedondoshwa. Hii ina maana kuwa kitenzi ndicho kinachofupishwa na kuwa kiangami. Viangami hapa vitakuwa ni (a) *w* (b) *w* na (c) *j*. Nomino inakuwa neno kuu. Hii ni tofauti na 3(d) na (e) pale ambapo irabu ya nomino ndiyo inayodondoshwa. Hivyo basi nomino ndiyo inayokuwa kiangami. Viangami hapa ni (d) *we* na (e) *we*. Kitenzi kinakuwa neno kuu.

### 1.7.4 Mfanano kati ya Viambishi na Viangami katika Lugha ya Degema

Katika lugha ya kidegema, viangami huambishwa kwenye kitenzi cha kwanza na pia kwenye kitenzi cha mwisho katika mfuatano wa maneno. Viangami katika lugha ya Degema huwa na uhuru mkubwa sana wa kuambishwa kwenye vipashio mbalimbali vya mofosintaksia. Kwa kiwango fulani, viangami hivi havina mipaka. Kari (2002b) anasema kuwa viangami na viambishi vinafanana kwa njia nne. Hii ni kwa mujibu wa lugha ya Degema inayozungumzwa Nigeria. Kwanza kuna;

#### (a) Irabu Linganishi

Lugha ya Degema huwa na irabu kumi. Irabu hizi zimeainishwa katika vikundi viwili. Kuna irabu zilizopanuliwa na ambazo hazijapanuliwa.

Irabu zilizopanuliwa. i u

e o

ə

Irabu ambazo hazijapanuliwa. ɪ ʊ

ɛ ɔ

a

Irabu katika maneno sahili hutolewa kwenye kikundi kimoja pekee, yaani kutoka kwa kikundi cha irabu zilizopanuliwa au ambazo hazijapanuliwa. Katika maneno ambatani, irabu hutolea kutoka vikundi vyote viwili. Kwa mfano,

4. *utóm* (kichwa)

*utɔm**

*ʊtɔndỉ* (Taa)

*ʊtondỉ**

*ɔk'ɔdỉ ə'tidə* (Mgurumo wa Radi)

Kulingana na Kari (2002a/b), muundo wa viambishi na viangami huathiriwa na aina ya irabu ya neno ambalo linaambishwa. Ikiwa neno limeundwa kwa irabu inayopanuliwa, basi irabu ya kiangami huwa pia imepanuliwa. Ikiwa irabu zilizopanuliwa zitatokea katika neno moja sahili, neno hilo halitakuwa sahihi kisarufi. Kwa mfano,

*5* *di-ɛn'ɛ* inajikula

*di-en'e**

*e-ŋotú* kiuno

*ɛ-ŋotú

#### (b) Sauti (toni)

Kari (2002) anaeleza ya kwamba, kifonolojia, viambishi na viangami havina toni. Kiasili viambishi na viangami vya Degema havina toni kwa sababu havina sifa binafsi za kiarudhi. Viangami na viambishi vimeunganishwa kiarudhi kwenye mzizi wa neno au neno kuu ili kupata matamshi bora. Kwa mujibu wa Frank na King (2000), viangami vinao udhaifu wa kimatamshi na hivyo kukosa lafudhi kama ilivyo kwa viambishi. Hii ina maana ya kuwa, kifonetiki, viangami ni vipashio tegemezi.

#### (c) Kuambatishwa kwa Neno Kuu au Mzizi

Viangami na viambishi huambatishwa kwenye vipashio ambavyo vinavitegemea kifonolojia na kimofolojia. Hivyo basi viambishi na viangami si vipashio huru. Kwa mfano**, a-na-ye-**soma, viangami vilivyokolezwa vinategemea mzizi wa neno *soma*. Kivyake, viambishi hivi havina maana. Mfano wa kiangami ni kama vile, wakataka**ni**? Kiangami *ni* kinategemea neno kuu *wataka.* Kiangami hiki kikiwa peke yake hakina maana.

#### (d) Sifa za Unyambuaji

Viangami na viambishi huwa na sifa sawa za unyambuaji. Unyambuaji ni utaratibu wa kupanua neno la kimsingi kwa kuongeza kiambishi kabla, katikati au baada ya mzizi wa neno. Katika unyambuaji, viambishi huongezewa kwenye mzizi na kuunda istilahi mpya. Wakati mwingine, uamilifu wa neno hubadilika. Kama vile

shamba (nomino) na shambani (kielezi). Kisarufi, sifa hizi zinahusishwa na viangami/viambishi awali na viangami/viambishi tamati.

### 1.7.5 Tafiti kuhusu Viangami na Mbinu Zilizotumika

Aloitaby na wenzake (2010) walifanya utafiti katika lugha ya Kiarabu. Utafiti wao ulihusu kugawa vifungu vya maneno katika sehemu maalumu yaani, mkato wa maneno. Katika utafiti wao, hatua ya kwanza katika ufupishaji wa matini ni kuigawa matini ile katika vitengo vya kiisimu kama vile maneno, uakifishaji, nambari au hata alfabeti. Katika utafiti wao, nafasi iliachwa ili kutenganisha vipashio mbalimbali. Data iliyotumika katika utafiti huu ilitolewa kwenye kongoo ya maneno ya Kiingereza na Kiarabu. Haya ni maneno ambayo yamekuwa yakikusanywa kwa muda na wanaisimu na yanapatikana kwenye makavazi ya Kiingereza na Kiarabu. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya majedwali na grafu.

Matokeo ya utafiti huu yalioorodhesha baadhi ya viangami vinavyotumika kwa wingi katika lugha ya Kiarabu. Kila kiangami kiolionyeshwa jinsi kilivyotumika na mara ngapi kilitumika. Tazama jedwali lifuatalo,

| **Kiangami (utafsri)** | **Uainishaji** | **Idadi ya mara ya matumizi** | **Asilimia ya matumizi (%)** |
|---|---|---|---|
| *Al#* | Kibainishi | 103,015016 | 57.02 |
| *w#* | Kiunganishi | 31,014,498 | 17.17 |
| *f#* | Kiunganishi | 1,462,196 | 0.81 |
| *l#* | Kihusishi | 11,470,854 | 6.35 |
| *b#* | Kihusishi | 8,857,080 | 4.9 |
| *k#* | Kihusishi | 737,638 | 0.41 |

Jedwali 1.1. limetokana na utafiti uliofanywa kuonyesha matumizi ya viangami vya kiarabu. Kulingana na Aloitaby na wenzake (2010), data huenda ikawa si sahihi kikamilifu.

### 1.7.6 Maana ya Mofosintaksia

Mofosintaksia huhusisha vipashio vya kimofolojia ambavyo uamilifu wake hubadilika katika sintaksia kama vile umoja, wingi, uyakinishi, ukananushi na mnyambuliko. Mofosintaksia ni jina jingine la sarufi. Mofolojia ni uchunguzi wa maneno na uundaji wake. Sintaksia ni uchunguzi wa sentensi na njia mbalimbali za kuunda sentensi.

Mofolojia hushughulikia uchambuzi wa mfumo wa maneno katika lugha. Haya ni kulinga na Massamba (1999). Kila lugha huwa na utaratibu wake wa kuunda maneno. Wanaeleza sintaksia kama uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika

sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Katika utafiti huu, mpangilio wa maneno yaliyo na viangami uliangaziwa kwa kina.

Maandishi haya yote yalirejelewa katika utafiti huu. Maandishi haya yalikuwa na umuhimu kwani yalimwongoza mtafiti kutimiza malengo yake. Malengo yenyewe yalikuwa ni kubainisha tofauti ya viambishi na viangami, kuchunguza sheria zilizotumika kuunda viangami vya Kiswahili na hatimaye kutathmini mwingiliano wa sifa za kiarudhi na viangami katika lugha ya Kiswahili. Ili kufanikisha utafiti huu, nadharia mwafaka ilihitajika. Sehemu inayofuata inahusu nadharia iliyotumiwa kumwongoza mtafiti katika utafiti huu.

## 1.8 Nadharia Boreshaji/Umbo Upeo

Utafiti huu unalenga kuweka wazi uchanganuzi wa kimofosintaksia wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ni wa kiisimu hivyo basi utaongozwa na nadharia ya kiisimu. Nadharia iliyotumiwa katika utafi huu inaitwa nadharia boreshaji. Kwa mujibu wa Massamba (2011), nadharia boreshaji pia huitwa nadharia ya fonolojia umbo upeo (UU). Nadharia hii ilipendekezwa na Prince na Smolensky (1993). Kwa mujibu wa Polyplossia (2013), nadharia hii hutumika kusuluhisha matatizo ya kifonolojia na pia kuelezea tofauti zinazopatikana katika lugha zote. Polyplossia anasisitiza kwamba, badala ya kuunda sheria mpya za kiisimu kila wakati, ni heri sifa bia za lugha zitumiwe kama miundo rasmi.

Kwa mujibu wa Massamba (2011), lengo la kuanzisha nadharia hii ni kushughulikia masuala ya kifonolojia yaliyojitokeza katika sheria za muundo wa

mofimu. Baadaye nadharia hii ilitumiwa kushughulikia maswala ya kiisimu kama vile mofolojia na sintaksia.

Massamba anazidi kueleza kuwa, katika nadharia ya umbo-upeo, umbo la ndani huchukuliwa kama malighafi au kama umboghafi. Umbo la nje huchukuliwa kama umbotokeo. Kulingana na nadharia hii, lugha yoyote ile inaweza kupokea maumboghafi yoyote na pia kutoa maumbotokeo ya aina yoyote ile.

### 1.8.1 Misingi ya Nadharia ya Umbo Upeo

Nadharia hii ina misingi mitatu. Msingi wa kwanza ni ZALI (zalishi). ZALI huchukua ujumbe na kuunda orodha ya matokeo yanayowezekana. Nayo MASHA-ZU (Mashartizuizi) inatoa mwelekezo kwa muundo unaotoa masharti yanayodhibiti na kutumia sheria. THATHI (Tathmini) nayo inachagua kundi linalofaa la uboreshaji kwa mujibu wa vidhibiti vilivyowekwa.

#### 1.8.1.1 ZALI

Huu ni ufupisho wa neno zalishi. Hiki ni kipengele kinachozalisha maumbotokeo mbalimbali katika lugha yanayoitwa maumboshindani. Yanaitwa maumboshindani kwa vile ndani ya maumbo hayo kuna umbo linalofikia upeo wa kukubalika. Jambo linaloshughulikiwa katika nadharia hii, ni lile umbokati la maumbotokeo ambayo yote ni maumboshindani. Kwa mujibu wa Prince na Smolenksy (1993), umbo linaloshinda ndilo limefikia upeo wa ukubalifu. Umbo hili linaweza kuwa limevunja mashartizuizi ya kiwango cha chini yanayovumilika. ‘Katika nadharia

hii lugha yoyote ile inaweza kuingiza katika sarufi yake maumboghafi yasokikomo,' (Massamba, 2011: 250).

#### 1.8.1.2 MASHA-ZU

Huu ni ufupisho wa neno mashartizuizi. Kipengele hiki kinahusika na kuweka vigezo na masharti yasiyoweza kuvunjwa na yanayoweza kuvunjwa. MASHA-ZU huwa na jukumu la kuchagua maumbotokeo. MASHA-ZU huweka vigezo ambavyo hutumika katika kuamua ni umbo lipi linalofikia upeo wa ukubalifu. Umbotokeo lipewalo ushindi ni lile ambalo halijavunja masharti yoyote au limevunja masharti ya hadhi ya chini na ambayo yanavumilika.

#### 1.8.1.3 TATHI

Kipengele hiki huwa na jukumu la kuamua umbo ambalo limefikia upeo wa kukubalika kati ya yale maumbo yaliyopo. TATHI hutimiza haya kwa kuangalia ni memba yupi kavunja mashartizuizi muhimu mengi na yupi kavunja machache.

Katika nadharia boreshaji kila sheria ni bia. Sheria hizi zinafanana katika kila lugha. Sheria hizi huweza kutabiri tanzu za lugha. Lugha za binadamu hutegemea sheria zilizopo. Si rahisi kutofautisha sarufi zote kwani si kila sheria inaweza kukubalika katika kila sarufi. Lugha mbili zinaweza kuwa na sheria tofauti ambazo hazipingani lakini zikawa na matokeo sawa.

Misingi hii mitatu itasaidia kufanikisha utafiti huu. Viangami ni vipashio vinavyojitokeza katika lugha nyingi ulimwenguni, hivyo basi vina sifa bia. Katika lugha ya Kiswahili, viangami vinaweza kujiambatisha kwenye mzizi wa neno au

neno kamili. Hata hivyo kunayo maneno yanayokubali na mengine yanayokataa kuambatishwa na viangami fulani. Kwa mfano;

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| *6* | *Mama* | + | *yake* | = | *mamaye* |
| | | | | | *mamake* |
| | *shangazi* | + | *yake* | = | *shangaziye* |
| | | | | | *shangazike** |
| | *baba* | + | *yake* | = | *babaye* |
| | | | | | *babake* |
| | *mwenzi* | + | *wake* | = | *mwenziwe** |
| | | | | | *mwenzike** |

Kulingana na mfano 6, kuna njia mbili za kupata kiangami kutokana kwa kimilikishi –**ake.** Katika njia ya kwanza,sauti za kati –ak- zinakatwa na umbotokeo linaloonekana haliathiriwi na mashartizuizi. Katika njia ya pili, silabi ya kwanza ya kimilikishi ndiyo inayokatwa na kudodoshwa. Silabi ya pili inatumika kama kiangami.

### 1.8.2 Mihimili ya Nadharia ya Umbo Upeo

Kwa mujibu wa Massamba (2011), nadharia hii ina mihimili minne. Mihimili hii ni, umajumui, ukiukwaji, upangiliaji MASHAZU na usambamba.

#### 1.8.2.1 Umajumui

Nadharia hii inadai kuwa MASHA-ZU ni sifa ya kimajumui na hupatikana katika sarufi zote za lugha. Kila nadharia inafaa kuchunguza, kugundua na hatimaye kueleza vile sifa za kimajumui hujitokeza katika lugha ya binadamu. Umuhimu wa nadharia yoyote huwa ni kuchunguza na kutambua sifa za kimajumui zilizo katika lugha. Sifa hizi hulenga sarufimajumui. Kulingana na nadharia ya umbo upeo, sarufimajumui ina seti za MASHAZU ya kimajumui.

### 1.8.2.2 Ukiukwaji

Mashartizuizi ni ya kimajumui. Kufuata au kutofuata mashartizuizi ya kimajumui kunategemea lugha husika. Hii ni kusema kuwa sheria iliyo na nguvu katika lugha moja yaweza kukosa nguvu katika lugha nyingine. Kwa mujibu wa nadharia hii mashartizuizi hutegemea lugha husika na hata kama mashartizuizi haya yatakiukwa, ukiukaji huo utakuwa wa kiwango kidogo.

### 1.8.2.3 Upangiliaji

Mashartizuizi huwa na mpangilio unaofuata nguvu na uhafifu wa masharti hayo. Ukiukaji wa masharti ukizidi sarufi hukosa kukubaliwa. Ili kukubalika, wanaisimu huwa wanaangalia ni mambo yapi yanayoweza kuvunjwa lakini yakakubalika katika sarufi ya lugha husika. Kila lugha huwa na mpangilio maalumu wa mashartizuizi. Sauti hupangwa na kuunda silabi. Silabi nazo hupangwa na kuunda neno. Maneno tofauti hupangwa na kuunda sentensi. Katika lugha ya Kiswahili, maneno mengi huundwa na silabi wazi. Silabi wazi ni zile zinazoishia kwa irabu. Hata hivyo, kuna silabi chache ambazo ni funge, zinazoishia kwa konsonanti.

### 1.8.2.4 Usambamba

Kulingana na Massamba (2011), utoshelezi wa kimpangilio wa mashartizuizi huangaliwa kwa kutazama jinsi seti nzima ya maumbotokeo inavyojidhihirisha katika mpangilio wote kwa ujumla. Nadharia hii inachukulia kuwa kila lugha huwa na uwezo wa kupokea maumboghafi ya aina yoyote. Hii ina maana ya kuwa, hakuna ukomo wakupokea maumboghafi.

Nadharia hii ilifaa sana katika utafiti huu kwani ilisaidia katika kuchambua sifa za viangami vya Kiswahili na vile vya lugha nyingine ulimwenguni. Pia, nadharia hii ilisaidia katika kufumbua fumbo la kuwepo kwa maneno yanayokubali kuambatishwa na viangami vya aina fulani lakini mengine yanakataa. Ili kupata umbo linalokubalika, mtafiti aliongozwa na mashartizuizi kadha.

Kwa mujibu wa Kager (2004), lengo la nadharia ya kiisimu ni kutoa mwanga wa kiini cha kanuni ambazo zinafanana katika lugha zote. Kimsingi, nadharia ya umbo upeo imejikita katika wazo kuwa kila sarufi ya lugha inao mfumo wa nguvu ambazo hazikubaliani. Nguvu hizi zimejumuishwa katika mashartizuizi ambayo huweka wazi mahitaji ya vipengele vya umbotokeo kisarufi. Mashartizuizi yenyewe huwa na mgogoro. Hii ina maana ya kuwa, kukubalika kwa shartizuizi moja kunapelekea kukiukwa kwa shartizuizi lingine. Hakuna umbo ambalo lina uwezo wa kukubali mashartizuizi yote kwa wakati huo huo.

### 1.8.3 Mashartizuizi ya Umbo Upeo

Nadharia ya umboupeo imetambua aina mbili za mashartizuizi. Kuna mashartizuizi ya uziada na mashartizuizi ya uadilifu (Kager, 2004). Kila aina ya mashartizui hutathmini kipengele mahususi cha umbotokeo. Kwanza tutaangalia mashartizuizi ya uziada kisha tutaangalia yale ya uadilifu.

#### 1.8.3.1 Mashartizuizi ya Uziada

Kulingana na mashartizuizi ya uziada, kama ilivyoelezwa katika nadharia ya umbo upeo, baadhi ya sarufi huhitaji kufanya mabadiliko fulani kwenye maumboghafi ili

maumbotokeo yakubalike kwa wasemaji wazawa wa lugha husika. Familia ya mashartizuizi ya uziada hulifanya umbo linalohusika lifikie kilele cha ukubalifu kwa jamii husika.

Katika utafiti huu, mtafiti aliangazia baadhi ya mashartizuizi ya uziada na jinsi yalivyokiukwa katika baadhi ya mifano ya viangami. Mashartizuizi haya ni kama vile:

1. **Kilele** Kila silabi iwe na kilelel/kiini.
2. **H-KODA** Silabi haifai kuishia kwa koda.
3. ***II:** Irabu mbili hazifai kufuatana.
4. ***$KKK_B$:** Hakuna mfuatano wa konsonanti tatu halisi.
5. ***$NI**: Nazali iliyo na sifa za usilabi haiwezi kufuatwa na irabu.
6. **KYI:** Ni sawa kwa konsonanti kufuatwa na kiyeyusho kisha irabu.
7. ***KYK:** Kiyeyusho hakiwezi kutokea katikati ya konsonanti mbili.
8. ***$N_mI_{jn}$+K:** Kiambishi kinachoanza kwa nazali ya midomo na irabu ya juu nyuma hakiwezi kufuatwa na konsonanti halisi.
9. ***Yk:** Hakuna mfuatano wa kiyeyusho na konsonanti halisi.

#### 1.8.3.2 Mashartizuizi ya Uadilifu

Katika maelezo yake Kager (2004), mashartizuizi ya uadilifu yanahitaji maumbotokeo yahifadhi sifa za kimsingi za misamiati husika. Kulingana na mashartizuizi ya uadilifu, maumbotokeo yanafaa kuwa yafanana na maumboghafi. Mifano ya mashartizuizi ya uadilifu ni:

(a) Lazima maumbotokeo yahifadhi sehemu zote zilizo katika umboghafi.

(b) Ni lazima mpangilio wa vipashio katika umbotokeo ufanane na ule wa umbogafi.

(c) Vipashio vyote vya umbotokeo vifanane na vile vya umboghafi.

(d) Kimatamshi, lazima kuwe na mfanano kati ya umboghafi na umbotokeo.

Mashartizuizi ya uadilifu yanatilia mkazo matamshi ya umbotokeo. Mashartizuizi ya uadilifu huwa na jukumu la kuhifadhi sifa za kimsingi za msamiati. Miongoni mwa mashartizuizi yaliyotumika katika utafiti huu ni yafuatayo:

**FIKI-UKO:** Huu ni ufupisho wa Fikia Ukomo. Sharti hili huweka ukomo wa kiwango cha udhahania kati ya umboghafi na umbotokeo. Kulingana na shartizuizi hili, kila kipande sauti cha umboghafi kinahitajika kijitokeze katika umbotokeo. Shartizuizi la FIKI-UKO linazuia udondoshaji wa kipande sauti chochote kile kilicho katika umboghafi.

**TEGE :** Shartizuizi hili huweka ukomo wa kiwango cha udhahania kati ya umboghafi na umbotokeo. Kulingana na TEGE, kila kitamkwa katika umbotokeo kinafaa kuwa katika umboghafi.

**SHABI-JI:** SHABI ni ufupisho wa neno shahibihiana. Sharti linahusiana na matamshi. SHABI-JI huzuia mabadiliko katika utamkaji wa umboghafi na umbotokeo.

**SHABI-SI:** Kulinga na sharti hili, ni lazima kuwe na mfanano katika sifa za vipande sauti vya umboghafi na umbotokeo.

**PATANA** Sharti hili lina maana ya kukubaliana na masharti. Kwa mujibu wa sharti hili, ikiwa kiambishi awali kinaanza kwa konsonanti ambayo ni hafifu, basi mzizi lazima uwe na konsonanti ghuna.

Aina zote mbili za mashartizuizi zinahusu maumbotokeo. Nadharia hii ya umboupeo haina mashartizuizi ambayo yanahusiana na umboghafi.

Hii itakuwa nadharia muhimu sana katika utafiti huu kwani imeweza kushughulikia maswala muhimu katika isimu yakiwemo fonolojia, mofolojia na pia sintaksia.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii ilishughulikia mbinu za usampulishaji, uteuzi wa sampuli, mbinu za kukusanya data, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), sehemu ya mbinu za utafiti hueleza mbinu zitakazotumiwa na mtafiti kufanikisha utafiti. Sehemu hii inashughulikia mbinu za usampulishaji, uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji wa data, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data na hatimaye uwasilishaji wa matokeo. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani na pia nyanjani. Mtafiti alirejelea machapisho mbalimbali yanayohusiana na viangami pamoja na kuangalia mtazamo wa wanajamii.

### 1.9.1 Mbinu za Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuchagua kitu kimoja kati ya vingi. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika. Baadhi ya makala yaliyotumika yalikuwa yameteuliwa kimaksudi ili kusaidia kupata data inayohitajika. Maandishi yanayofafanua na kueleza kuhusu viangami yaliteuliwa kimaksudi ili kumsaidia mtafiti kuwa na uhuru wa kupata data anayokusudia. Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), uteuzi maksudi wenye upeo wa kutofautiana ulimwezesha mtafiti kuchagua data iliyomsaidia kuchanganua mada yake kwa undani. Makala yaliyochapishwa katika lugha ya Kiswahili yalitumika. Pia maandishi ya kishairi yalitumika.

### 1.9.2 Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), uteuzi wa sampuli ni utaratibu unaotumiwa na mtafiti kukusanya watu, vitu au mahali pa kufanyia utafiti. Mtafiti

huteua kikundi cha watu ambao huwakilisha sifa za jamii lengwa. Kwa maoni yao Kombo na Tromp (2006), sampuli ni idadi ndogo ya watu au vitu inayochaguliwa na mtafiti kwa lengo la kuwakilisha jamii lengwa katika utafiti anaofanya. Kikundi kitakachochaguliwa kitatumika katika shughuli ya utafiti ili kupata sampuli lengwa. Mtafiti alichagua kikundi fulani cha utafiti kimaksudi ili aweze kufanya utafiti wake moja kwa moja. Uteuzi wa kimaksudi katika utafiti huu ulimsaidia mtafiti kupata sampuli ya utafiti huu. Data iliteuliwa kutoka kwa machapisho katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alifanya utafiti wake kwa kuangalia viwango tofauti vya sampuli yake. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003), sampuli iliyoteuliwa inastahili kuwa asilimia thelathini ya kundi jumuishi.

### 1.9.3 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Buliba na wengine (2014), data ndiyo malighafi ya utafiti. Hivyo ni muhimu kwa kila mtafiti kukusanya data yake kwa njia inayofaa. Katika utafiti huu, mbinu ilizotumika kukusanya data ni ya kusoma na kunukuu.

### 1.9.4 Kusoma na Kunukuu

Mtafiti alijihusisha na kusoma makala ya viangami makatabani na pia mtandaoni. Kunayo maandishi yanayohusiana na viangami kwenye mtandao na pia kwenye vitabu vilivyochapishwa. Baadhi ya vitabu vilivyoteuliwa na mtafiti ni kama vile, Robert (1967), Muguti (1989), Mulokozi (1999) na Ipara, Burudi na Wakio (2010). Baadhi ya wataalamu wa isimu wamefanikiwa kuangazia viangami katika lugha mbalimbali. Mtafiti aliangazia mbinu zilizotumiwa na watafiti wengine ili

kupata data. Hii ilirahisisha shughuli hii ya utafiti kwani makala hayo yanapatikana kwa urahisi.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Kombo na Tromp (2006), uchanganuzi wa data ni kule kuchunguza kwa kina data iliyokusanywa katika utafiti ili kuweza kuifahamu. Uchanganuzi katika utafiti huu ulihusu kuweka wazi data iliyokuwa imekusanywa kwa msingi wa nadharia ya umbo upeo. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo kulingana na malengo ya utafiti huu ambayo ni kuchanganua viangami vya lugha ya Kiswahili kimofosintaksia. Kwa maelezo, mtafiti aliweka wazi tofauti zilizopatikana kati ya viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alieleza sheria na utaratibu unaofuatwa katika uundaji wa viangami vya Kiswahili. Uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika pale ambapo maneno yaliyotumika yalichunguzwa kulingana na mihimili iliyowekwa wazi na Prince na Smolensky (1993) katika nadharia boreshaji ambayo ni umajumui, ukiukwaji, upangiliaji MASHAZU na usambamba. Uchanganuzi wa yaliyomo ulieleza mfumo wa data iliyoandikwa au kutamkwa kuhusiana na viangami. Data iliyokusanywa ilipangwa kulingana na malengo ya utafiti. Baada ya kupanga data mtafiti aliichanganua na kuiainishwa kwa mujibu wa utafiti.

### 1.9.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Kuwasilisha data ni kuelewa data itakayochanganuliwa, kuieleza na pia kuifasiri. Haya ni kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003). Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Mtafiti alieleza kwa muktasari

matokeo yake ambayo yalielezwa na kufasiriwa kwa maelezo ya kinathari, majedwali na michoro.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii ndiyo iliyotanguliza tasnifu ya utafiti huu. Mambo yaliyozingatiwa katika sura ya kwanza ni kama vile: usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua data, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu viangami, misingi ya nadharia ya umbo-upeo na hatimaye mbinu za utafiti. Sura inayofuata ni sura ya pili. Hii ni Sura ambayo inashughulikia lengo la kwanza la utafiti ambalo ni kulinganisha uambishaji wa viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili.

# SURA YA PILI

# UAMBISHAJI WA VIANGAMI NA VIAMBISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti analinganisha na kulinganua uambishaji wa viangami na viambishi vya lugha ya Kiswahili. Sura hii imeanza kwa kueleza mofolojia ya Kiswahili. Suala la jinsi ya kuambisha viangami na viambishi limeshughulikiwa kwa upana. Hapa, mtafiti ameshughulikia maumbo mbalimbali ya vipashio hivi viwili. Mtafiti pia ameainisha viangami na viambishi vya lugha ya Kiswahili. Katika sura hii, mifano kadha imetolewa ili kuelezea dhana hizi. Mifano hii itatumika kujenga msingi wa utafiti huu. Viangami na viambishi hupatikana katika lugha nyingi ulimwenguni. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umbo upeo. Kwa mujibu wa nadharia ya umbo upeo, kunayo mashartizuizi ya kimajumui yanayopatikana katika lugha zote za binadamu. Utafiti unawezesha mtafiti kugundua sifa za kimajumui zilizomo katika dhana za kiangami na kiambishi.

## 2.2 Mofolojia ya Kiswahili

Dhana ya mofolojia imeshughulikiwa na wanaisimu kama vile Hartman na Stork (1972), Matthews (1974) na Mgullu (2001). Neno ‘mofolojia’ limetoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza ‘morphology’. Mofolojia ni tawi la isimu linalojishughulisha na uchambuzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofimu mbalimbali ili kuunda maneno yenye maana katika lugha (TATAKI, 2013). Muthooka (2016) anaeleza mofolojia kama somo au tawi la isimu

linalochunguza maumbo ya maneno na aina zake. Hili ni tawi la isimu linaloshughulikia kipashio cha neno. Mofolojia huchunguza maneno na aina zake kwa lengo la kuelewa maumbo ya maneno yalivyo (Mgullu, 2001). Dhana muhimu katika uchambuzi wa mofolojia ni mofu, alomofu na mofimu. Katika sura hii, mofimu ndiyo dhana itakayoangaziwa zaidi. Katika utafiti huu, viangami vilichanganuliwa kimofolojia. Utafiti huu uliangazia dhana ya viangami kwa kuangalia maana ya neno baada ya kuambishwa kiangami, maumbo mbalimbali ya viangami pamoja na uamilifu wa kiangami katika neno kuu. Maneno yanayofupishwa na kuwa kiangami huwa ni ya aina tofauti. Kwa mfano,

| **7.** | **Kiangami** | **Aina ya Neno** | **Neno Lililoambishwa** |
|---|---|---|---|
| | (a) -ni- (nini) | kiwakilishi | watakan*i?* |
| | (b) -ye- (yake) | kivumishi | hatima*ye* |
| | (c) -mcha- (mchana) | kielezi | chamcha |
| | (d) -mi- (mimi) | kiwakilishi | nami |

Kulingana na Mfano 7, maneno yaliyofupishwa na kisha kuambishwa kwa neno kuu kama viangami ni ya aina mbalimbali. Katika mfano (a) na (d) viangami vinatokana na viwakilishi. Mfano (b) unatokana na kivumishi nao mfano (c) unatokana na kielezi.

Mofolojia imejigawa katika matawi mawili: Mofolojia ya minyambuliko ya maneno na mofolojia ya uundaji wa maneno (Mgullu, 2001). Katika mofolojia ya minyambuliko ya maneno, neno hurefushwa kwa kuongezwa vipashio vya kisarufi kama vile kiambishi kwenye mzizi wa neno. Vipashio hivi huwakilisha dhana

mbalimbali za kisarufi. Minyambuliko ya maneno haibadilishi aina ya neno na mzizi wa neno. Lengo la minyambuliko si kupata neno jipya bali ni kuongeza maana ya kisarufi katika neno hilo. Mofolojia ya minyambuliko pia huitwa mofolojia ambishi kwa vile vipashio hupachikwa na kuongezwa kwenye mizizi ya maneno na kuzalisha maneno ya ziada yenye maana mbalimbali.

Kwa kutumia vitenzi viwili, *piga* na *soma*, vipashio mbalimbali vya unyambuaji vinadhihirika. Jedwali 2.1 linaonyesha mnyambuliko wa vitenzi katika kauli tofauti tofauti.

**Jedwali 2.1 Mnyambuliko wa Vitenzi**

| **Mzizi** | **Tenda** | **Tendewa** | **Tendwa** | **Tendea** | **Tendesha** | **Tendeshwa** | **Tendeshea** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| -pig- | pig-a | pig-*iw*-a | pig-*w*-a | pig-*i*-a | pig-*ish*-a | pig-ish-*w*-a | pig-*ish*-i-a |
| -som- | som-a | som-*ew*-a | som-*w*-a | som-*e*-a | som-*esh*-a | som-*esh*-w-a | som-*esh*-e-a |

Kulingana na Jedwali 2.1, viambishi vya mnyambuliko wa vitenzi vinatokea baada ya mzizi wa neno. Mzizi wa neno unaonekana kuathiri viambishi vya mnyambuliko hasa kwa upande wa irabu inayoongezewa. Katika kauli ya kutendea, kiambishi cha mnyambuliko kinaweza kuwa –*i*- au –*e*-. Neno *pig*-a, ambalo mzizi wake una irabu *i*, kiambishi chake cha mnyambuliko pia kinakuwa na irabu *i*. Kitenzi *som-a* ambacho mzizi wake una irabu *o*, kiambishi cha mnyambuliko kinachukua irabu *o*. Maneno yanayonyambuliwa yanabaki kuwa vitenzi.

Kila lugha hufuata utaratibu fulani katika kunyambua vitenzi. Katika mnyambuliko wa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili, viambishi vya mnyambuliko huongezwa baada ya mzizi lakini kabla ya kiishio. Maneno mawili yaliyonyambuliwa hapo juu (*piga* na *soma*) ni vitenzi. Hata baada ya maneno haya kunyambuliwa katika kauli mbalimbali, maneno mapya yanabaki kuwa vitenzi na pia maana asili haibadiliki.

Mofolojia ya uundaji wa maneno huangazia jinsi maneno mapya yanavyoundwa katika lugha. Viambishi mbalimbali huweza kuongezwa kwenye mzizi wa neno na kuunda neno jipya. Neno jipya linalopatikana linaweza kuwa la aina tofauti na lile la awali. Kwa mfano, kutokana na mzizi *–som-*, tunaweza tukapata maneno mbalimbali.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **8.** | (a**)** | **Som**a | - | Kitenzi |
| | (b**)** | **Som**o | - | Nomino |
| | (c) | M**som**i | - | Nomino |
| | (d) | Ku**som**a | - | Kitenzi au nomino |

Mzizi *–som-*, unapoongezewa viambishi mwanzoni na pia mwishoni, tunapata maneno mbalimbali. Hata kama kiasili mzizi wenyewe ni wa kitenzi, maneno mapya yanayoundwa si lazima yawe kitenzi. Mgullu (2001) anaeleza kuwa uainishaji wa maneno katika lugha hutegemea vigezo vitatu. Vigezo hivi ni maana ya neno, maumbo ya maneno na uamilifu wa maneno katika sentensi. Kulingana na uainishaji wake Mgullu, lugha ya Kiswahili ina aina nane za maneno; Nomino, Kiwakilishi, Kivumishi, Kielezi, Kitenzi, Kihusishi, Kiunganishi na Kihisishi.

Maneno katika lugha ya Kiswahili yamewekwa katika kategoria mbili. Kuna kategoria ya maneno yanayoambishwa na yale yasiyoambishwa. Kiswahili ni lugha ambishi, hivyo basi maneno yanayoambishwa ni mengi ikilinganishwa na yale yasiyoambishwa (Mgullu, 2001). Maneno yasiyoambishwa hayaongezewi viambishi. Baadhi ya maneno yasiyoambishwa ni kama vile, nomino (kaka, shangazi, ndugu na samaki), vivumishi (shujaa, fisadi, karimu, safi na stadi), viwakilishi (mimi, sisi, yeye, wao, wewe na nyinyi), vielezi (sana, mno, daima, shaghalabaghala na wima), viunganishi (seuze, lakini, bali, wala na ingawa) vihisishi (ebo, ala, kefule! na lo!), vitenzi vishirikishi (ni, si, yu) na vihusishi (katika, tangu, kwa na hadi).

Kuambisha ni kuongeza au kubandika kitu cha ziada kwenye kitu kingine. Baada ya utafiti, huu ni wazi kuwa kuna vipashio viwili vinavyoambishwa katika maneno ya Kiswahili, hivi ni kiambishi na kiangami.

Katika shughuli ya kuambisha maneno, kuna vipashio viwili muhimu, mzizi wa neno au neno kuu na kiungo kinachoambishwa ambacho huweza kuwa kiangami au kiambishi. Mzizi ni sehemu ya neno inayobakia mara baada ya kuondoa viambishi vyote vya awali na tamati katika neno. Mzizi huwa ndiyo sehemu muhimu zaidi katika kila neno kwani huwa kama muhimili wa neno (Mgullu, 2001). Neno kuu ni neno lililokamilika kimaana na kisarufi na linaweza kujisimamia kifonolojia na pia katika sentensi. Neno hili huongezewa kiangami bila kubadilisha maana ya kisarufi iliyokusudiwa.

Kwa mujibu wa TATAKI (2013), mzizi ni umbo la kimsingi la neno ambalo ndilo kiini cha neno na ndilo hutumika pia kama msingi wa kuundia maneno mengine yanayohusiana nalo. Kwa mfano, kutokana na mzizi –*toto* tunapata maneno kama vile, *m-toto*, *ki-toto, wa-toto, vi-toto* na *ma-toto.*

Mgullu ameainisha aina mbili za mizizi. Kuna mzizi huru na mzizi tegemezi. Mizizi huru huweza kusimama peke yake na kukamilika kimaana bila kuambishwa chochote. Mifano ya mizizi huru ni kama vile *nyanya, sungura, nyumba* na *meza*. Kwa ule upande mwingine ni sharti mizizi tegemezi iambishwe ili iwe na maana. Kwa mfano –chez- ni mzizi tegemezi. Ili tupate maana mbalimbali za kisarufi, viambishi awali na tamati huongezwa na hivyo kupata maneno kama vile wana*chez*a, *mchez*o, ku*chez*a na kadhalika.

## 2.3 Kuambisha Viangami na Viambishi

Shughuli ya kuambisha vipashio vya kisarufi hufanywa kwa uangalifu mkubwa sana. Katika lugha ya Kiswahili, kiambishi na kiangami ndivyo vipashio viwili vinavyoambishwa kwa neno kuu au hata mizizi wa neno. Baada ya utafiti, imebainika kuwa, uambishaji wa viangami na viambishi unafanana na pia kutofautiana kwa njia mbalimbali. Utafiti huu uliweza kubaini tofauti zinazopatikana wakati wa kuambisha viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili.

### 2.3.1 Maumbo ya Viangami na Viambishi

Viambishi na viangami vya lugha ya Kiswahili huchukua maumbo mbalimbali. Hii ina maana kuwa vipashio hivi viwili hudhihirisha sura tofauti tofauti vinapotenganishwa katika neno. Maumbo ya vipashio hivi huweza kuwa na sauti moja, mbili au hata zaidi kutegemea dhana inayowakilishwa. Maumbo ya viangami na viambishi vya lugha ya Kiswahili huweza kufanana na pia kutofautiana kimuundo. Tazama mfano huu

9. **Viambishi**

(a) *A-na-ye*-**som**-*a*

(b) *Wa-na-o*-**som**-*a*

(c) *Ki-li-cho*-**som**-*w-a*

(d) *I-li*-**som**-*ek-a*

**10. Viangami**

(a) **binti**-*ye*

(b) **wataka**-*ni*

(c) **dada**-*ke*

Kulingana na mifano hii, viangami na viambishi vya lugha ya Kiswahili huchukua maumbo mbalimbali. Kunayo maumbo ya viambishi yanayofanana na yale ya viangami katika lugha ya Kiswahili lakini maumbo mengine yanapatikana katika viambishi pekee ila hayapatikani katika viangami. Katika sehemu inayofuata, mtafiti anashughulikia maumbo haya kwa undani. Kwanza mtafiti alishughulikia

maumbo ya viambishi vya lugha ya Kiswahili kama ilivyoainishwa na wanaisimu mbalimbali. Pili, mtafiti aliyashughulikia maumbo mbalimbali ya viangami kama ilivyopatikana wakati wa utafiti. Sehemu inayofuata imeweka wazi baadhi ya maumbo ya viambishi katika lugha ya Kiswahili.

### 2.3.2 Maumbo ya Viambishi

Kwa mujibu wa Ipara na wengine (2010), viambishi ni mofimu zinazoambatishwa kwenye mzizi wa neno ili kutoa maana tofauti tofauti. Viambishi vikiwa peke yake havina maana isipokuwa ile maana ya kisarufi. Viambishi hupata maana kamili ikiwa vitapachikwa kwenye mzizi wa neno.

Viambishi vinavyopachikwa kwenye mzizi wa neno huonekana kuchukua maumbo mbalimbali. Hii hutegemea maana ya kisarufi ya kiambishi kile na pia matumizi yake katika neno lile. Mgullu (2001) ameelezea maumbo ya viambishi kama yafuatayo;

11. (a) Viambishi vinavyoundwa kwa herufi moja. Kwa mfano:

| | |
|---|---|
| *m*-*ke* | (umoja) |
| Ali-*m*-pig-a | (mtendwa) |
| Pig-*i*-a | (kauli ya kutendea) |

(b) Viambishi vya konsonanti mbili kama vile:

| | |
|---|---|
| *mw*-alimu<br>*KK* | (umoja) |
| *vy*-akula<br>*KK* | (wingi) |

(c) Viambishi vya silabi moja kama vile:

A – *li*-*ye*-*ni*-pig-a (wakati, kirejeshi na mtendwa)
KI-KI-KI
*Ki*-*ku*-lacho (ngeli na mtendwa)
*KI -KI*

(d) Viambishi vya irabu, konsonanti na konsonanti.

Som – *esh*-a (kauli ya kutendesha)
IKK
Pig- *ish*- *a*
IKK

(e) Viambishi vya irabu moja kama vile,

Pig-*i*-*a* (kauli ya kutendea na kiishio)
I
Fung-*u*-a (kauli ya kutendua)
I

Hayo ni baadhi ya maumbo ya viambishi katika lugha ya Kiswahili. Ni wazi kuwa viambishi vya lugha ya Kiswahili huweza kuundwa kwa sauti moja, mbili au hata tatu. Wakati mwingine, mfuatano wa irabu na konsonanti hauzingatii mfuatano ulio katika silabi kwani, kilicho muhimu ni kuwa kila kiambishi kiweze kusimamia maana fulani kisarufi inayokubalika katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya viambishi vya Kiswahili havijisimamii kifonolojia. Hii ina maana kuwa si rahisi kuchunguza sifa za kiarudhi za viambishi vya Kiswahili. Kulingana na matokeo ya utafiti, muundo wa viambishi hutegemea maana inayowakilishwa katika lugha ya Kiswahili.

Baada ya kuangazia maumbo mbalimbali ya viambishi katika lugha ya Kiswahili, mtafiti alichunguza maumbo ya viangami katika lugha ya Kiswahili. Lengo la mtafiti lilikuwa kubainisha ikiwa kuna kufanana na kutofautiana kwa maumbo ya

viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili. Yafuatayo ni maumbo ya viangami katika lugha ya Kiswahili kulingana na utafiti uliofanywa.

### 2.3.3 Maumbo ya Viangami

Sehemu iliyotangulia iliangazia maumbo mbalimbali ya viambishi katika lugha ya Kiswahili. Ni wazi kuwa viambishi katika lugha ya Kiswahili huwa na maumbo mbalimbali. Sehemu hii ya utafiti iliangazia maumbo ya viangami katika lugha ya Kiswahili. Katika utafiti huu, tulipata viangami vya aina mbalimbali. Tazama mfano huu,

| **12** | **Kiangami** | **Neno Kuu** | **Neno Lililoambishwa** |
|---|---|---|---|
| | (a) -o- | mke | mke**o** |
| | (b) -ke- | bwana | bwana**ke** |
| | (c) -ni- | umeleta | umeleta**ni**? |
| | (d) -ngu- | kaka | kakan**gu** |

Kwa mujibu wa mifano hii, ni wazi kuwa viangami vya lugha ya Kiswahili huchukua maumbo mbalimbali. Hapo awali tulikuwa tumeshughulikia maumbo ya viambishi. Kwa kuzingatia mfano huu, maumbo ya viambishi yanatofautiana na yale ya viangami. Tofauti kubwa ni kuwa, baadhi ya viangami huchukua umbo la silabi huru. Kwa mfano, *-o-*, *-ke-*, *-ni-* na *-ngu-* ni aina ya silabi wazi. Hii ina maana kuwa viangami ni tamko na huishia kwa irabu ili viweze kutamkika. Kimatamshi, kiangami hakitegemei vipashio vingine katika neno kuu. Mfano (a) ni wa kiangami kilichoundwa na irabu moja. Mfano (b) na (c) ni mfano wa

viangami vya konsonanti moja ikifuatwa na irabu. Nao mfano (d) ni aina ya kiangami cha konsonanti mbili mwambatano zikifuatwa na irabu.

Baada ya utafiti, viangami vya lugha ya Kiswahili vimedhihirisha kuwa na maumbo mbalimbali. Kuna yale maumbo yanayofanana na ya viambishi na pia kuna mengine yanatofautiana. Sehemu inayofuata inayaangazia kwa undani maumbo tuliyodokeza hapo juu. Maumbo haya yanaainishwa kwa njia zifuatazo:

(a) Viangami vya irabu moja

(b) Viangami vya konsonanti ikifuatwa na irabu

(c) Viangami vya silabi mbili

(d) Viangami funge

Maumbo ya viangami yaliyoorodheshwa hapo juu 6 (a, b, c, d) yaliainishwa kwa kuongozwa na mashartizuizi mbalimbali yanayopatikana katika nadharia ya umbo upeo. Ili umbo fulani la kiangami likubalike katika lugha ya Kiswahili, kuna masharti ambayo huzingatiwa. Kwa mujibu wa nadharia ya umbo upeo, haya ni mashartizuizi mbalimbali ambayo huongoza mwanaisimu kujua ni umbo lipi linalokubalika na lisilokubalika katika lugha husika. Kabla ya kuingilia maumbo mbalimbali ya viangami, hebu kwanza tuangazie mashartizuizi yaliyoongoza utafiti huu.

Mtafiti aliongozwa na Mashartizuizi kulingana na nadharia ya umbo upeo. Kama tulivyoona katika sura ya kwanza, mashartizuizi ni mahitaji ya kimuundo ambayo yanaweza kuvunjwa au kukubalika na umbotokeo (Kager, 2004). Mashartizuizi huweka vigezo ambavyo huamua umbo linalofikia ukubalifu. Umbo fulani

hukubalika ikiwa litatimiza mahitaji yote ya kimuundo. Kager anaendelea na kusema kuwa umbo ambalo halijatimiza mahitaji ya kimuundo husemekana kuwa limekiuka.

Ili kuambisha kiangami kwenye neno kuu, baadhi ya sauti za neno kamili zinadondoshwa na tunapata kiangami. Kwa mfano katika neno *wako* sauti *ak* zinadodoshwa na tunabaki na sauti *wo* ambayo inatumika kama kiangami. Kiangami -*o*- kinaweza kuambishwa kwenye maneno mengine kama vile *mkeo, mwanao* na *wanao.* Tazama mfano huu

Mke wako - mkeo

Mwana wako - mwanao

Wana wako - wanao

Udondoshaji huu haufanywi kiholela. Kwa mujibu wa Kager (2004), mashartizuizi huelekeza wananisimu kupata umbo sahihi katika lugha husika. Wakati mwingine, mabadiliko hufanyika kwenye umboghafi ili umbotokeo likubalike katika lugha husika. Katika mfano huu, sauti *ak* inaondolewa katika neno *wako* na tunabaki na sauti *wo*. Kutokana na kutobainika kwa kiyeyusho *w* kabla ya irabu *o* katika mazingira haya, *w* inadondoshwa na tunasalia na *o* peke yake. Hii ndiyo maana *o* inakuwa kiangami na wala si *wo*.

Uainishaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili unafanana na pia kutofautiana na viangami katika lugha zingine. Hivyo basi mashartizuizi yatakayotumika

yatajifunga na lugha ya Kiswahili. Kager (1999) anaeleza kuwa si sawa kusema kuwa mashartizuizi yote yatazingatiwa kwa njia sawa katika lugha zote. Kila lugha huwa na upangiliaji wa mashartizuizi ambao hutumika kutambua ikiwa umbo limekiuka au halijakiuka sheria zilizowekwa. Katika kila lugha, mashartizuizi hupangwa kulingana na nguvu na uhafifu wake. Hebu sasa tuyaangazie baadhi ya maumbo ya viangami yaliyopatikana katika utafiti huu.

#### 2.3.3.1 Viangami vya Irabu Moja

Hivi ni viangami ambavyo vimeundwa kwa sauti moja na ambayo huwa ni irabu. Tunapounda viangami vya irabu moja, sauti zingine katika neno zinadondoshwa na hivyo kubakia irabu pekee. Irabu hii inatumika kama kiangami na inaambishwa kwenye neno lingine lililo karibu katika sentensi. Yaani neno kuu. Kwa kawaida irabu hii hutamkwa kama silabi baada ya kuambishwa kwa neno kuu. Baadhi ya mifano ya viangami vya silabi moja ni kama vile:


| 13. | **Neno kuu** | | **Kiangami** | | **Umbotokeo** |
|---|---|---|---|---|---|
| | (a) Mwenzi | + | -o- (wako) | = | mwenzi**o** |
| | (b) Wana | + | -o- (wako) | = | wana**o** |
| | (c) Mke | + | -o- (wako) | = | mke**o** |
| | (d) Mwenzi | + | -o- (wako) | = | mwenza**o** |
| | (e) Na | + | -o- (wao) | = | na**o** |

Kuliangana na mfano 13 (a-e), irabu ya mwisho ya neno linalofupishwa ndiyo imetumika kama kiangami. Irabu yenyewe ni –**o-** ambayo imetokana na maneno kamili *wako* na *wao*. Kiangami –**o-** kinatokana na kimilikishi *wako* na *wao*.

Kulingana na utafiti huu, ni vigumu kupata kiangami cha lugha ya Kiswahili cha konsonanti moja peke yake kwani viangami vya lugha ya Kiswahili vinatamkika. Pia viangami vya lugha ya Kiswahili huwa na muundo wa silabi wazi. Hii ni kinyume na maumbo ya viambishi katika lugha ya Kiswahili kwani kunavyo viambishi vya konsonanti moja.

Kulingana na utafiti huu, viangami ni silabi wazi ambayo imeundwa na irabu moja pekee. Kwa kawaida, silabi huwa na sehemu tatu kuu. Sehemu hizi ni kilele (LE), tangulio (TA) na koda/fungio (Yule, 1996). Tangulio huundwa na konsonanti moja au zaidi. Si lazima silabi iwe na tangulio kwani silabi huweza kuanza kwa irabu hasa katika maneno yanapoanza na irabu inayotamkika. Sehemu ya pili ya silabi ni kilele. Hiki ndicho kiini au kitovu cha silabi. Sehemu hii huwa na irabu ambayo ndiyo husikika zaidi wakati wa matamshi. Kilele ni kiungo cha lazima. Koda au fungio ndiyo sehemu ya mwisho katika silabi. Koda huwa ni konsonanti moja au zaidi. Hiki si kiungo cha lazima katika silabi. Koda hupatikana ikiwa silabi ni funge.


**Kielelezo cha Silabi**




Kielelezo hiki cha silabi kinadhihirisha sehemu tatu muhimu za silabi moja. Kuna mwanzo konsonanti (K), kitovu, irabu (I) na koda, konsonanti (K).

Viangami vya irabu moja ni aina ya silabi iliyo na kiini pekee kwani haianzi kwa konsonanti wala kuishia na koda. Kwa kutumia mfano tutaangalia muundo wa kiangami cha irabu moja.

14.




Silabi ya mwisho –o-, ndicho kiangami katika neno *wanao*,. Kiangami –o- kimeundwa na irabu moja tu. Kwa kutumia mashartizuizi, mtafiti anaonyesha jinsi neno *wanao* lilivyoibuka mshindi kati ya maumbo mbalimbali yanayopatikana baada ya kuunganisha neno *wana* na *wako.*

**Jedwali 2.3: Ukiukwaji wa Mashartizuizi ya 'wanao'**

| **/wana+wako/** | **H-KODA** | ***II** | **FIKI-UKO*KKKn** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|---|
| 1.☞ wa.na.o | | | | * |
| 2. wa.na.k | | | | * |
| 3. wa.na.a.o | | * | | |
| 4. wa.na.wk | *! | | | |

Kulingana na Jedwali 2.3, umbo *wanao*, ndilo linaloibuka mshindi. Hata kama mshindani *wanao*, ndilo umbo linalokuwa umbo upeo, limevunja sharti moja ambalo ni FIKI-UKO. Kulingana na utafiti huu, ukiukaji huu unavumilika kwani, sharti la FIKI-UKO linazuia udondoshaji wa vipandesauti, jambo ambalo linakubalika katika dhana ya viangami. Ili kupata kiangami, vitamkwa fulani hudondoshwa.

Maumbotokeo ya pili na nne, (*wanak* na *wanawk*) yamevunja sharti ambalo haliwezi kuvumilika katika lugha ya Kiswahili. Maneno haya yanaishia na konsonanti hivyo kumaanisha kuwa silabi ya mwisho inaishia kwa koda. Kwa vile silabi za Kiswahili ni wazi na huishia kwa irabu, maumbo haya hayakubaliki. Umbotokeo la tatu nalo (*wanaao*) lina irabu tatu zinazofuatana. Huo ni ukiukaji mwingine ambao hauwezi kuvumilika. Kwa kurejelea Jedwali 2.3, ni wazi kuwa umbo *wanao* limefikia ukomo wa kukubalika kwa kuzingatia dhana ya viangami katika lugha ya Kiswahili.

#### 2.3.3.2 Viangami vya Konsonanti Ikifuatwa na Irabu

Sehemu hii inashughulikia umbo la pili la viangami vya lugha ya Kiswahili. Hivi ni vile viangami ambavyo vimechukua umbo la silabi moja ambayo imeundwa kwa zaidi ya sauti moja. Sauti hizi huwa ni konsonanti moja ikifuatwa na irabu moja na pia kuna viangami ambavyo huchukua muundo wa konsonanti mbili mwambatano zikifuatwa na irabu moja. Tazama Mfano 15.

| 15. | **Neno kuu** | | **Kiangami** | | **Umbotokeo** |
|---|---|---|---|---|---|
| | (a) Wana | + | (wetu) **-tu-** | = | Wanetu |
| | Mama | + | (yako) –**ko-** | = | Mamako |
| | Dada | + | (yake) –**ke-** | = | Dadake |
| | (b) Wana | + | (**wa**k**e) –we-** | = | Wanawe |
| | Sura | + | (**y**ak**o) –yo-** | = | Surayo |
| | Mama | + | (**y**ak**e) –ye-** | = | Mamaye |
| | (c) Si | + | (yeye) –**ye-** | = | Siye |
| | Na | + | (mimi) –**mi-** | = | Nami |
| | (d) Kwa | + | (hivyo) –**vyo-** | = | Kwavyo |
| | Kaka | + | (yangu) –**ngu-** | = | Kakangu |

Kulingana na data ya utafiti huu, viangami vingi katika lugha ya Kiswahili huchukua muundo huu ikilinganishwa na ile miundo mingine iliyoorodheshwa. Kulingana na Mfano 15, viangami huchukua muundo wa silabi moja ambayo ni silabi wazi. Konsonanti moja au mbili hufuatwa na irabu na kuunda kiangami. Silabi hii huweza kuwa yoyote katika kila neno. Kwa mfano, mifano mitatu ya kwanza (15, a) imekubali silabi za mwisho jinsi zilivyo. Silabi hizo zimeweza kutumika kama viangami. Mifano inayofuata inachukua konsonanti ya mwanzo katika neno linalofupishwa na irabu ya mwisho. Sauti hizi mbili zinaunganishwa na kuunda kiangami kinachokubalika katika lugha ya Kiswahili.

Hebu sasa tuangalie jinsi viangami vya konsonanti ikifuatwa na irabu vinavyokiuka mashartizuizi ya umbo upeo. Katika jedwali letu, tuliongozwa na masharti manne ambayo ni, Kilele, H-KODA, *II na *YK. Kwa kuzingatia

masharti haya, tulionyesha jinsi neno *hatimaye* lilivyofikia upeo wa kukubalika. Neno hali linatokana na neno kuu, *hatima* ambalo limeambishwa kiangami *ye* (yake).

**Jedwali 2.3: Ukiukwaji wa Mashartizuizi ya Hatimaye**

| /hatima+yake/ | **Kilele** | **H-KODA** | ***II** | ***YK** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) ☞ha.ti.ma.ye | | | | | * |
| (b) ha.ti.ma.yk | *! | * | | * | * |
| (c) ha.ti.ma.e | | | *! | | * |

Katika Jedwali 2.4, mshindani (a) ndiye mshindi. Hajavunja mashartizuizi yaliyotumika. Mshindani (b) anavunja masharti matatu muhimu. Kwanza, amevunja sharti la Kilele kwani kiangami chake ambacho ni silabi ya mwisho hakina kilele. Kiangami hicho pia hakina koda na mwisho ni kuwa mshindani huyu anavunja sharti la *YK kwani sauti *y* ambayo ni kiyeyusho imefuatwa na sauti *k* ambayo ni konsonanti halisi.

#### 2.3.3.3 Viangami vya Silabi Mbili

Viangami hivi huweza kuchukua silabi mbili kutoka kwa neno linalofupishwa. Viangami vya silabi mbili huchukua sehemu kubwa ya neno hivi kwamba, silabi zinazodondoshwa ni chache ikilinganishwa na zile zinazotumika kama kiangami.

Katika lugha ya Kiswahili, viangami vya silabi mbili ni vichache ikilinganishwa na vile vya silabi moja. Ifuatayo ni mifano ya viangami vya silabi mbili:

| 16. | **Neno kuu** | | **Kiangami** | **Umbotokeo** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | (a) Cha | + | **-jio- (**jioni) | = | cha**jio** |
| | (b) Cha | + | **-mcha- (**mchana) | = | cha**mcha** |

16 (a, b) inadhihirisha kuwa, viangami vya silabi mbili huweza kuambishwa mwanzoni mwa neno kuu. Katika neno *mchana* na *jioni*, silabi moja tu ndiyo inayodondoshwa nayo sehemu kubwa ya neno inatumika kuunda kiangami.

**Jedwali 2.4 Ukiukwaji wa Masharti-Zuizi wa *chamcha***

| **/Cha+mchana/**<br>**(chakula cha mchana)** | **H-KODA** | **SHABI-SI** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|
| (a) ☞cha.m.cha | | | * |
| (b) cha.m | *! | * | * |
| (c) cha.na | | | *! |

Kulingana na Jedwali 2.4, neno *chamcha* ndilo umbotokeo ukilinganisha na maumbo hayo mengine. Kando na kuonekana kuwa linazingatia sheria zote zilizotumika, neno hili pia limeweza kukubalika na wanajamii na ndilo hutumika katika mazungumzo ya kawaida. Neno la pili *cham* halijaibuka mshindi na pia neno la tatu *chana*. Maneno haya yameshindwa katika ushindani huu. Hata kama maneno haya mawili yamefupishwa, yanaonekana kuvunja masharti yasiyoweza kuvumilika.

### 2.3.3.4 Viangami Funge

Hivi ni viangami ambavyo haviishii na irabu, badala yake vinaishia na konsonanti aina ya nazali. Viangami hivi si vingi. Ni nadra kupata neno la Kiswahili ambalo haliishii kwa irabu. Baada ya utafiti huu, kiangami kimoja funge kiliweza kupatikana. Mfano wenyewe ni,

17. **Twen**de + zetu =twenzetu


Kutokana na mfano huu, neno kuu ni *zetu.* Hili ndilo neno kamili linaloambishwa kiangami mwanzoni. Neno linalofupishwa ili kupata kiangami ni *twende*. Kiangami kinachopatikana ni *twen*- ambacho kinaambishwa mwanzoni mwana neno kuu *zetu*. Hiki kitaitwa kiangami funge kwani hakina muundo wa silabi wazi, kwani sauti ya mwisho ya kiangami hiki ni konsonanti */n/* ambayo ni nazali ghuna ya kaakaa laini. Kiangami kina uwezo wa kujisimamia kifonolojia. Hii ina maana kuwa viangami huweza kutamkika kwani katika lugha ya Kiswahili, viangami huchukua muundo wa silabi huru. Kiangami *twen*- kinavunja sheria hiyo lakini bado ni kiangami.

Hata kama kiangami *twen*- kinaonekana kuwa silabi funge inayoishia koda, wakati wa kutamka neno *twenzetu* silabi zote huwa wazi. Konsonanti /*n*/ inaunganishwa na silabi –*ze*- na kuwa silabi mwambatano. Hivyo basi utamkaji wa neno hili baada ya kuambishwa kiangami utakuwa kama ifuatavyo:

*Twe-nze-tu*

Tazama Mfano 18,

18.




Kwa mujibu wa nadharia ya umbo upeo, kunayo mashartizuizi ambayo huweza kukiukwa lakini umbo likakubalika katika lugha husika. Nadharia hii inaeleza kuwa kunaweza kuwa na shartizuizi ambalo liko katika daraja ya chini yaani hafifu hivi kwamba hata likikiukwa hapatakuwepo na athari yoyote (Massamba, 2011). Konsonanti ya mwisho katika kiangami hiki ambayo ni *n*, inaunganishwa na konsonanti ya kwanza ya neno kuu *zetu* na hivyo kutamkika kama sauti moja.

Utafiti huu ulibaini kuwa kuna tofauti katika maumbo ya viambishi na viangami vya lugha ya Kiswahili. Kwanza, ni wazi kuwa baadhi ya viangami ni huru kifonolojia. Viangami vingi vinachukua muundo wa silabi. Hii ni tofauti na hali ilivyo katika viambishi. Baadhi ya maumbo ya viambishi yanaonyesha kuwa si lazima viambishi vijisimamie kifonolojia. Pili ni kuwa viangami huambishwa kwenye neno kamili ilhali viambishi vinaambishwa kwenye mzizi wa neno. Tofauti ya tatu ni kuwa viangami ni lazima viishie kwa irabu lakini si lazima kiambishi kiwe kwa irabu.

## 2.4 Uainishaji wa Viangami na Viambishi

Baada ya kuangalia maumbo ya viangami katika lugha ya Kiswahili, tutaainisha viangami hivyo. Utafiti huu unadhihirisha kuwa kunazo aina mbalimbali za viangami. Kutokana na utafiti huu, kila kiangami kinaonekana kusimamia dhana fulani kama ilivyo katika viambishi. Kabla ya kuangazia uainishaji wa viangami kulingana na utafiti huu, kwanza tulishughulikia uainishaji wa viambishi.

Viambishi huainishwa kwa kutumia vigezo viwili. Kigezo cha kwanza ni maana inayowakilishwa na cha pili ni kwa kuzingatia nafasi vinamotokea. Kwa mujibu wa Mgullu (2001), kuna aina tatu za viambishi. Kuna viambishi awali, viambishi ndani na viambishi tamati. Mgullu ameainisha viambishi kutegemea upande wa neno vinapopatikana, kabla ya mzizi au baada ya mzizi. Massamba (1999), kwa kuzingatia nafasi vinamotokea, amesema kwamba Kiswahili kina viambishi vya aina mbili, viambishi vinavyotangulia mzizi na viambishi vinavyotokea baada ya mzizi. Hivi ni viambishi awali na viambishi tamati. Katika utafiti huu, tuliangazia viambishi vya lugha ya Kiswahili kulingana na mahali vinamotokea, yaani kabla au baada ya mzizi wa neno. Pia tuliangalia viambishi kutegemea maana inayowakilishwa.

Ni vyema kukumbuka kuwa viambishi huambatishwa kwenye mzizi wa neno yaani sehemu ya neno ambayo hubeba wazo kuu na haiwezi kuvunjwa zaidi. Kwa kuzingatia uamilifu wake kama vipengele vya kisarufi, viambishi vya lugha ya Kiswahili huainishwa kwa njia mbalimbali kutegemea dhana mbalimbali za

kisarufi zinazowakilishwa. Dhana hizi ni kama vile ngeli, mnyambuliko, nafsi na wakati.

Katika sehemu hii, mtafiti aliangalia kufanana na kutofautiana kwa viangami na viambishi kwa kuzingazita uainishaji wake. Kwanza, mtafiti alianisha viambishi vya Kiswahili na baadaye kuanisha viangami vya Kiswahili. Vipashio hivi viwili vilianishwa kwa kuzingatia vigezo viwili. Vigezo hivi ni uamilifu wake na nafasi vinamotokea. Hebu sasa tuangalie uanishaji wa viambishi kwa kutumia kigezo cha kwanza ambacho ni nafasi vinamotokea.

### 2.4.1 Uainishaji wa Viambishi kwa Kuzingatia Nafasi Vinamotokea

Katika lugha mbalimbali ulimwenguni, viambishi huainishwa kwa kutegemea mahali vinawekwa kwenye neno (Mgullu, 2001). Kunazo aina tatu za viambishi kwa kuzingatia mahali vinamotokea. Viambishi hivi ni, viambishi awali, viambishi ndani na viambishi tamati. Viambishi awali hutokea kabla ya mzizi, viambishi ndani hutokea katikati ya mzizi navyo viambishi tamati huwekwa baada ya mzizi.

Lugha ya Kiswahili ina aina mbili za viambishi: kiambishi awali na kiambishi tamati. Katika lugha ya Kiswahili, hakuna viambishi ndani. Mzizi wa neno ndicho kipengele muhimu katika uainishaji huu. Mzizi wa neno ni ile sehemu ya neno isiyobadilika na pia haiwezi kuvunjwavunjwa bila kupoteza maana yake. Katika lugha ya Kiswahili, viambishi huweza kupachikwa kabla au baada ya mzizi wa neno.

#### 2.4.1.1 Viambishi Awali

Kulingana na utaratibu wa othografia ya Kiswahili, viambishi awali hutokea upande wa kushoto wa mzizi (Mgullu, 2001). Hivi ndivyo viambishi vinavyotokea kabla ya mzizi wa neno kama vile nomino au kitenzi. Tazama mfano huu

| 19. | **Mzizi** | **Neno Lililoambishwa** |
|---|---|---|
| | -chor- | **a-li-ni-**chor-a |
| | -pik- | **tu-ta-**pik-a |
| | -samehe- | **wa-ta-ka-o-wa-**samehe |

Kulingana na mfano huu, viambishi awali yaani vilivyokolezwa vinajitokeza kabla ya mzizi wa neno. Viambishi hivi vinachukua maumbo tofauti na pia vinaonenkana kubeba wazo tofauti. Viambishi awali ni vingi na huweza kuwakilisha dhana mbalimbali za kisarufi. Baadhi ya dhana ni kama zifuatazo,

(a) Viambishi vya ngeli

(b) Viambishi vya wakati au njeo

(c) Viambishi vya o-rejeshi

(d) Viambishi vya udogo na ukubwa

(e) Viambishi vya ukanushi

(f) Viambishi vya nafsi

**(a) Viambishi vya Ngeli**

Ngeli ni kundi la nomino za aina moja (Mgullu, 2001). Kwa kuzingatia kigezo cha kisintaksia, nomino katika ngeli moja huwa na upatanisho wa kisarufi unaofanana. Upatanisho wa kisarufi huzingatia uhusiano wa nomino na maneno mengine katika

tungo. Vipatanishi vya kisarufi huwekwa kwenye vitenzi, vivumishi na viwakilishi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ngeli katika lugha ya Kiswahili.

| | | |
|---|---|---|
| 20. | Mwanafunzi *a*-na**som**a. | |
| | Wanafunzi *wa*-na**som**a | A/wa |
| | Kiatu *ki*-li**pote**a | |
| | Viatu *vi*-li**pote**a | ki/vi |
| | Tunda *li*-me**iv**a | |
| | Matunda *ya*-me**iv**a | li/ya |

Mfano 20 unaonyesha kuwa, nomino inayotumika katika sentensi huathiri viambishi vya mwanzo katika kitenzi kilicho katika sentensi. Kwa mujibu wa mifano iliyotolewa, viambishi vya ngeli huja mwanzoni mwa kitenzi.

**(b) Viambishi vya Wakati au Njeo**

Viambishi vya wakati hutumika kuonyesha wakati ambapo tendo lilitendeka au halikutendeka. Katika lugha ya Kiswahili, kuna aina tatu za wakati: kwanza, kuna wakati uliopita unaowakilishwa na kiambishi –li- katika kuyakinisha na kiambishi –ku- cha ukanushi. Pili, kuna wakati uliopo unaowakilishwa na kiambishi –na cha kuyakinisha na mwisho, kuna wakati ujao ambao huwakilishwa na kiambishi –ta-. Ifuatayo ni mifano ya viambishi vya wakati.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21. | Kuyakinisha | kukanusha | |
| | (a) a-*li*-**som-**a | ha-*ku*-som-a | (wakati uliopita) |
| | (b) a-*na*-**som**a | ha-som-i | (wakati uliopo) |
| | (c) a-*ta*-som-a | ha-*ta*-som-a | (wakati ujao) |

Mfano 21 umeonyesha viambishi vya njeo. Kama inavyojitokeza katika mifano, lugha ya Kiswahili huwa na aina tatu za njeo. Katika kuyakinisha, viambishi vya njeo vinajitokeza baada ya kiambishi cha nafsi. Katika ukanushaji wake, viambishi hivi hubadilika isipokuwa kiambishi cha wakati ujao –ta-. Katika (a) kiambishi –li- cha wakati uliopita kinabadilika na kuwa –ku-. Katika (b) tunaona kuwa kiambishi –na- cha wakati uliopo kinatoweka baada ya kukanusha.

(c) **Viambishi vya –o- rejeshi**

Hivi ni viambishi vinavyorejelea nomino ambayo imetajwa kabla ya kitenzi katika sentensi. Umbo la kiambishi cha –o- rejeshi hutegemea ngeli ya nomino inayorejelewa. Ifuatayo ni baadhi ya mifano katika sentensi inayoonyesha matumizi ya urejeshi.

22. KI/VI

Kitabu kili-*cho*-**som**wa

Vitabu vili-*vyo*-**som**wa

A/WA

Mtu ali-*ye*-**faulu**

Watu wali-*o*-**faulu**

**(d) Viambishi vya udogo na ukubwa**

Nomino katika lugha ya Kiswahili hupatikana katika hali tatu. Hali ya kawaida au wastani, hali ya udogo na hali ya ukubwa. Nomino inapobadilika kutoka hali ya kawaida hadi hali ya ukubwa au udogo, umbo lake huwa tofauti. Mifano ifuatayo inaonyesha viambishi vya ukubwa na udogo.

| 23. | **Wastani** | **Udogo** | **Ukubwa** |
|---|---|---|---|
| | (a) m-**toto** | *ki*-**toto** | *ji*-**toto** |
| | (b) wa-**toto** | *vi*-**toto** | *ma*-**toto** |
| | (c) m-**guu** | *ki*-**guu** | guu/ji-**guu** |
| | (d) mi-**guu** | *vi*-**guu** | *ma*-**guu** |

Mifano 16 inaonyesha kuwa, viambishi vya udogo au ukubwa huwekwa mwanzoni mwa neno. Katika udogo, kuna kiambishi –ki- katika umoja na –vi- katika wingi. Katika ukubwa kuna kiambishi –ji- au Ө katika umoja na ma katika wingi.

**(d) Viambishi vya Nafsi**

Katika lugha ya Kiswahili, kuna aina tatu za nafsi. Kuna nafsi ya kwanza (mimi, sisi), nafsi ya pili (wewe, nyinyi) na nafsi ya tatu (yeye, wao). Viambishi vya nafsi huambishwa mwanzoni mwa neno. Ifuatayo ni mifano ya viambishi vya nafsi.

| 24. | **nafsi** | **umoja** | **wingi** |
|---|---|---|---|
| | **(a)** kwanza | *ni*-na-**pik**-a | *tu*-na-**pik**-a |
| | (b) pili | *u*-na-**pik**-a | *m*-na-**pik**-a |
| | (c) tatu | *a*-na-**pik**-a | *wa*-na-**pik**-a |

Katika lugha ya Kiswahili, viambishi awali huwasilisha dhana kadha kama vile, ngeli, wakati, urejeshi, ukubwa, udogo na nafsi. Hizi tu ni baadhi ya dhana zinazowakilishwa na viambishi awali.

### 2.4.1.2 Viambishi Tamati

Hivi ni viambishi ambavyo hutanguliwa na mzizi. Viambishi tamati hutokea upande wa kulia baada ya mzizi wa neno. Baadhi ya viambishi vinavyotamatisha neno ni:

| 25 | **Mzizi** | **Neno Lililoambishwa** |
|---|---|---|
| | **(a)** -tazam- | a-li-tazam-**i-a** |
| | **(b) -**tembe- | tu-li-tembe-**le-w-a** |
| | **(c) -**pik- | ni-li-pik-**i-w-a** |

Baadhi ya maana za kisarufi zinazowakilishwa na viambishi hivi ni kama vile:

(a) Viambishi vya kauli au mnyambuliko wa kitenzi

(b) Viambishi vya rai

(c) Viambishi viishio

(d) Viambishi vya o-rejeshi ya tamati

(e) Viambishi vya mahali

Hebu sasa tueleze viambishi hivi. Kila moja ya viambishi ilielezewa kwa kutumia mifano.

**(a) Viambishi vya Kauli au Mnyambuliko wa Kitenzi**

Viambishi hivi huwekwa baada ya mzizi wa kitenzi na huwakilisha kauli mbalimbali katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya kauli zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili ni pamoja na:

26. (a) **som**-a kauli ya kutenda

(b) **som**-*w*-a kauli ya kutendwa

**(c) som-**ew-a kauli ya kutendewa

**(d) som-**ek-a kauli ya kutendeka

**(e) som-**esh-a kauli ya kutendesha

**(f) som-**e-a kauli ya kutendea

(b) **Viambishi vya Rai, Dhamira, Tegemezi au Amri**

Viambishi hivi huwezesha kitenzi kuwa na dhana ya kuomba, kusihi au kuhimiza. Kiambishi –e- hutumika kuonyesha rai. Kwa mfano,

27 (a) ni-**som**-e-*e*

(b) ni-**let**-e-*e*

(c) tu-**fung**-i-*e*

**(c) Viambishi Viishio**

Hivi ni viambishi vinavyotumika kama vimalizio vya vitenzi. Vitenzi vya asili ya kibantu huishia na irabu –a- ikiwa kitenzi kiko katika hali yakinishi. Katika hali ya kukanusha, kiishio –a- hubakia au hubadilika na kuwa –i- ikiwa lengo la kitenzi ni kutoa taarifa.

| | | |
|---|---|---|
| 28 | **Kuyakinisha** | **Kukanusha** |
| | (a) a-na-**som**-*a* | ha-**som**-*i* |
| | (b) ni-li-**imb**-*a* | si-ku-**imb**-*a* |
| | (c) u-na-**pik**-*a* | hu-**pik**-*i* |

**(d) Viambishi vya o-rejeshi ya Tamati**

Viambishi hivi hutumiwa kurejelea nomino ambayo tayari imetajwa kabla ya kitenzi. Kwa mfano,

29. (a) Mwanafunzi a-**som-**a-*ye*

(b) Nyumba i-**jeng**-w-a-*yo*

(c) Kalamu zi-**nunu**-li-w-a-z*o*

**(e) Viambishi vya Mahali**

Viambishi hivi hutumika kuonyesha mahali ambapo kitendo kilitendeka. Wakati unaoonyeshwa na viambishi hivi huwakilisha mahali ambapo si dhahiri. Ifuatayo ni baadhi ya mifano.

30. (a) Mahali a**ingi**a-**mo** ni humu.

(c) Pahali a**simam**a-*po* ni hatari.

(d) Mahali a**chez**ea-*ko* ni huku.

Mfano 30 unaonyesha kuwa viambishi tamati hutokea baada ya mzizi. Viambishi hivi vinawakilisha dhana kama vile, kauli, rai, na kiishio. Pia kuna viambishi vingine kama vile vinavyowakilisha mahali na mnyambuliko. Hivi vina uwezo wa kujipachika kabla ya mzizi na pia baada ya mzizi.

Jedwali 2.5 linatoa muhtasari wa uainishaji wa viambishi kwa kuzingatia nafasi vinamotokea. Mtafiti ametumia neno ‘soma’. Neno hili limeambishwa viambishi mbalimbali, vya awali na tamati.

**Jedwali 2.5: Viambishi Awali na Viambishi Tamati**

| viambishi awali | | | | | mzizi | viambishi tamati | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nafsi | Wakati | Kirejeshi | mahali | mtendwa | Mzizi | Kauli | kiishio | Kirejeshi |
| a | Li | ye | | ni | som | e | a | |
| a | | | | ni | som | e | a | ye |
| wa | Li | | po | | som | e | a | |
| a | | | | | som | | a | po |

Kwa kuzingatia Jedwali 2.5, viambishi awali vimejitokeza kabla ya mzizi navyo viambishi tamati vinapatikana baada ya mzizi. Katika uainishaji wa viambishi kwa kutegemea nafasi vinamotokea, kuna viambishi ambavyo huwakilisha dhana fulani na huweza kujitokeza kama viambishi awali na pia viambishi tamati. Viambishi hivi ni viambishi vinavyowakilisha mahali na viambishi vya *–o* rejeshi. Kwa mfano,

31. (a) a-li-ye-**som**-a o-rejeshi

(b) a-**som**-e-a-ye

(c) a-**chez**-e-a-po mahali/wakati

(d) a-na-po-**chez**-e-a

Kwa kuzingatia kigezo hiki cha nafasi, tuliweza kupata aina mbili za viambishi katika lugha ya Kiswahili. Kuna viambishi awali na tamati. Mzizi ndicho kigezo muhimu kinachotumika kuainisha viambishi hivi. Vinaitwa viambishi awali kwa vile hupatikana mwanzoni mwa neno kabla ya mzizi, navyo viambishi tamati ni

vile vinavyojitokeza baada ya mzizi wa neno husika. Hebu sasa tuangazie uainishaji wa viambishi kwa kuzingatia kigezo cha pili ambacho ni uamilifu wa viambishi.

### 2.4.2 Uainishaji wa Viambishi Kiuamilifu

Kila kiambishi katika lugha ya Kiswahili huwakilisha maana ya kisarufi. Kiambishi huweza kuongeza maana ya neno na pia kuibadilisha. Kila kiambishi kinachoambishwa kwenye mzizi wa neno huwakilisha dhana fulani ya kisarufi. Maana yenyewe ni lazima ikubalike katika lugha ya Kiswahili. Viambishi havipachikwi kiholela. Kwa mujibu wa Massamba na wengine (1999), viambishi vya Kiswahili huweza kuwakilisha maana zifuatazo:

(a) Idadi
(b) Upatanisho wa kisarufi
(c) Unyambulishaji wa nomino
(d) Unyambulishaji wa vitenzi
(e) Nafsi
(f) Wakati
(g) Hali
(h) –o- rejeshi

Viambishi hivi vilielezwa kwa kutumia mifano. Kila kiambishi kilifafanuliwa kivyake.

#### (a) Idadi

Viambishi hivi huleta dhana ya umoja na wingi wa nomino inayorejelewa. Kwa mfano:

| **32** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| | (a) *M* – toto | *wa* – toto |
| | (b) *Ki* – tu | *vi* – tu |
| | (c) *Ji* – cho | *ma* – cho |
| | (d) *M* – ti | *mi* – ti |

Viambishi vya idadi katika nomino hutokea mwanzoni mwa neno. Viambishi hivi hutofautiana kutegemea nomino. Si nomino zote za lugha ya Kiswahili zilizo na viambishi vya idadi. Nomino kama vile *samaki*, *shangazi* na *samba* hazichukui viambishi vya idadi.

**(b) Upatanisho wa Kisarufi**

Upatanisho wa kisarufi ni ile hali ya viambishi vya maneno katika sentensi kukubaliana na kushikamana ili kuleta maana iliyokusudiwa. Kwa mujibu wa Bakita (2015), upatanisho wa kisarufi ni kukubaliana kisarufi kunakojitokeza kati ya nomino kiima na kitenzi au kivumishi na hubainishwa na viambishi. Kutokana na upatanisho wa kisarufi, tunapata ngeli mbalimbali za Kiswahili.

| 33. **Ngeli** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| (a) KI-VI (Kiatu) | **ki** – me – pote – a | **vi** – me – pote – a |
| (b) A-VWA (Mtu) | **a** – li – rudi | **wa** – li – rudi |
| (c) LI-YA (Embe) | **li** – me – baki | **ya** – me – baki |
| (d) U-I (Mswaki) | **u** – me –anguk-a | **i** – me – anguk – a |

Viambishi hivi vya ngeli vinaathiriwa na nomino inayotumika katika sentensi. Nomino hiyo huwa ndiyo inarejelewa na kitenzi kilichotumika na pia kufafanuliwa zaidi na kivumishi. Nomino inapobadilishwa, viambishi vya upatanisho wa

kisarufi vinabadilika pia. Viambishi hivi hupatikana mwanzoni mwa kitenzi na pia mwishoni mwa kivumishi.

### (c) Unyambuaji wa Nomino

Njia moja ya kuunda nomino mpya ni kwa kunyambua mzizi wa nomino. Viambishi huweza kuongezwa mwanzoni na pia mwishoni mwa mzizi wa nomino. Ifuatayo ni mifano ya mnyambuliko wa nomino.

| 34 **Nomino ya Kawaida** | **Nomino ya Kawaida (mazoea)** | **Nomino Dhahania** |
|---|---|---|
| Siki – o | m – siki – li – za – ji | u-siki-vu |
| M – chez – o | m – chez – a – ji | u-chez-a-ji |
| M – sem – o | m – sem-a – ji | u-sem-a-ji |

### (d) Unyambuaji wa Vitenzi

Hivi ni viambishi vinavyorefusha kitenzi na hivyo kuongeza maana za kitenzi kile. Baada ya kunyambua vitenzi vya Kiswahili, vitenzi huweza kujitokeza katika kauli mbalimbali kama vile kauli ya kutendea, kutendeka, kutendeana, kutendesha na kadhalika.

Katika kila kauli, kiambishi cha mnyambuliko huongezewa baada ya mzizi wa kitenzi. Neno kama vile *pig-a* linaweza kuongezewa viambishi kadha baada ya mzizi ili kuleta dhana mbalimbali. Kwa mfano, kwa kuongeza kiambishi –*e*- baada

ya mzizi, tunapata neno, *pig-i-a.* Neno *pigia* liko katika kauli ya kutendea na linaleta dhana ya kufanya kitendo cha kupiga kwa niaba ya au kwa sababu ya.

Jedwali 2.6 linaeleza mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili kwa kuzingatia kauli nne ambazo ni kauli ya kutenda, kutendea, kutendewa, kutendeka na kutendesha.

**Jedwali 2.6 Mnyambuliko wa Vitenzi**

| **Mzizi** | **Tenda** | **Tendea** | **Tendewa** | **Tendeka** | **Tendesha** |
|---|---|---|---|---|---|
| omb- | omb-a | omb-**e**-a | omb-**ew**-a | | omb-**esh**-a |
| -pik- | pik-a | pik-**i**-a | pik-**iw**-a | pik-**ik**-a | pik-**ish**-a |
| -lim- | lim-a | lim-**i**-a | lim-**w**-a | lim-**ik**-a | lim-**ish**-a |
| chez- | chez-a | chez-**e**-a | chez-**w**-a | chez-**ek**-a | chez-**esh**-a |

Jedwali 2.6 linadhihirisha kuwa, kila kauli huwa na viambishi mbalimbali vinavyowezesha neno kuwakilisha dhana fulani baada ya kunyambuliwa. Ni sharti kila mnyambuliko uwe na maana inayokubalika kisarufi. Mzizi huweza kuathiri kiambishi cha mnyambuliko. Katika mifano iliyo kwenye Jedwali 2.6, ikiwa mzizi wa kitenzi kinachonyambuliwa una irabu /o/, viambishi vya mnyambuliko huwa na irabu /e/ na ikiwa mzizi una irabu /i/, viambishi vya mnyambuliko huwa na irabu /i/.

**(e) Nafsi**

Lugha ya Kiswahili huwa na nafsi tatu, nafsi ya kwanza umoja (mimi) na wingi (sisi), nafsi ya pili umoja (wewe) na wingi (nyinyi), na nafsi ya tatu umoja (sisi) na wingi (wao). Kila nafsi huwakilishwa na kiambishi fulani. Kwa mfano, nafsi ya kwanza huwakilishwa na kiambishi –*ni*- katika umoja na –*tu*- katika wingi. Katika

nafsi ya pili, kiambishi –*u*- hutumika katika umoja na –*m*- katika wingi. Nayo nafsi ya tatu huwakilishwa na kiambishi -*a*- katika umoja na -*wa*- katika wingi.

| 35. | **Nafsi** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|---|
| | kwanza | *Ni* – me – som – a | *tu* – me – som – a |
| | pili | *U* – me – som – a | *m* – me – som – a |
| | tatu | *A* – li – som – a | *wa* – li – som – a |

Viambishi vya nafsi hutokea mwanzoni mwa kitenzi. Viambishi hivi hutumika kurejelea viumbe vilivyo hai.

**(f) Wakati/Njeo**

Hivi ni viambishi vinavyowakilisha wakati unaorejelewa. Kunazo nyakati tatu ambazo ni wakati uliopo, ujao na uliopita. Ifuatayo ni mifano:

| | | |
|---|---|---|
| 36 | A – *li* – end – a | (uliopita) |
| | A – *na* – end – a | (uliopo) |
| | A – *ta* – end – a | (ujao) |

**(g) Hali**

Katika lugha ya Kiswahili kunazo hali kadhaa. Ifuatayo ni mifano,

| | | |
|---|---|---|
| 37 | A – <u>me</u> – lim – a | (timilifu) |
| | Hu – <u>li</u>m – a | (mazoea) |
| | A – <u>ki</u> – lim – a | (masharti) |

**(h) Kirejeshi cha – o –**

Hiki ni kiambishi cha mtenda au mtendewa ambacho hujitokeza katika kitenzi ili kuonyosha dhana ya urejeshi. Tazama Mfano 38.

38 Ki – li – cho – iv – a
Li – li – lo – ish - a

Kwa kuzingatia kigezo cha uamilifu, tunapata viambishi vya aina mbalimbali. Kulingana na mifano iliyotolewa, kuna viambishi ambavyo kila mara huja kabla ya mzizi. Hivi ni viambishi kama vile vya nafsi, ngeli, wakati, hali na mtendwa. Kuna viambishi vingine ambavyo huja baada ya mzizi. Viambishi hivi ni kama vile viambishi vya rai, viishio na pia viambishi vya mnyambuliko. Kuna baadhi ya viambishi vilivyo na uwezo wa kuambishwa kabla ya mzizi na pia baada ya mzizi. Viambishi hivi ni kama vile viambishi vya –o- rejeshi, viambishi vya wakati na mahali.

## 2.5 Uainishaji wa Viangami

Baada ya kuainisha viambishi, mtafiti alishughulikia uainishaji wa viangami. Kama ilivyojitokeza katika viambishi, pia viangami vinaainishwa kwa njia kadha. Viangami hujiambisha kwenye neno lililokamilika kimaana na linalojisimamia. Hii ni kinyume na viambishi vinavyoambishwa kwenye mzizi wa neno. Utafiti huu utaainisha viangami vya Kiswahili kwa kuzingatia njia zile mbili zilizotumika katika uainishaji wa viambishi yaani, nafasi vinamotokea na uamilifu wake. Kwa kufanya hivi, mtafiti alibaini kufanana na kutofautiana kwa uambishaji wa viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili.

### 2.5.1 Uainishaji wa Viangami kwa Kuzingatia Nafasi Vinamotokea

Kwa kuzingatia kigezo hiki, kipengele muhimu katika shughuli hii ya uainishaji ni neno kuu. Hili ni neno kamili ambalo ndilo huambishwa kiangami. Kulingana na

utafiti huu, viangami huweza kupatikana kabla ya neno kamili au baada ya neno. Matokeo ya utafiti yanadhihirisha kuwa viangami vinavyojitokeza kabla ya neno kuu ni vichache ikilinganishwa na viangami vinavyopatikana baada ya neno kuu. Maneno mawili yanapofuatana na yanawakilisha dhana fulani, kunao uwezekano mkubwa wa neno la pili kufupishwa. Hata hivyo, kunayo maneno machache yanayotokea mwanzoni na huishia kufupishwa. Hivyo basi tunazo aina mbili kuu za viangami kwa kuzingatia kigezo cha nafasi vinamotokea, viangami awali na viangami tamati.

#### 2.5.1.1 Viangami Awali

Hivi ni viangami ambavyo hupatikana kabla ya neno kuu, yaani mwanzoni mwa neno. Kwa mfano katika lugha ya Kiswahili kuna *twenzetu.* Kitenzi 'twende' kimefuatana na kimilikishi 'zetu'. Hivyo, kitenzi kimefupishwa na kuwa *twen.* Huu ni mfano wa kiangami awali. Mifano mingine ni:

| 39. | | **Neno lenye Kiangami** | | **Nenokuu** | **Umbotokeo** |
|---|---|---|---|---|---|
| | (a) | **Ma**ma | + | mkubwa | = **Ma**mkubwa |
| | (b) | **Ma**ma | + | mdogo | = **Ma**mdogo |
| | (c) | **Ma**ma | + | mkwe | = **Ma**mkwe |
| | (d) | **Ma**ma | + | vyaa | = **Ma**vyaa |
| | (e) | **Ba**ba | + | mdogo | = **Ba**mdogo |
| | (f) | **Ba**ba | + | mkubwa | = **Ba**mkubwa |
| | (g) | **Ba**ba | + | mkwe | = **Ba**mkwe |
| | (h) | **Ba**ba | + | vyaa | = **Ba**vyaa |
| | (i) | **Bi**bi | + | mkubwa | = **Bi**mkubwa |
| | (j) | **Bi**nti | + | mdogo | = **Bi**mdogo |

Katika mifano hii yote (30 a-j), neno la pili ndilo neno kuu, hili ndilo neno linaloambishwa. Neno la kwanza linafupishwa na hivyo kuwa kiangami awali.

Baadhi ya mifano ya viangami awali inatokana na nomino za kinasaba. Nomino kama vile mama, baba, na bibi zinapofuatwa na kivumishi, nomino hizi hufupishwa na kuwa viangami.

Jedwali 2.7 linaonyesha namna viangami awali vinatokea katika maneno ya Kiswahili. Hapa, mtafiti alitumia neno moja kuonyesha lilivyoweza kuibuka na kushinda maumbo mengine yaliyokuwapo. Neno lenyewe ni 'bimdogo'. Mashartizuizi yaliyoyotumika ni pamoja na FIKI-UKO na SHABI.

FIKI-UKO huweka ukomo wa kiwango cha udhahania baina ya umboghafi na maumbotokeo. FIKI-UKO huzuia udondoshaji wa kitamkwa chochote kilichokuwa katika umboghafi. Kulingana na sharti hili, ni lazima umbotokeo lifikie ukomo wa kukubalika.

SHABI ina seti ndogo tatu za mashartizuizi. Kwanza kuna SHABI-(SI) ambalo huzuia mabadiliko ya sifa na hivyo kuhakikisha kuwa kuna mshabaha wa sifa za vitamkwa baina ya maumboghafi na maumbotokeo. SHABI- (JI) huzuia mabadiliko ya jinsi ya matamshi baina ya maumboghafi na maumbotokeo. Mwisho, kuna SHABI- (PA). Hili ni shartizuizi linalozuia mabadiliko ya mahali pa matamshi baina ya maumboghafi na maumbotokeo.

Lifuatalo ni jedwali linalohusu ukiukwaji wa mashartizuizi ya *bimdogo*. Neno kuu ni mdogo. Kiangami kimetokana na kufupisha nomino *bibi.* Silabi moja tu ndiyo iliyoambishwa kwa neno kuu.

**Jedwali 2.7 Ukiukwaji wa Mashartizuizi ya 'Bibi mdogo'**

| /Binti+mdogo/ | H-KODA | *II | SHABI | FIKI-UKO | TEGE |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) ☞bi-m-do-go | | | | * | |
| (b) bi-m-doo | | * | * | * | |
| (c) bi-nti-go | | | * | | * |
| (d) bi-m-dog | * | | * | * | |

Kulingana na Jedwali 2.7, neno *bibi* linapofuatana na neno *mdogo* katika sentensi, neno la kwanza *bibi* ndilo linalofupishwa na kuna kuwa na kiangami *–bi-*. Neno *mdogo* linakuwa ndilo neno kuu linaloambishwa kiangami. Miundo hiyo mingine haikubaliki katika Kiswahili sanifu na pia kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Mshindani (a) amekiuka sharti moja pekee la FIKI-UKO. Sharti hili linavumilika na hivyo basi anaibuka mshindi. Mshindai (b) amekiuka masharti matatu. Amekiuka sharti muhimu la II, kwani irabu mbili zimefuatana. Pia amekiuka sharti la SHABI pamoja na lile la FIKI-UKO. Mshindani (c) amekiuka sharti la TEGE kwani kuna sauti *t* ambayo haiko kwenye umboghafi. Mshindani (d) naye amekiuka sharti muhimu la H-KODA kwani silabi yake ya mwisho ni inaishia kwa konsonanti.

### 2.5.1.2 Viangami Tamati

Hivi ni viangami ambavyo hupatikana baada ya neno kuu. Matokeo ya utafiti yamedhihirisha kuwa viangami hivi ni vingi. Katika viangami awali, neno la

kwanza ndilo neno kuu. Neno kuu linabakia likiwa zima lakini neno linalofuata linafupishwa na hivyo kupata viangami tamati. Baadhi ya mifano ni:

| 40. | **Neno kuu** | **Kiangami** | **Neno Lenye Kiangami** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) | Sura | + -yo- | (**y**ak**o)** | = | sura*yo* |
| (b) | Sifa | + -ze- | (**z**ak**e)** | = | sifa*ze* |
| (c) | Na | + -nyi | (nyinyi) | = | na*nyi* |
| (d) | Na | + -si- | (sisi) | = | nasi |
| (e) | Na | + -ye- | (yeye) | = | na*ye* |
| (f) | Na | + -we- | (wewe) | = | na*we* |
| (g) | Kwa | + -vyo- | (hi**vyo)** | = | kwa*vyo* |
| (h) | Kwa | + -vyo- | (hi**vyo)** | = | kwavyo |
| (i) | Kwa | + -cho- | (hi**cho)** | = | kwacho |
| (j) | Wala | + -ni- | (nini) | = | wala*ni*? |
| (k) | Utakula | + -ni- | (nini) | = | utakula*ni*? |

Viangami awali vinaweza kuwa vya aina mbalimbali. Vinawakilisha dhana mbalimbali za kisarufi kama vile vimilikishi, vionyeshi, viulizi na hata viangami vya nafsi. Neno kuu pia linaweza kuwa la aina yoyote ile. Linaweza kuwa nomino, kiwakilishi, kihusishi, kitenzi na pia kivumishi. Viangami tamati ni vingi na vinawakilisha dhana nyingi ikilinganishwa na viangami awali. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa kuna viangami awali na viangami tamati. Matokeo haya ni sawa na yale ya viambishi.

### 2.5.2 Uainishaji wa Viangami Kiuamilifu

Kulingana na data iliyopatikana baada ya utafiti huu, viangami vya lugha ya Kiswahili vinaonekana kuwasilisha maana mbalimbali za kisarufi. Katika sehemu hii, viangami vinaainishwa kwa kuzingatia utendakazi wake wa kisarufi katika fungu. Utafiti huu unaonyesha kuwa viangami huweza kuwasilisha dhana kama

vile, kumilikisha, nafsi, kuashiria na pia kuuliza. Dhana hizi zilishughulikiwa kwa mapana. Mifano mwafaka ilitolewa.

#### 2.5.2.1 Viangami Vimilikishi

Kunavyo viangami vinavyoashiria umiliki, yaani ile hali ya kuwa na kitu, hali au jambo. Viangami hivi vinapatikana baada ya nomino kama vile nomino ya kawaida inapofuatwa na kivumishi kimilikishi. Kimilikishi kinafupishwa na kisha kinaambishwa kwa neno kuu kama kiangami. Viangami vimilikishi vinatokana na vimilikishi –angu, -ake, -ako na kadhalika. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya viangami vinavyotokana na vimilikishi:

41.

| | **Nenokuu** | | **Kiangami** | **Neno Lenye Kiangami** |
|---|---|---|---|---|
| (a) | Wana | + | wa**ngu** | = wana**ngu** |
| (b) | Mama | + | **y**ak**e** | = mama**ye** |
| (c) | Mama | + | ya**ko** | = mama**ko** |
| (d) | Sifa | + | **z**ak**e** | = sifa**ze** |
| (e) | Sifa | + | **z**ak**o** | = zifa**zo** |
| (f) | Kaka | + | ya**o** | = kaka**o** |
| (g) | Kaka | + | **y**ak**e** | = kaka**ye** |
| (h) | Kaka | + | ya**ko** | = kaka**ko** |
| (i) | Wenzi | + | w**enu** | = wenz**enu** |
| (j) | Wana | + | we**tu** | =wane**tu** |

Kulingana na mifano hii (41 a-j), neno kuu ni nomino. Neno kuu huweza kuwa nomino za aina mbalimbali ambazo zinafuatwa na kimilikishi. Hata hivyo, si lazima kila wakati nomino inapofuatwa na kimilikishi kupatikane kiangami. Kuna baadhi ya maneno yanakataa ufupisho huo na hayakubaliki katika Kiswahili. Jedwali 2.8 linaonyesha kuwa kuna baadhi ya viangami vimilikishi vinavyokubali

kuambishwa kwa nomino fulani lakini katika nomino zingine haviwezi kuambishwa.

**Jedwali 2.8: Viangami Vimilikishi**

| **-angu** | **-etu** | **-ako** | **-enu** | **-ake** | **-ao** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mamangu | Mametu | Mamako | Mamanu* | Mamake | mamao |
| Dadangu | Dadetu | Dadako | Dadanu* | Dadake | dadao |
| Kakangu | Kaketu* | Kakako | Kakanu* | Kakake | kakao |
| mwenzangu | mwenzetu | Mwenzako | Mwenzenu | Mwenzake | mwenzao |
| Bibingu* | Bibitu* | Bibiko* | Bibibu* | Bibike* | Bibio |
| Shangazingu* | Shangazitu* | Shangaziko* | Shangazenu* | Shangazike | Shabgazio |
| Babungu* | Babutu* | Babuko* | Babunu* | Babuke* | babuo |

Kulingana na Jedwali 2.8, kuna maneno ambayo yanakubali kuambishwa viangami vyote sita vya nafsi. Mfano mwafaka ni neno ‘mwenzi’ ambalo limeweza kuambishwa viangami vyote vya kumiliki katika nafsi zote tatu, umoja na wingi. Neno kama vile ‘kaka’ linakubali tu baadhi ya umiliki. Neno hili limekataa uambishi kama vile, *kaketu** na *kakenu**. Ingawa maneno yote mawili yanaonekana kuzingatia masharti ya Kiswahili, mipangilio yake haitumiki katika lugha ya Kiswahili. Kimilikishi *–angu* huunda viangami na maneno yanayoishia na irabu –a- hii ndiyo maana kimilikishi kinakataa kuambishwa kwa maneno kama vile bibi, babu na shangazi.

Kimilikishi –enu kinapounganishwa na maneno yanayoishia na irabu –a- kuna kuwa na mfanyiko wa kifonolojia ambapo –a- ya neno kuu hudondoshwa na kuunda maneno kama vile mamenu, kakenu na kadhalika.

### 2.5.2.2 Viangami vya Nafsi

Hivi ni viangami vinavyopatikana baada ya viwakilishi vya nafsi kufupishwa na kisha kuambatishwa kwa neno lililo kamili kama vile kitenzi, kiunganishi na pia kihusishi. Katika lugha ya Kiswahili kuna nafsi tatu. Nafsi ya kwanza ni 'mimi' katika umoja na 'sisi' katika wingi. Nafsi ya pili 'wewe' na 'nyinyi' nayo nafsi ya tatu ni 'yeye' na 'wao'. Ifuatayo ni mifano ya viangami nafsi.

| 42 | Nenokuu | | Kiangami | | | Neno Lenye Kiangami |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | (a) Si | + | -ye- | (yeye) | = | Siye |
| | (b) Si | + | -o- | (wa**o)** | = | Sio |
| | (c) Si | + | -nyi- | (nyinyi) | = | Sinyi |
| | (d) Na | + | -mi- | (mimi) | = | Nami |
| | (e) Na | + | -we- | (wewe) | = | Nawe |
| | (f) Na | + | -ye- | (yeye) | = | Naye |
| | (g) Na | + | -si- | (sisi) | = | Nasi |
| | (h) Na | + | -o- | (wa**o)** | = | Nao |

Kulingana na mifano hii, si maneno yote yanayoweza kuambishwa viangami nafsi. Baadhi ya maneno yaliyotumika ni vitenzi vishirikishi na pia viunganishi. Katika Mfano 42 (a) hadi (c), kitenzi kishirikishi *si* kimetumika kama neno kuu. Nayo mifano kutoka (d) hadi (h), kiunganishi *na* kimetumika kama neno kuu.Kuna baadhi ya maneno ambayo yanakubali kuambishwa kiangami katika hali ya kuyakinisha lakini unapokanusha kiangami hakikubaliki. Kwa mfano:

| 43. | Kuyakinisha | Kukanusha | |
|---|---|---|---|
| | (a) na**we** | si**we** | **(**wewe**)** |
| | (b) na**ye** | si**ye** | **(**yeye**)** |
| | (c) na**mi** | si**mi** * | (mimi) |
| | (d) na**si** | si**si***! | (sisi) |

Kulingana na mfano 43 (a na b), viangami vinakubali kuambishwa katika hali yakinishi na pia katika hali ya ukanushi. Katika 43 (c na d), kiangami kinaambishwa katika hali yakinishi na pia hali ya kukanusha. Tunapoambisha kiangami –mi- kwa neno kuu **si**, neno linalopatikana katika hali ya kukanusha ni *simi*. Hili halitumiki sana katika lugha ya Kiswahili.

### 2.5.2.3 Viangami Viashiria

Hivi ni viangami aina ya viashiria vinavyopatikana baada ya neno. Kiashiria hufupishwa na kuunganishwa na neno lingine lililokamilika kimaana. Viashiria vinaainishwa mara tatu. Kuna vile vya ujirani, viashiria vya mbali kidogo na viashiria vya mbali. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya viangami viashiria.

| **44.** | **Nenokuu** | **Kiangami** | | **Neno Lenye Kiangami** |
|---|---|---|---|---|
| | (a) Na + | hi**cho** | = | Nacho |
| | (b) Na + | hu**ko** | = | Nako |
| | (c) Na + | hi**yo** | = | Nayo |
| | (d) Na + | hi**lo** | = | Nalo |
| | (e) Na + | ha**po** | = | Napo |
| | (f) Kwa+ | hi**vyo** | = | Kwavyo |
| | (g) Kwa+ | hi**cho** | = | Kwacho |
| | (h) Kwa+ | hi**lo** | = | Kwalo |

Baadhi ya mifano katika aina hii ya viangami inatokana na viashiria vya mbali kidogo. Viashiria vya ujirani wa mbali, karibu na vya mbali zaidi havitumiki kama viangami.

### 2.5.2.4 Viangami Viulizi

Hivi ni viangami vinavyopatikana baada ya neno ambalo ni kiulizi kufupishwa na kisha kuambishwa kwenye neno kuu. Neno kuu laweza kuwa kitenzi au hata kihusishi. Neno linalopatikana baada ya kuambisha kiangami kwa neno kuu hufanya kazi ya kuulizia swali. Baadhi ya mifano ya viangami viulizi ni kama vile.

| 45 | **Neno kuu** | | **Kiangami** | | **Umbotokeo** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **(a)** Kwa | + | -ni- (nini) | = | kwani? |
| | (b) Wanitakia | + | -ni- (nini) | = | wanitakiani? |
| | (c) Wala | + | -ni- (nini) | = | walani? |
| | (d) Utakula | + | -ni- (nini) | = | utakulani? |
| | (e) Twenda | + | -pi- (wapi) | = | twendapi? |
| | (f) Alisema | + | -ni- (nini) | = | alisemani? |

Katika mfano huu, kiangami kilichotumika ni –*ni*- kinachotokana na kiulizi *nini*, na kiangami –*pi*- kinachotokana na kiulizi *wapi*. Katika lugha ya Kiswahili, viulizi ni vya aina nyingi ila si vyote vilivyo na uwezo wa kufupishwa na kuwa viangami. Katika utafiti huu kuna viulizi ambavyo havikuweza kuvunjwa kwa mfano ‘ngapi’ na ‘gani’.

Utafiti huu unabainisha kuwa viangami huweza kuainishwa kwa kuzingatia kigezo hiki cha uamilifu sawa na ilivyo katika viambishi. Baada ya kuangazia vigezo vyote viwili, tofauti zilibainika. Sehemu inayofuata imeshughulikia tofauti kati ya viangami ni viambishi

## 2.6 Tofauti kati ya Viangami na Viambishi katika Lugha ya Kiswahili

Katika lugha ya Kiswahili, vipashio vidogo huweza huambishwa kwa vile vikubwa. Hii ni kwa sababu Kiswahili ni lugha ambishi bainifu. Kiambishi na

kiangami vyote ni vipashio vidogo vilivyo na uwezo wa kuambishwa kwa vipashio vingine. Viangami na viambishi huambishwa kwa njia tofauti. Hebu basi tuangalie tofauti kati ya viangami na viambishi.

### 2.6.1 Viangami Huambishwa kwa Neno, Viambishi Huambishwa kwa Mzizi

Kutokana na utafiti hii, ni wazi kuwa viangami vya lugha ya Kiswahili huambishwa kwa maneno kamili. Kiangami huambishwa kwa aina tofauti za maneno kama vile nomino, kiwakilishi, kitenzi na kihusishi. Neno lililokamilika huwa ndilo neno kuu ambalo linaambishwa kiangami mwanzoni au mwishoni. Tazama mifano ifuatayo:

**46.** **Neno Lililoambishwa** **Aina ya Neno Kuu**

| | |
|---|---|
| (a) mwana**o** | nomino |
| (b) nikupe**ni** | kitenzi |
| (c) cha**mcha** | kihusishi |

Kwa upande mwingine, viambishi katika lugha ya Kiswahili huambishwa kwenye mzizi wa neno. Ili kuwe na viambishi ni sharti kuwe na mzizi wa neno. Mzizi huweza kuwa wa kitenzi, nomino, kivumishi, kiwakilishi na pia kielezi. Tazama mifano ilifuatayo:

47. **Neno Lililoambishwa Kiambishi** **Mzizi wa Neno**

| | |
|---|---|
| **(a)** a-na-ye-**chez-**a | -chez- |
| (b) a-na-ye-**pik**-a | -pik- |
| (c) a-na-ye-**lim**-a | -lim- |

Kwa mujibu wa mifano hii, ni wazi kuwa viangami na viambishi huambishwa kwa vipashio vya ngazi tofauti. Kiangami kinaambishwa kwa neno kamili kisarufi ilhali viambishi huambishwa kwenye mzizi ambao ni sehemu ya neno isiyobadilika hata wakati neno linanyambuliwa.

### 2.6.2 Viangami na Viambishi Huwakilisha Dhana Tofauti

Tofauti ya pili ni kuwa dhana zinazowakilishwa na viambishi ni tofauti na dhana zitokanazo na viangami. Viambishi vinawakilisha dhana za kisarufi kama vile wakati, njeo, hali, mtendwa, mnyambuliko na kadhalika. Kwa upande ule mwingine viangami huwakilisha dhana kama vile, umiliki, nafsi, viashiria na viulizi. Tazama mifano hii:

48. **Viambishi**

| Ngeli | wakati | kirejeshi | mzizi | kauli | kiishio |
|---|---|---|---|---|---|
| I | na | yo | pik | i | a |
| Li | li | lo | pik | w | a |
| Ki | na | cho | pik | w | a |

### 2.6.3 Viangami Hubadilika ila Viambishi Havibadiliki

Tofauti ya tatu ni kuwa baadhi ya viambishi hubaki jinsi vilivyo vinapoambishwa katika maneno tofauti. Kwa mfano, kiambishi –li- cha hali ya kuyakinisha wakati uliopita hakibadiliki hata kinapoambishwa kwenye mizizi tofauti, kwa mfano,

49.

| Wakati Uliopo | Wakati Uliopita | Wakati Ujao |
|---|---|---|
| a-**na-**som-a | a-**li**-som-a | a-**ta**-som-a |

| | | |
|---|---|---|
| wa-**na**- chez-a | wa-**li**-chez-a | wa-**ta**-som-a |
| ki-**na**-anguk-a | ki-**li**-anguk-a | ki-**ta**-anguk-a |

Kulingana na mifano hii, viambishi vya wakati havibadiliki. Viambishi *–na-*, *-li-*, na *–ta-* vinabaki jinsi vilivyo katika maneno mbalimbali. Hata hivyo viambishi vya ngeli hubadilika kutegemea ngeli ya nomino inayorejelewa.

Kwa upande mwingine kuna viangami vichache ambavyo huwa tofauti lakini dhana inayowakilishwa ni ile ile. Kwa mfano,

| 50. | **Neno kuu** | | **Kiangami** | **Neno Lenye Kiangami** | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mama | + | (ye) yake | = | mamaye |
| | Mama | + | (ke) yake | = | mamake |
| | Dada | + | (ke) yake | = | dadake |
| | Dada | + | (ye) yake | = | dadaye |
| | Kaka | + | (ke) yake | = | kakake |
| | Kaka | + | (ye) yake | = | kakaye |

Kulingana na mfano huu, neno *yake* linapofupishwa na kuwa kiangami, linachukua maumbo tofauti. Maumbo *ye* na *ke* ni tofauti lakini dhana inayowakilishwa ni sawa, yaani umiliki katika nafsi ya tatu. Katika mfano 50, mifano yote inafuata michakato tofauti ya kuunda viangami. Jambo hili haliwezekani katika uundaji wa viambishi.

### 2.6.4 Mabadiliko katika Neno Jipya

Kiangami kinapoambishwa kwenye neno kuu, hakibadilishi aina ya neno wala maana asili ya neno lile. Kwa mfano, tukiambisha kiangami *–ngu-* katika neno

*dada*, tunapata *dadangu*. Maana inayopitishwa katika neno *dadangu* ni sawa na maana katika kirai *dada yangu*. Pili, neno *dada* linabaki kuwa nomino. Hivyo basi kuambisha kiangami katika neno kuu hakubadilishi kategoria ya neno husika. Kwa upande mwingine, viambishi huweza kubadilisha maana ya neno na pia aina ya neno. Hii ina maana ya kuwa, kila kiambishi katika neno fulani huwa na jukumu lake la kisarufi. Kwa kubadilisha kiambishi kimoja, basi maana ya neno pia hubadilika. Tazama mifano hii:

| 51. | **Mzizi** | **Neno Lenye Viambishi** | **Aina ya Neno** |
|---|---|---|---|
| | -som- | a-na-som-a | kitenzi |
| | -som- | ma-som-o | nomino |
| | -som- | u-som-i | nomino |

### 2.6.5 Viangami ni kwa Virai, Viambishi ni kwa Neno

Kutokana na utafiti huu, viangami vinahusishwa na kirai. Kiangami ni neno moja linalofupishwa na kuambishwa kwa neno lililo jirani katika sentensi. Hii ina maana kuwa kiangami na neno kuu ni aina ya kirai. Kwa mfano, *shangazi yake* ni kirai nomino kilichoundwa kwa nomino na kivumishi. Kivumishi *yake* kinapofupishwa tunapata kiangami –ye- ambacho kinaambishwa kwa nomino *shangazi*. Neno jipya linalopatikana linabaki kuwa kirai nomino. Kwa upande mwingine, kiambishi hupatikana tu katika neno pekee.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imebainisha kuwa viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili ni vipashio viwili tofauti. Sifa zake hufanana na pia kutofautiana kwa kiasi fulani. Ni wazi kuwa kama ilivyo katika kiambishi, kiangami ni kiungo cha kisarufi kinachoweza kuambatishwa kwa vipashio vingine vya kisarufi. Kinyume na kiambishi kinachoambishwa kwenye mzizi wa neno, kiangami huambatishwa kwa neno lililo kamili na linalojisimamia kimaana. Katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi awali na viambishi tamati. Kama tulivyoona katika utafiti huu, viangami pia huweza kuambishwa mwanzoni mwa neno au pia baada ya neno lililokamilika. Sura ya tatu inaangalia utaratibu unaofuatwa wakati wa kuunda viangami katika lugha ya Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia ya umbo upeo.

# SURA YA TATU

# UTARATIBU WA UUNDAJI WA VIANGAMI VYA KISWAHILI

## 3.1 Utangulizi

Sura ya pili iliweka wazi uambishaji wa viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alionyesha maumbo mbalimbali ya viangami na namna yalivyoambishwa. Basi sura hii ya tatu ilishughulikia utaratibu wa uundaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Kwanza, sarufi ya Kiswahili ilijadiliwa kwa muhtasari.

Kabla ya kushughulikia taratibu za uundaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili, mtafiti aliangazia baadhi ya vipashio vya lugha ya Kiswahili na sheria zinazofuatwa na kila kipashio. Lengo la kushughulikia vipashio hivi ni kuonyesha kuwa kiangami ni kipashio cha lugha ya Kiswahili. Kama mojawapo wa vipashio vya lugha ya Kiswahili, viangami huzingatia kanuni za kisarufi zilizokubalika.

Nadharia ya umbo upeo imetumika kuweka wazi baadhi ya tarartibu zinazozingatiwa na viangami vya Kiswahili. Kanuni zinazoongoza uundaji wa viangami zinatokana na sheria za kisarufi za lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni lugha ambishi bainishi kwani inavyo vipashio mbalimbali. Kila kipashio huundwa kwa kuzingatia utaratibu fulani ili kiwe na maana inayokubalika. Kipashio ni kipande cha tungo ambacho huweza kujenga au kujengwa na tungo nyingine. Ili kuweza kuunda vipashio vinavyokubalika, ni vyema kuzingatia sheria za kisarufi za lugha husika. Kiangami kama mojawapo

wa vipashio vya lugha ya Kiswahili, huundwa kwa kuzingatia utaratibu unaokubalika kisarufi.

### 3.2 Sarufi ya Lugha ya Kiswahili

Kwa mujibu wa Massamba (2009), sarufi ni taaluma ya uchambuzi wa lugha inayojumuisha viwango vyote vya uchambuzi. Viwango hivi ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kila kiwango kimetawaliwa na sheria fulani ambazo zimekubalika katika lugha husika. Sarufi ya Kiswahili imejigawa katika viwango vitatu ambavyo ni sarufi maumbo, sarufi miundo na sarufi sauti.

Sarufi maumbo ni kiwango cha isimu ambacho hushughulikia namna maneno ya lugha yanavyoundwa kulingana na lugha. Kila lugha huwa na utaratibu fulani wa kuunda vipashio vyake. Utaratibu unaofuatwa ndio unaoifanya lugha iwe sahihi na ikubalike na wanajamii.

Kiwango hiki cha isimu hushughulikia namna ambavyo maneno ya lugha huundwa. Kila lugha huwa na utaratibu fulani wa kuunda maneno. Sarufi maumbo hushughulikia jinsi mofimu mbalimbali huungana ili kujenga neno au maneno katika lugha.

Sarufi miundo ni tawi la isimu ambalo hushughulikia uchanganuzi wa taratibu na kanuni zilizopo baina ya maneno katika lugha. Sarufi maumbo huangalia sheria au kanuni ambazo lazima zifuatwe ili kupanga maneno ya lugha katika mfuatano. Kila lugha ni sharti ifuate utaratibu uliopo wa mpangilio wa maneno katika

sentensi ili kupata tungo zinazokubalika katika lugha husika. (Massamba na wengine 2009). Kwa mujibu wa Radford (1981), isimu miundo ni taaluma inayojishughulisha na namna maneno yanavyoweza kupangwa pamoja ili kuwa na muundo wa sentensi.

Sarufi sauti ni kiwango cha sarufi kinachochunguza mfumo wa sauti katika lugha. Sarufi sauti huchambua jinsi sauti za lugha zinaungana ili kujenga maneno yanayokubalika katika lugha ile. Kila lugha ina utaratibu wa mpangilio wa sauti unaofuatwa ili kuunda vipashio vingine kama vile mofimu, silabi na maneno. Kuna mfuatano unaokubalika ila kuna mwingine usiokubalika kutegemea lugha husika.

**3.3 Vipashio vya Lugha ya Kiswahili**

Kutokana na utafiti huu, ni wazi kuwa kiangami ni kipashio cha lugha ya Kiswahili. Hebu kwanza tufasili maana ya kipashio. Kipashio ni kipande cha tungo ambacho hujenga au hujengwa na tungo nyingine. Baadhi ya vipashio vya lugha ya Kiswahili ni sauti, silabi, mofimu, neno na sentensi. Vipashio ni muhimu kwa kila lugha kwani ndivyo hujenga sarufi ya lugha husika. Yanayofuata ni maelezo ya kila kipashio tulichotaja. Kwanza, tutaanza na kipashio kidogo zaidi ambacho ni sauti na tumalizie na kile kikubwa.

Kipashio kidogo zaidi katika lugha ya Kiswahili ni sauti. Sauti ni mlio unaotokatana baada ya mgongano wa ala za kutamkia kama vile ulimi, meno, midomo na kadhalika. Kila lugha huwa na sauti zinazotumika na wanajamii katika

mawasiliano yao. Lugha ya Kiswahili inazo aina mbili za sauti: irabu kama vile /o/ na konsonanti kama vile /p/.

Silabi ni kipashio cha utamkaji kinachoruhusu sauti kutamkwa kama fungu moja. Kwa mujibu wa Njogu na wengine (2006), silabi ni sauti au mwambatano wa sauti unaoweza kutamkika. Hili ndilo tamko la chini na dogo kabisa. Mfano wa silabi ni:

52. /Ki$swa$hi$li/

/vi$a$nga$mi/

/ki$a$mbi$shi/

Kulingana na mifano 52, kila silabi inatamkika kivyake kama tamko moja. Silabi huweza kuwa sauti moja, mbili au hata tatu. Cha muhimu ni kuwa sehemu hiyo ya neno inatamkika. Silabi za Kiswahili haziwakilishi maana yoyote ile ya kisarufi kwani ni tamko tu. Hata hivyo kuna wakati ambapo silabi na mofimu hushahibiana. Kwa mfano katika neno ***ni-ta-ka-po-ku****-j-a*, silabi zinazotokea kabla ya mzizi *–j-* ni mofimu pia kwani kuna maana ya kisarufi inayowakilishwa. Maana inayowakilishwa ni nafsi (ni), wakati (ta), hali (ka) na wakati (po). Tunapoweka silabi zaidi ya moja pamoja, tunapata neno kamili lililo na maana na pia tuweza pata mofimu moja.

Mofimu ni kipashio kidogo kabisa cha kisarufi kilicho na maana. Hiki ndicho kipashio kidogo kabisa amilifu katika maumbo ya neno. Mofimu ni kipashio dhahania cha umbo fulani ambacho huwakilishwa na mofu tofauti tofauti katika mazingira mbalimbali (Hartman, 1990). Hivyo basi, ni sawa kusema kuwa mofimu

ndicho kipashio kidogo zaidi katika lugha kilicho na maana ya kisarufi. Hakina uwezo wa kuvunjwa kwani kikivunjwa basi kitapoteza maana yake ya kisarufi. Mofimu huweza kuwa neno au sehemu ya neno.

Neno ni mfuatano wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa na huweza kuwa na maana ya kileksia au kisarufi. Neno huundwa kwa mofimu zaidi ya moja au hata mofimu moja ikawa neno kamili. Mofimu huru huunda neno huru nazo mofimu changamano huunda neno changamano. Katika lugha ya Kiswahili, kila neno huwa na maana yake. Maneno mengi yenye maana yanapopangwa kwa utaratibu fulani, huunda kipashio kikubwa na ambacho ni sentensi.

Sentensi ni kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo chenye maana kamili (Massamba, na wengine 1999). Kila sentensi ya Kiswahili ni lazima ikamilike kimaana na pia kisarufi. Kimuundo, kila sentensi ya lugha ya Kiswahili huwa na muundo wa kiima na kiarifu au kundi nomino na kundi tenzi.

Tulivyovitaja ni baadhi vipashio vya lugha ya Kiswahili. Kinachodhihirika hapa ni kuwa, kunao utaratibu wa kuunda kila kipashio. Vipashio vile vidogo huungana na kuunda vipashio vikubwa. Kuna vipashio vilivyo na maana ya kisarufi kama vile mofimu, neno na sentensi lakini kuna vipashio vingine havina maana ya kisarufi kama vile sauti na silabi.

Kiangami ni mojawapo wa vipashio katika lugha ya Kiswahili. Kama ilivyo katika vipashio vingine, viangami hufuata utaratibu fulani. Viangami katika lugha ya Kiswahili havipatikani wala kutumika kisadfa tu. Kunao utaratibu wa lugha

unaozingatiwa wakati wa uundaji wa viangami vya lugha ya Kiswahili. Katika sehemu inayofuata, mtafiti alieleza matokeo yake ya utafiti kuhusu utaratibu wa uundaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili.

### 3.4 Utaratibu wa Uundaji wa Viangami vya Lugha ya Kiswahili

Katika sehemu hii ya utafiti, mtafiti alirejelea baadhi ya sheria zilizofuatwa wakati wa kuunda viangami vya lugha ya Kiswahili. Mtafiti pia aliangazia kwa kifupi tu baadhi ya sheria zilizotukimika katika uundaji wa viangami katika lugha zingine duniani. Kila lugha huwa na sheria zinazoiongoza katika matumizi na uundaji wa vipashio vyake. Viangami ni mojawapo wa vipashio katika lugha ya Kiswahili.

Kama tulivyoona katika sura ya kwanza, vipashio vyote vya lugha ya Kiswahili huzingatia sheria fulani. Kila lugha inazo sheria zake za kisarufi. Sheria hizo ndizo huvipa vipashio hivyo maana na pia kuvifanya vikubalike katika lugha husika.

Katika lugha ya Kiswahili, viangami havitokei kisadfa tu wala kuundwa kiholela bali hufuata sheria fulani. Sheria hizi ndizo huwaongoza wanajamii ili watumie viangami mwafaka katika maandishi yao na maongezi yao ya kila siku. Katika sehemu hii ya utafiti, nadharia ya umbo upeo ilitumika kama mwongozo.

Nadharia ya umbo upeo imeongozwa na masharti-zuizi ambayo yalizingatiwa katika utafiti huu. Kwa mujibu wa Kager (1999), mashartizuizi huweka vigezo ambavyo huamua umbo linalofikia ukubalifu. Kutokana na maelezo yake Kager, umbo la kipashio fulani hukubalika linapotimiza mahitaji yote yanayohitajika.

Sheria za kisarufi katika lugha ya Kiswahili ndizo zinafanya matumizi ya viangami yakubaliwe na wanajamii pamoja na wanaisimu katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya sheria zinazozingatiwa katika uundaji na uambishaji wa viangami ni zile zile zinazopatikana katika vipashio vingine vya lugha ya Kiswahili.

Baadhi ya miundo iliyopatikana katika viangami vya Kiswahili ilidhihirisha kuwa viangami vinafuata sheria fulani. Hebu sasa tuangalie sheria hizi katika sehemu inayofuata. Sheria zilizoshughulikiwa katika sehemu hii ni kama zifuatazo:

1. Viangami ni vipashio vinavyotamkika kwa mkupuo
2. Viangami ni vipashio vya irabu moja
3. Maana halisi ya kiangami hubakia
4. Lazima maneno yanayoathirika yafuatane
5. Kiangami huhusiana na neno kuu kisarufi
6. Neno moja hupachikwa kiangami kimoja
7. Hakuna kiangami cha konsonanti pekee

Sheria hizi saba ndizo zilizotambulika wakati wa utafiti. Sheria hizi zote zilielezewa kwa mapana moja baada ya nyingine kwa kutumia mifano mwafaka. Sehemu inayofuata inaelezea sheria hizi.

### 3.4.1 Viangami ni Aina ya Silabi Kamili

Kulingana na utafiti huu, viangami vya Kiswahili ni lazima viweze kutamkika kivyake na kwa mkupuo mmoja; yaani sehemu katika neno ambayo huwa ni

kiangami hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. Viangami vya lugha ya Kiswahili huchukua muundo wa silabi. Kiangami cha Kiswahili huwa ni sehemu ya neno inayotamkika. Hivyo basi viangami vya Kiswahili ni aina ya silabi kamili. Katika lugha ya Kiswahili, silabi ni kiungo cha neno ambacho hujumuisha vokali moja. Hata hivyo, katika lugha ya Kiswahili sauti za nazali *m* na *n* huweza kujisimamia kama silabi kwa muktadha fulani. Kwa mfano katika m-tu na n-ta.

Jedwali 3.1 limetumika kuonyesha baadhi ya viangami ambavyo vinatamkika kwa mkupuo mmoja.

**Jedwali 3.1 Viangami ni Aina ya Silabi Kamili**

| | **Kiangami** | **Nenokuu** | **Neno lililoambishwa** |
|---|---|---|---|
| a. | -ma- (mama) | Mkwe | /$**ma$**m$kwe$/ |
| b. | -mi- (mimi) | Na | /$na$**mi**$/ |
| c. | -o- (wao) | Wana | /$wa$na$**o**$/ |

Kwa mujibu wa mifano katika Jedwali 3.1, viangami vya lugha ya Kiswahili ni vipashio vinavyotamkika kwa mkupuo mmoja. Katika mfano (b), kiangami -ma- kimetokana na neno lililokamilika *mama.* Muundo wake ni wa konsonanti moja ikifuatwa na irabu moja. Kiangami -ma- kinapoambishwa kwenye neno kamili *mkwe*, kinachukua sehemu ya neno ambayo inatamkika kwa mkupuo mmoja. /$**ma$**m$kwe$/

Muundo wa silabi hujumuisha vipengele vitatu muhimu kama anavyoeleza Mwihaki (20I6). Kwanza kuna kilele (KE), ambacho ndicho kiini cha silabi. Kilele ni kiungo cha lazima katika muundo wa silabi. Kilele huwa na irabu. Kipengele cha pili ni tangulizo (TA). Tangulizo ni sauti ambazo huja kabla ya kilele. Tangulizo huundwa kwa konsonanti moja au zaidi. Mwisho, kuna fungio (FU) au koda. Hiki ni kiungo kinachofuata kilele. Fungio huundwa kwa konsonanti moja au zaidi. Hiki si kiungo cha lazima katika silabi.

Kulingana na utafiti huu, viangami vya Kiswahili ni lazima viwe na irabu mwishoni. Kwa kawaida matamshi ya Kiswahili hayakatizwi ghafla. Viangami vya Kiswahili pia havikatizwi ghafla wakati wa matamshi kwani vinaishia na irabu. Hii ina maana kuwa viangami vya Kiswahili huchukua muundo wa silabi wazi.

Viangami vya lugha ya Kiswahili havina fungio au koda. Hii ina maana kuwa viangami katika lugha ya Kiswahili huishia kwenye kilele. Ifuatayo ni mifano ya viangami:

| 53. | **Neno kuu** | **Kiangami** | | **Umbotokeo** |
|---|---|---|---|---|
| | (a) Mama | -ngu- | (yangu) | mama**ngu** |
| | (b) Utakula | -ni- | (nini) | utakula**ni** |
| | (c) Mdogo | -ma- | (mama) | **ma**mdogo |

Kwa mujibu wa Mifano 53 (a, b, na c), viangami ni vipashio vinavyochukua muundo wa silabi wazi. Viangami awali na viangami tamati vyote vinachukua muundo wa silabi wazi yaani haviishii na koda.


54. (a) #ma$ma$ngu#

(b) #U$ta$ku$la$ni#

(c) #ma$m$do$go#

Viangami katika 54, ni aina ya silabi wazi. Mfano -*ngu*-, -*ni*- na –*ma*- ni aina ya silabi. Silabi hizi zimeishia na irabu. Mfano 54 unaonyesha muundo wa viangami vya Kiswahili kama silabi wazi. Hebu sasa tuonyeshe muundo wa silabi katika neno lililoambishwa kiangami. Mfano wa neno uliotumika ni *mamangu*. Hili ni neno moja lililounganishwa na kiangami. Neno kuu hapa ni nomino *mama*. Kiangami ni –ngu- ambacho kimetokana na neno kamili *yangu*. Tazama mfano ufuatao.

55. **Muundo katika Neno *mamangu***




Mchoro 55 unadhihirisha kuwa viangami vya Kiswahili ni aina ya silabi wazi kwani kiangami -*ngu*- hakiishii kwa fungio. Sheria hii imeongozwa na baadhi ya

mashartizuizi kama vile, H-KODA (silabi huishia na koda), KILELE (kila silabi iwe na kiini au kilele) na SHABI-JI (hakuna mabadiliko ya kimatamshi kati ya umboghafi na umbotokeo). Mtafiti alitumia jedwali kuonyesha matumizi ya mashartizuizi haya kulingana na nadharia ya umbo upeo. Tazama Jedwali 3.2 lifuatalo.

**Jedwali 3.2: Viangami na Mashartizuizi ya Nadharia ya Umbo Upeo**

| /mama+yangu/ | **H-KODA** | **KILELE** | **SHABI-JI** | **SHABI-SI** |
|---|---|---|---|---|
| (a) ☞ma-ma-ngu | | | * | |
| (b) ma-ma-yng | * | * | * | |
| (c) ma-ma-ya | | | * | *! |

Katika Jedwali hili 3.2, mshindani (a) ndiye mshindi mshindi kwani anakubaliana na baadhi ya mashartizuizi. Mshindani (a) amevunja sharti moja tu la SHABI-JI ambalo linavumilika. Tunaona kuwa kiangami -ngu- hakina koda na ni aina ya silabi iliyo na kilele. Mshindani (b) amekiuka masharti yote matatu ambayo ni SHABI-JI, H-KODA na KILELE. Mshindani (c) anakiuka sharti moja muhimu ambalo ni SHABI-JI. Baada ya kulinganisha washindani wote watatu, ni wazi kuwa mshindani (a) ameshinda kwani hajakiuka masharti muhimu. Hii inaonyesha kuwa ni lazima viangami vya Kiswahili vizingatie masharti muhimu.

Kulingana na utafiti huu ni wazi kuwa mojawapo wa kanuni za uundaji viangami ni kuwa kiangami sharti kifuate muundo wa silabi wazi. Katika lugha ya Kiswahili, kipashio kinachokubalika kuwa kiangami ni lazima kiwe na uwezo wa

kujisimamia kimatamshi. Baada ya kuangalia kanuni ya kwanza ya uundaji wa viangami vya lugha ya Kiswahili sasa tutaangalia kanuni ya pili.

### 3.4.2 Viangami huwa na Irabu Moja

Kulingana na utafiti huu, sheria nyingine iliyoonekana kufuatwa katika uundaji wa viangami ni kuwa, viangami vya Kiswahili huwa na irabu moja. Viangami vya Kiswahili huweza kuundwa kwa konsonanti na irabu, konsonanti mbili zikiambatana na irabu moja au irabu moja pekee. Hii ni kinyume na baadhi ya lugha kama vile Kiingereza pale ambapo kiangami huweza kuundwa kwa konsonanti pekee.

56. **Viangami vya Kiswahili**

(a) Shangazi*ye*

(b) *Bi*mkubwa

(c) Hamna*zo*

57. **Viangami katika Kiingereza**

| | |
|---|---|
| (a**)** She'*s* | yeye ni |
| (b) They'll | wao wata… |
| (c) They're | wao ni |

Mifano 56 na 57 imetumika kuonyesha mifano ya viangami katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza mtawalia. Viangami vya Kiswahili vimeundwa na konsonanti ikifuatwa na irabu kama vile *–ye-*, -*bi*- na -*zo*-. Tazama mfano 56. Viangami vya Kiingereza vinaweza kuundwa na konsonanti moja pekee au hata

konsonanti mbili kama vile, -*s*-, -*ll*- na –*re*-. Kimatamshi, kiangami '*ll* hutamkwa kama konsonanti moja. Kiangami *'re* nacho kimefupishwa kimaandishi tu ila si kimatamshi kwani kimatamshi, *they're* na *they are* hutamkwa sawa. Tazama mfano 57. Viangami vya Kiswahili hutamkika kwa urahisi kwani vimeundwa kwa irabu. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya viangami vinavyochukua muundo wa silabi wazi.

| 58. | **Neno kuu** | **Kiangami** | **Neno lenye Kiangami** |
|---|---|---|---|
| | (a) Mwana | -o- (wao) | mwa-na-**o** |
| | (b) Shangazi | -ye- (yake) | sha-nga-zi-**ye** |
| | (c) Kaka | -ngu- (yangu) | ka-ka-**ngu** |

Kwa mujibu wa mifano hii, viangami vya Kiswahili vinachukua miundo mbalimbali. Hata hivyo, ni sharti kuwe na irabu. Kiangami cha kwanza -o- kimeundwa na irabu moja pekee. Kiangami cha pili -ye- kimeundwa kwa sauti mbili, konsonanti ikifuatwa na irabu. Nao mfano wa mwisho (3) -ngu- ni kiangami cha sauti tatu ambazo ni konsonanti mbili zikiambatana na irabu moja. Katika mifano yote mitatu, ni wazi kuwa viangami vya Kiswahili huweza kuchukua maumbo mbalimbali lakini ni sharti viishie na irabu.

Kuwepo kwa irabu katika viangami vya Kiswahili huwezesha viangami vile vitamkwe kama fungu moja la sauti linalojisimamia. Kutamkika kwa kiangami kwa mkupuo mmoja ni muhimu kwani kunasaidia katika kuunda mapigo ya sauti kwenye neno lililoambishwa kiangami.

Jedwali 3.3 limetumika kudhihirisha mashartizuizi ya nadharia ya umbo upeo kwa kutumia neno /mwana + wangu/

**Jedwali 3.3 Ukiukwaji wa Mashartizuizi Kuhusu *mwana wangu***

| **Umbo msingi** /mwana+wangu/ | **II** | **KKKB** | ***YK** | **HKODA** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) ☞mwa.na.ngu | | | | | * |
| (c) Mwa.na.wng | | *! | * | * | * |
| (c) mwa.nau | *! | | | | * |

Jedwali 3.3 linaonyesha jinsi neno *mwanangu* linavyodhihirisha matumizi ya nadharia ya umbo upeo. Mshindani (a) hajakiuka sharti lolote lile muhimu kwa yale masharti yaliyotumika. Mshindani huyu amekiuka sharti moja tu la FIKI-UKO na ambalo limepangwa nyuma ya kabisa ya mashartizuizi mengine na linavumilika. Jambo hili linamfanya mshindi. Mshindani (b) amekiuka masharti matatu muhimu ambayo yanamfanya asishinde naye mshindani (c) amekiuka sharti moja.

Katika lugha zingine kama vile Kiingereza si lazima viangami viwe na irabu. Kwa mfano *is not*, neno la pili linapofupishwa na kuwa kiangami, irabu ndiyo

huondolewa na konsonanti mbili zinatumika kama kiangami, kama vile i*sn't.* Mifano mingine katika lugha ya Kiingereza ni kama vile:

| **59** | **Neno Kuu** | **Kiangami** | **Neno Lenye Kiangami** |
|---|---|---|---|
| | *(a) She* | *s (is)* | *she's* |
| | Yeye | ni | |
| | *(b) They* | *re* | *they're* |
| | Wao | ni | |
| | *(c) I* | *ve* | *I've* |
| | Mimi | nime.. | |
| | *(d) We* | *ve* | *we've* |
| | Sisi | tume… | |

Katika lugha ya Kiswahili, kiangami huwa na irabu moja pekee. Hii ina maana kuwa hakuna uwezekano wa irabu mbili au zaidi kufuatana katika kiangami cha Kiswahili. Pia hakuna uwezekano wa kuwa na kiangami cha konsonanti pekee bila irabu.

Kiswahili ni lugha ya kibantu. Katika lugha za kibantu irabu ni muhimu sana. Hii ni kwa sababu muundo wa irabu wa silabi katika lugha ya Kiswahili ni wazi. Silabi wazi hudhihirika zaidi katika lugha ya Kiswahili na lugha nyinginezo kadha za kiafrika.

Kulingana na sharti hili la pili, kiangami cha lugha ya Kiswahili ni kipashio kilicho wazi kimatamshi. Hii ina maana kuwa viangami vya Kiswahili vinapoundwa vinachukua muundo wazi na wala si funge. Hebu sasa tuangalie

sharti la tatu katika uundaji wa viangami vya Kiswahili. Sharti hili linahusiana na maana ya kiangami.

### 3.4.3 Maana Halisi ya Neno Hubaki

Katika lugha ya Kiswahili, neno linapofupishwa na kuwa kiangami, maana asili ya neno lile hubakia. Maana iliyokusudia hapo awali haibadiliki bali hubakia kama hapo awali. Hii ina maana kuwa kiangami ni kipashio cha lugha kilicho na maana ya kisarufi. Kiangami kinapoambishwa kwa neno kuu, hulipa neno kuu maana ya ziada. Maana ya kiangami hutokana na maana ya neno lililofupishwa. Angalia, Jedwali 3.4

**Jedwali 3.4 Maana ya Viangami**

| **Umboghafi** | **Kiangami** | **Maana** | **Neno lenye kiangami** |
|---|---|---|---|
| a. Mama yake | -ke- (yake) | Umiliki wa nafsi ya kwanza | Mamake |
| b. Mama yako | -ko- (yako) | Umiliki nafsi ya pili | Mamako |
| c. Utakula nini? | -ni- (nini) | Kiulizi | Utakulani |
| d. Bibi mkubwa | -bi- (bibi) | Mama wa baba/mama | Bimkubwa |

Jedwali 3.4 linaonyesha mifano ya viangami na maana yake. Viangami katika lugha ya Kiswahili huwakilisha maana mbalimbali. Katika Jedwali 3.4, (1). kiangami -*ke*- kinatokana na neno kamili *yake*. Hiki ni kivumishi kinacholeta dhana ya kumiliki katika nafsi ya kwanza. Hivyo basi unapotumia -*ke*- kama kiangami au *yake* kama neno kamili maana haibadiliki. Mfano katika sentensi.

60. Mama *yake* amewasili.

Mama*ke* amewasili.

Kulingana na sentensi hizi mbili, maana inayowakilishwa ni sawa. Kufupishwa kwa neno na kuwa kiangami hakupaswi kubadilisha dhana iliyokusudiwa hapo awali. Kiangami cha tatu (3.4, c) ni aina ya kiulizi. Nacho kiangami cha nne ni aina ya nomino.

### 3.4.4 Lazima Maneno Yanayoathirika Yafuatane

Kulingana na utaratibu huu wa kuunda kiangami ni sharti neno linalofupishwa na kuwa kiangami lifuatane na neno kuu linaloambishwa kiangami kile. Tazama mfano,

61 (a) *Shangazi yake* amesafiri.

*Shangaziye* amesafiri.

(b) *Bwana mkubwa* yu barazani.

*Bwamkubwa* yu barazani.

Kulingana na Mfano 61, neno kuu na kiangami hufuatana moja kwa moja katika sentensi. Kulingana na mfano huu, viangami awali na pia viangami tamati hufuata utaratibu huo.

| 62. | Neno Kuu | Kiangami | Neno Lililoambishwa |
|---|---|---|---|
| | Shangazi | -ke- (yake) | shangaziye |
| | Mkubwa | -bwa- (bwana) | bwamkubwa |

Neno kuu huweza kutangulia neno linalofupishwa kama ilivyo katika neno *shangaziye.* Neno kuu pia hujitokeza kabla ya neno linalofupishwa kama ilivyo katika neno *bwamkubwa.* Ifuatayo ni mifano ya ziada:

**Jedwali 3.5 Kufuatana kwa Kiangami na Neno Kuu**

| Neno lililoambishwa | Neno kuu | Kiangami | Sentensi |
|---|---|---|---|
| (a) Bintiye | Binti | -ye- | Binti yake alifika juzi. |
| (b) Bamkubwa | Mkubwa | -ba- | Baba mkubwa atatutembelea. |
| (c) Utakulani? | Utakula | -ni- | Kesho utakula nini? |

Kulingana na Jedwali 3.5, lazima neno kuu lifuatane na neno linaloambishwa iwe ni kwa upande wa kulia au kwa upande wa kushoto. Katika mfano wa kwanza (a), neno kuu linatangulia kisha kufuatwa na neno linalofupishwa. Hii ni sawa na mfano (c). Katika mfano wa pili (b), neno linaloambishwa linafuata neno linalofupishwa. Ni vigumu kupata maneno yaliyotenganishwa yakiunganishwa na moja kuwa kiangami. Kwa mfano,

63. *Binti yake* amesafiri. *Bintiye* amesafiri.

*Binti* aliyesafiri ni *wake.* ø

Katika sentensi ya kwanza, nomino ‘binti’ inaambatishwa kiangami -ye, kinachotokana na kivumishi kinachofuatana na nomino husika. Sentensi ya pili haina uwezo huo. Hata kama kivumishi *wake* kinaeleza nomino *binti*, maneno

haya hawezi kuambatishwa na neno moja kuwa kiangami bila kubadilisha muundo wa maneno katika sentensi yenyewe.

Kulingana na sheria hii, ni wazi kuwa uambishaji wa viangami kwa neno kuu haufanywi kiholela. Ni sharti kwanza maneno yanayoathiriana yafuatane moja kwa moja katika sentensi. Sehemu inayofuata inaonyesha kuwa, kando na maneno yale kufuatana, ni sharti yahusiane pia.

### 3.4.5 Kiangami Kihusiane na Neno Kuu Kisarufi

Kulingana na utafiti huu, maneno mawili hayaunganishwi kiholela. Kufuatana kwa maneno husika katika sentensi hakutoshi kuunganisha maneno yale. Ni sharti maneno yale mawili yanayoathiriana yawe na uhusiano wa kisintaksia. Kwanza, neno kuu na kiangami huashiria jambo sawa katika sentensi. Neno kuu na kiangami huwa ni aina ya kirai. Kwa mfano:

| | | |
|---|---|---|
| 64. | *Kaka yake* amefika. | *Kakake* amefika. |
| | Kirai nomino | |
| | Mama *atakula nini*? | Mama *atakulani?* |
| | Kirai kitenzi | |
| | Chakula *cha jioni* ni hiki | *Chajio* ni hiki. |
| | Kirai kihusishi | |

Kulingana na mifano 64, kiangami na neno kuu huhusiana kisarufi. Kwa mfano ikiwa neno la kwanza ni nomino, neno la pili huwa ni kivumishi ambacho kazi yake katika sentensi ni kuifafanua nomino iliyotangulia. Na ikiwa neno la kwanza

ni kitenzi basi neno la pili litakuwa ni kielezi kinachoeleza kitenzi kile. Hii inaonyesha kuwa kiangami na neno kuu ni aina ya kirai.

Kwa mujibu wa Chisia (2019), uainishaji wa virai hutegemea neno kuu. Kila kirai huwa na neno kuu. Neno la kwanza katika kirai ndilo neno kuu na husaidia kujua ni kirai cha aina gani. Ikiwa neno kuu ni nomino, kirai husika huainishwa kama kirai nomino na vile vile ikiwa neno kuu ni kivumishi basi kirai husika ni kirai kivumishi.

Miundo ya virai hukitwa katika aina za maneno ambazo ndizo chimbuko la mahusiano maalumu ya ndani ya vipashio hivyo. Kiangami na neno kuu huwa ni kirai. Vifuatayo ni baadhi ya viangami.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 65. | **Kirai Nomino** | **Neno Kuu** | **Kiangami** | **Neno Lililoambishwa** |
| | **(a)** Kaka yake | Kaka | -ke- | kakake |
| | (b) Shangazi yake | shangazi | -ye- | shangaziye |
| | (c) Mwana wangu | mwana | -ngu- | mwanangu |
| | **Kirai Kitenzi** | | | |
| | **(d)** Utakula nini? | Utakula | -ni- | utakulani |
| | (e) Unaenda wapi? | Unaenda | -pi- | unaendapi |
| | **Kirai Kihusishi** | | | |
| | **(f)** Cha jioni | cha | -jio- | chajio |
| | (g) Cha mchana | cha | -mcha- | chamcha |

Kulingana na mifano 65, neno kuu na kiangami ni aina ya kirai. Haya ni maneno ambayo yanawakilisha maana sawa katika sentensi. Jedwali 3.6, limetumika kuonyesha mashartizuizi ya kirai *mama yake.*

**Jedwali 3.6 Ukiukaji wa Mashartizuzi katika *‘mama yake’***

| /Mama + yake/<br>(umboghafi) | ***II** | **H-KODA** | **SHABI-JI** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|---|
| ☞ (a) ma.ma.ke | | | | * |
| (b) ma.ma.e | *! | | | * |
| (c) ma.ma.k | | *! | * | * |

Kulingana na Jedwali 3.6, mshindani (a) ndiye mshindi. Mshindani huyu amezingatia masharti yaliyopo. Hata kama amevunja sharti la FIKI-UKO mara mbili, yeye bado ni mshindi kwani amehifadhi masharti ya uadilifu. Mshindani (b) amevunja sharti muhimu la *II kwani irabu mbili zinafuatana pia. Mshindani (c) naye amevunja sharti la H-KODA kwani neno hili linaishia na *k* ambayo ni konsonanti halisi. Pia amevunja SHABI-JI, sharti ambalo ni muhimu.

Kando na kuvunja masharti muhimu, washindani b. na c. Wanakosa kuonyesha uhusiano wa kisarufi kati ya kiangami na neno kuu. Maana halisi inayokusudiwa haijitokezi kwa uwazi katika maneno *mamae* na *mamak.* Kwa mfano katika neno la kwanza, *mama**ke*** kiangami –*ke*- kinaonyesha dhana ya umiliki kama ilivyo katika *shogake*, *dadake* na *kakake*. Lakini katika maneno *mamae* na *mamak*, kiangami –e- na –k- hakionyeshi dhana ya umiliki.

### 3.4.6 Neno Moja Kupachikwa Kiangami Kimoja

Kwa mujibu wa utafiti huu, neno kuu hupachikwa kiangami kimoja tu katika lugha ya Kiswahili. Neno kuu linalopachikwa kiangami ni sharti liwe neno kamili kisarufi. Kwa mfano,

66. Bibi mdogo anacheza. Bimdogo anacheza.
    Binti yake anacheza. Bintiye anacheza.
    Binti yake mdogo anacheza. *Bimdogoye anacheza.

Kulingana na mifano 66, kiangami kinaambishwa kwa neno moja kamili. Katika lugha ya Kiswahili, neno hutengwa ili lijisimamie. Neno moja kamili haliwezi kuchanganuliwa kwa undani na kuwa na maneno mengine. Hii ina maana kuwa neno linaloambishwa kiangami huwa ni neno moja tu hata likichanganuliwa. Baada ya neno kuambishwa kiangami, tunapata neno moja lililo na maana ya ziada. Jedwali 3.6 linaonyesha mashartizuizi ya viangami.

**Jedwali 3.6: Ukiukaji wa Mashartizuizi katika Kirai *bibi yake mdogo***

| /binti yake mdogo/ | **SHABI-JI** | **TEGE** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|
| (a) ☞bimdogo | * | | * |
| (b) bintie | *! | * | * |
| (c) bimdotoye | * | *! | * |

Jedwali 3.6 limetumika kuonyesha uundaji wa kiangami –*bi*- ambacho ni kiangami cha awali. Kiangami hiki kimetokana na neno *bibi*. Katika kirai *bibi yake mdogo* neno *bibi* ambalo ni neno kuu linaambishwa kiangami –ye- na kuwa *bibiye.* Pia

neno bibi linaweza kufupishwa na kisha kuambishwa kama kiangami kwa neno kuu *mdogo*. Na kuwa *bimdogo*. Hata hivyo, ni vigumu kwa maneno yote matatu kuunganishwa pamoja na kuwa neno moja. Ni lazima neno moja pekee lifupishwe na liwe kiangami na lingine moja pekee liwe neno kuu. Hivyo basi, kivumishi *yake* kikifupishwa inakuwa vigumu kufupisha kivumishi *mdogo* na kisha kukiambisha kwenye neno *bibiye*.

Kama ilivyo katika viangami awali, pia katika viangami tamati neno kuu huambishwa kiangami kimoja pekee. Hebu sasa tuangalie mfano wa kiangami tamati. Tazama Jedwali 3.7.

**Jedwali 3.7: Ukiukaji wa Mashartizuizi katika Kirai *bibi yake mdogo***

| /binti yake mdogo/ | **H-KODA** | **TEGE** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|
| (a) ☞bibiye | | | * |
| (b) bintim | * | * | * |
| (c) bibiyemd | *! | | ** |

Kulingana na Jedwali 3.6 na 3.7 washindani 3.6 (a) na 3.7 (a) wameibuka washindi kwani wanakubaliana na masharti yaliyowekwa. Mshindani 3.6 (c) anakiuka masharti muhimu kama vile SHABI-JI. Sharti hili linazuia mabadiliko ya matamshi kati ya umboghafi na umbotokeo. Mshindani huyu pia amevunja sharti la TEGE. Kulingana na sharti hili, umbotokeo linalofikia kiwango cha ukubalifu ni lile ambalo kila sehemu inategemea kilichomo katika umboghafi. Mshindani 3.7 (b) amevunja sharti H-KODA kwani neno hili limeishia na konsonanti *m*.

Kulingana na mashartizuizi haya, neno kuu huweza kupachikwa kiangami kimoja pekee

Katika Jedwali 3.7, kirai *bibi yake mdogo* neno *bibi* linapotumika kama neno kuu, kivumishi *yake* ndilo neno tu lililo na uwezo wa kufupishwa na kuambishwa kama kiangami kwenye neno kuu. Basi kivumishi *yake* kinapofupishwa, inakuwa vigumu tena kufupisha

### 3.4.7 Kiangami Huambishwa kwa Neno Kamili

Kulingana na utafiti huu, ni lazima kiangami kimoja kiambishwe kwa neno moja lililokamilika, yaani ni sharti neno kuu likamilike kimuundo na kimaana pia ili liweze kuambishwa kiangami. Kiangami kinapoambishwa kwa neno moja kamili, kinaambishwa moja kwa moja. Alama za uakifishaji hazitumiki kutenganisha kiangami na neno kuu. Kwa mfano,

| 67. | **Neno kuu** | **Kiangami** | **Neno Lililoambishwa Kiangami** |
|---|---|---|---|
| | **(a)** Sifa | -ze- | sifa*ze* |
| | **(b)** Na | -si- | na*si* |
| | **(c)** Rafiki | -ye- | rafiki*ye* |
| | **(d)** Wana | -o- | wana*o* |
| | **(e)** Utakula | -ni- | utakula*ni*? |

Kulingana na Mifano 67, maneno yote yaliyoambishwa kiangami ni maneno kamili kisarufi na pia kimuundo. Mfano 67 (a), (c) na (d) ni nomino, mfano (b) ni kihusishi nao mfano (e) ni kitenzi. Hata hivyo katika vitenzi ni vigumu kwa kiangami kuambishwa kwenye kitenzi kilichonyambuliwa. Kiangami

kinapoambishwa kwa neno lililokamilika, neno lile linapata maana ya ziada. Kulingana na mifano hii, viangami vinaambishwa kwa maneno kamili moja kwa moja bila kutumia alama za uakifishaji kama tutakavyoona katika sehemu ifuatayo.

### 3.4.8 Viangami Huambishwa Moja kwa Moja

Katika lugha ya Kiswahili, viangami huambishwa kwa neno kuu moja kwa moja bila kutumia alama za uakifishaji. Hii ni tofauti na lugha zingine ambazo hutumia alama za uakifishaji kutenganisha viangami na neno kuu. Ifuatayo ni baadhi ya mifano inayoonyesha kuwa viangami vinaambishwa kwa neno kuu moja kwa moja. Tazama Mfano 68.

| 68. | **Neno Kuu** | **Kiangami** | **Neno Lililoambishwa** |
|---|---|---|---|
| | **(a)** Binti | -ye- | binti*ye* |
| | (b) Shangazi | -ye- | shangazi*ye* |

Kulingana na Mfano 68 (a) neno ‘binti’ limeunganishwa na kiangami –ye- moja kwa moja bila kutumia alama yoyote ile ya uakifishaji. Hii ni kinyume na lugha zingine kama vile lugha ya Kiingereza. Katika lugha ya Kiingereza, si lazima kiangami kiambishwe kwenye neno kuu moja kwa moja. Mara nyingi ritifaa hutumika kutenganisha kiangami na neno kuu. Tazama Mfano 69.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 69. | (a) It | + | is | = | it’s |
| | *Hicho* | *ni* | | | |
| | (b) She | + | is | = | she’s |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| *Yeye* | *ni* | | | |
| (c) They | + | are | = | they're |
| *wao* | | *ni* | | |
| (d) We | + | are | = | we're |
| Sisi | | ni | | |

Kulingana na mfano 69 (a), katika lugha ya Kiingereza ritifaa inatenganisha neno kuu *it* na kiangami *s*. Hivyo basi katika lugha ya Kiingereza ritifaa hutumika kuonyesha kuwepo kwa ritifaa katika neno.

Kiangami kinapoambishwa kwa neno kuu, kunakuwa na kipashio kimoja kikubwa chenye maana. Hivyo basi kiangami na neno kuu huunda neno moja.

### 3.4.9 Hakuna Viangami vya Konsonanti Moja

Katika lugha ya Kiswahili, kulingana na data iliyokusanywa, hakuna uwezekano wa kuwa na kiangami cha konsonanti moja pekee au hata mbili zikiwa peke yaani bila irabu. Viangami vya lugha ya Kiswahili huweza kujisimamia kimatamshi. Hii ina maana ya kuwa viangami vinatamkika kivyake bila kutegemea sauti zingine katika neno kuu. Katika viangami vya lugha ya Kiswahili, irabu ni kiungo muhimu.

Kutokana na utafiti huu ni wazi kuwa kuna tofauti katika viangami vya lugha ya Kiswahili na vile vya lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kiingereza huweza kuwa na viangami vya konsonanti moja au hata mbili bila ya kuwa na irabu. Tazama mfano,

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 70. | (a) She | + | is | =She's |
| | *Yeye* | + | *ni* | *(yeye ni)* |
| | (b) Are | + | not | = aren't |
| | Wao | + | ni | |
| | (c) It | + | is | = it's |
| | Hicho | + | ni | |
| | (d) I | + | will | = I'l |
| | Mimi | + | nita… | |
| | (a) we | + | will | = we'l |
| | Sisi | + | tuta.. | |

Kulingana na data iliyopatikana katika utafiti huu, lazima viangami vya lugha ya Kiswahili viwe na irabu moja. Hakuna viangami vya lugha ya Kiswahili vinavyoundwa na konsonanti pekee bila ya kuambatana na irabu. Hii kinyume na lugha kama vile ya Kiingereza. Katika lugha ya Kiingereza, unapoandika kiangami si lazima kuwe na irabu. Tazama jedwali lifuatalo.

**Jedwali 3.7: Ukiukwaji wa Mashartizuizi katika Uundaji wa Viangami ‘shangaziye’**

| /shangazi+yake/ Umboghafi | H-KODA | *KKK | SHABI | KILELE | FIKI-UKO |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) ☞sha.nga.zi.ye | | | | | * |
| (b) Sha.nga.zi.k | * | | * | * | * |
| (c) Sha.nga.zi.y | *! | | * | * | * |
| (d) Sha.nga.zyk | * | *! | | * | |

Kulingana na Jedwali 3.7, neno kuu *shangazi*, linapoambishwa kiangami *ye* linafuata kanuni kadha hadi linafikia upeo wa kukubalika. Mshindani (a) ndiye mshindi kwani amekubali masharti yote yaliyotumika. Washindani (b), (c), na (d) hawajashinda. Hii ni kwa sababu, viangami katika maneno haya vinaishia na koda. Washindani b, c, na d wamevunja masharti yasiyovumilika ambayo ni H-KODA NA KILELE. Jedwali 3.1 linadhihirisha kuwa viangami vya Kiswahili haviundwi kiholela bali kuna kanuni zinazozingatiwa. Utafiti huu unaonyesha kuwa viangami vya Kiswahili havina uwezo wa kuundwa kwa konsonanti pekee. Kulingana na utafiti, ni lazima viangami vya lugha ya Kiswahili viwe na irabu.

### 3.5 Hitimisho

Sura hii ilishughulikia utaratibu wa uundaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na utafiti huu, viangami vya lugha ya Kiswahili huundwa kwa kuongozwa na sheria za lugha ya Kiswahili. Baadhi ya mashartizuizi

yanayofuatwa ni kama vile, viangami vya Kiswahili ni aina ya silabi; Lazima silabi hii iwe na kilele; na silabi hiyo pia havina koda. Hii ina maana kuwa viangami katika lugha ya Kiswahili huwa na kiima lakina havina koda.

Sharti lingine linalofuatwa ni kuwa, viangami vya Kiswahili huundwa tu na irabu moja. Hakuna uwezekano wa irabu mbili kufuatana. Katika utafiti huu, ni wazi kuwa viangami vya Kiswahili vinaweza kuwa na konsonanti mbili lakini hakuna muundo wa konsonanti tatu halisi zikifuatana. Utafiti huu ulidhihirisha kuwa viangami huongozwa na sheria kadha. Haya yote ni kutokana na matumizi ya nadharia ya umbo upeo.

Uambishaji wa viangami unapozingatia kanuni hizi zote, basi maumbotokeo yanayopatikana huweza kukubalika na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili na pia wanaisimu. Kuna baadhi ya maneno yaliyoambishwa viangami na yakakubalika hata katika Kamusi Sanifu ya Kiswahili. Baadhi ya maneno yaliyokubalika ni kama vile, hamnazo, hatimaye, chajio, chamcha, bimkubwa na mamantilie. Sura inayofuata inatathmini mwingiliano uliopo baina ya sifa za kiarudhi na viangami vya lugha ya Kiswahili. Sura hii pia itaongozwa na mashartizuizi ya nadharia ya umbo upeo.

# SURA YA NNE

# MWINGILIANO BAINA YA SIFA ZA KIARUDHI NA VIANGAMI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti alitathmini mwingiliano uliopo baina ya sifa za kiarudhi na viangami vya Kiswahili. Viangami vya Kiswahili vimeingiliana na baadhi ya sifa za kiarudhi. Sifa za kiarudhi zilizoshughulikiwa katika sura hii ni shadda na kiimbo. Mtafiti alitumia mifano ya viangami vilivyopatikana baada ya utafiti kuonyesha namna vinavyoingiliana na sifa za kiarudhi. Katika sehemu hii, mtafiti alianza kwa kueleza maana ya sifa arudhi. Kila sifa ya arudhi imeshughulikiwa kivyake. Mtafiti aliongozwa na nadharia ya umbo upeo. Mashartizuizi ya uadilifu na uziada yalitumika kuonyesha namna umbo upeo ulivyofikiwa.

## 4.2 Fasili ya Sifa za Kiarudhi

Neno ‘arudhi’ lina maana ya usuli na matumizi ya lugha kwa ujumla. Kwa mujibu wa Mwihaki (2006), arudhi ni neno linalotumika kurejelea muundo, maumbo na mahusiano mwafaka ya vipashio vya sauti vilivyozidi foni. Sifa za kiarudhi ni sifa za kifonolojia ambazo zinahusu mabadiliko ya mkazo, kiimbo na toni katika vipashio mbalimbali.

Sifa za kiarudhi ni mabadiliko katika sifa mbalimbali za utamkaji ambazo hutokea kwenye vipashio vikubwa zaidi kuliko fonimu. Kulingana na maelezo yaliyotolewa na Chomsky na Halle (1968), sifa za kiarudhi huwekwa kwenye vipashio ambavyo ni vikubwa zaidi kuliko foni. Vipashio vya lugha vinavyowekwa sifa za kiarudhi ni pamoja na silabi, neno, kirai na sentensi.

Vipashio hivi vimeshughulikiwa katika sehemu hii. Viangami katika lugha ya Kiswahili huweza kuchukua dhima ya vipashio vyote vinne.

Kwa mujibu wa utafiti huu, sifa za kiarudhi zinawekwa katika viangami. Hii ni kwa sababu kadha. Kwanza, kiangami katika lugha ya Kiswahili kinachukua muundo wa silabi. Kulingana na Fromkin na waandishi wenza (2003), sifa za kiarudhi hudhihirika katika silabi. Kwa mfano, katika neno ***nyanyake, (#nya$nya$ke#)*** -ke- ni kiangami ambacho kinachukua muundo wa silabi iliyoundwa kwa konsonanti moja na irabu moja. Hii ni aina ya silabi wazi.

Sababu ya pili ni kuwa kiangami kinaambishwa kwa neno kuu ambalo ni neno kamili. Kwa mfano, *mjomba**ye*** ni neno kamili**.** Kiangami –ye- kimeambishwa kwa neno kuu ‘mjomba’. Hii ina maana kuwa, kiangami kinapatikana ndani ya neno kamili na hivyo basi, sifa za kiarudhi zinazopatikana kwa maneno kamili huathiriwa na uwepo wa kiangami.

Tatu ni kuwa, neno lililoambishwa kiangami ni aina ya kirai. Kwa mfano, *kaka yake.* Huu ni mfano wa kirai nomino ambacho kimeundwa kwa nomino *kaka* na kivumishi *yake*. Tunafupisha kivumishi *yake*, na kukitumia kama kiangami na kisha kukiambisha kwa nomino *kaka* ambalo linatumika kama neno kuu. Baada ya kiangami kuegemezwa kwa neno kuu, umbotokeo ambalo linapatikana ni *kakaye* au *kakake.* Maneno yote mawili yatakuwa bado ni virai nomino.

Katika utafiti huu, kipashio kikubwa zaidi kilichoshughulikiwa ni sentensi. Viangami vya Kiswahili vina uwezo wa kuambishwa kwa neno kuu na kuunda

sentensi iliyokamilika kisarufi na kimuundo. Kwa mfano, *watakani?* ni sentensi aina ya swali. Kiangami –ni- kinachotokana na kiulizi *nini*, kimeambishwa kwa neno kuu *wataka.* Kwa sababu hii, sifa za kiarudhi zinazohusiana na kipashio cha sentensi zinapatikana katika maneno yaliyoambishwa viangami.

Sifa arudhi huzingatia ruwaza na uamilifu mwafaka. Sifa hizi za kiarudhi hutumika kutofautisha maumbo linganifu kimuundo. Sifa za arudhi hurejelea umbo la silabi. Katika utafiti huu mtafiti alishughulikia sifa za kiarudhi kwa kuongozwa na nadharia ya umbo upeo. Sifa za kiarudhi zilizoshughulikiwa ni mkazo (shadda) na kiimbo.

### 4.2.1 Shadda katika Viangami

Katika lugha za kiafrika, mfumo wa arudhi huelezewa kwa kutumia mkazo au toni. Mkazo hutokea katika lugha chache za kibantu. Baadhi ya lugha za kibantu zinazodhihirisha uwepo wa shadda ni lugha ya Xhosa, lugha ya Tswana na lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha mkazo ambayo huwa na mkazo sahili.

Katika sehemu hii, mtafiti aliangazia jinsi shadda inavyojitokeza katika viangami vya lugha ya Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa unatathmini jinsi shadda katika neno, kirai au sentensi ilivyoathiriwa na kuwepo kwa kiangami katika kipashio husika. Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999), shadda ni kiwango cha nguvu inayotumiwa wakati wa utamkaji wa silabi. Kwa upande wake Mgullu (2001), shadda ni jinsi maneno yanavyotamkwa kwa nguvu zaidi katika sehemu fulani.

Hivyo basi shadda pia ni mkazo linganifu wa silabi sanjari. Shadda ni mkazo mzito unaosikika tunapotamka silabi fulani katika neno.

Kulingana na Mgullu (2001), kuna aina mbili za shadda. Kuna shadda inayopatikana katika neno na shadda katika sentensi. Shadda katika sentensi huwekwa kutegemea aina ya sentensi. Mkazo hutofautiana katika sentensi ya kutolea taarifa, sentensi ya kuulizia swali na hata sentensi ya kuonyesha mshangao.

Shadda katika neno hutegemea lugha. Kila lugha huwa na utaratibu wake wa kuweka shadda. Katika lugha ya Kiswahili, sheria ya shadda ni kuwa, shadda huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho wa neno.

$\sigma \rightarrow$ [+shadda]/_ $\sigma$#

shadda huwekwa silabi ya pili kutoka mwisho.

Kulingana na sheria hii, silabi ya pili kutoka mwisho ndiyo huwekwa mkazo. Kwa mfano, katika neno lililoambishwa kiangami ‘binamuye’, shadda itakuwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho ambayo ni –*mu*-.

/$bi$na$mú$ye$

Kwa vile lugha ya Kiswahili huwa na mkazo sahili, sheria hii hutumika kila mara. Hata hivyo, kunayo maneno machache yanoyokiuka sheria hii. Haya ni maneno yaliyokopwa kutoka lugha zingine kama vile lugha ya Kiarabu.

Kwa mujibu wa Halpern (2001), viangami ni viungo ambavyo havina mkazo wake peke yake na hivyo basi, ni sharti kiangami kitegemee neno kuu. Kwa upande wake Said (2011), kiangami ni mofimu funge ambayo haina mkazo. Kiangami huambishwa kwa neno kuu na hivyo kuunda kirai au hata sentensi.

Katika utafiti huu, tulishughulikia maneno, virai na pia sentensi zilizo na viangami. Kwa kuzingatia Mfano wa 71, ni wazi kuwa shadda katika lugha ya Kiswahili huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho. Mfano 71 unaonyesha mwingiliano wa shadda katika viangami.

| **71.** | **Neno Kuu** | **Kiangami** | **Neno lenye Kiangami** | **Kipashio** |
|---|---|---|---|---|
| | (a) Má-ma | -ke- (yake) | ma-má-**ke** | kirai |
| | (b) Wá-la | -ni- (nini) | wa-lá-**ni**? | Sentensi |
| | (c) M-kú-bwa | -bi- (bibi) | **bi**-m-kú-bwa | kirai |


Mfano 71 umeshughulikia viangami vya aina tofauti. Mifano (a), (b) na (c) ni aina ya viangami tamati nao mfano (d) ni kiangami awali. Kwa mujibu wa mfano 71, silabi asilia inayowekwa shadda katika neno kuu inabadilika baada ya kuweka shadda. Neno kuu linapoambishwa kiangami, kunayo mabadiliko ambayo hufanyikia mkazo katika neno kuu. Mabadiliko hayo hupelekea kubadilishwa kwa nafasi ya kwanza ya mkazo. Kulingana na mfano 71 (a), tunapata neno *mama*. Katika neno *mama*, mkazo unawekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho (‘ma-ma). Mkazo huhamishwa kutoka silabi awali na kupelekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho katika neno lililoambishwa. Tunapoambisha kiangami –*ke*- kwa

neno mama, tunapata *mamake*. Neno lililoambishwa sasa lina silabi tatu (*ma-ma-ke*). Mkazo unabadilika na kuwekwa katika –ma- ya pili *(Ma'make).*

Viangami huambishwa kwa neno kamili baada ya mkazo wa kwanza kuwekwa kwenye neno hilo kuu. Mzunguko wa pili wa kifonolojia hutokea baada ya kiangami kuambishwa kwenye neno kuu. Hivyo mkazo unahamishwa baada ya kuambishwa kwa kiangami.


Katika lugha ya Kiswahili kila neno la kimsamiati huwa na mkazo katika silabi fulani. Hivyo basi, ni vigumu katika lugha ya Kiswahili kupata neno lisilo na mkazo. Mkazo husaidia katika utamkaji wa neno. Kila neno la kiarudhi huwa na futi kuu inayotiliwa mkazo mzito. Kila futi huwa na silabi inayotiliwa mkazo. Silabi zenye uzito na zile hafifu hufuatana katika maneno. Mkazo huwakilishwa kwa kutumia gridi au matawi. Katika utafiti huu, shadda imewakilishwa kwa njia ya matawi. Kwa kutumia mfano wa *mama* na *mamake* tulionyesha mabadiliko ya shadda kabla ya kiangami kuambishwa kwa neno 'mama' na baada ya kuambisha kiangami kwa neno kuu.

72.




Kinachodhihirika katika Mfano 72. ni kuwa, shadda nzito katika neno ‘mama’ inawekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho, yaani ‘ma’ ya kwanza. Hebu tuangalie mabadiliko ya shadda baada ya kuambisha kiangami –ke- kinachotokana na kivumishi *yake*. Kiangami –ke ni aina ya kiangami tamati, hivyo basi kiangami hiki kinaambishwa mwishoni mwa neno. Hii ina maana kuwa silabi ya awali iliyowekwa mkazo itakuwa silabi ya tatu kutoka mwisho. Ikiwa neno hili litatamkwa kwa kuweka shadda katika silabi ya tatu kutoka mwisho, hayo yatakuwa makosa ya kimatamshi katika lugha ya Kiswahili kwani mkazo unafaa kuwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho. Hii ina maana ya kuwa silabi ya awali iliyowekwa shadda itabadilika baada ya kuambisha kiangami tamati. Tazama Mfano 73.

73.




Mfano 73 unaonyesha kiangami tamati kinachoambishwa kwa neno kuu. Baada ya kuambisha kiangami –ke- kwa neno *mama*. Tunapata neno *mamake*. ‘ma’ ya pili ya neno *mama* ndiyo inyowekwa mkazo kinyume na hapo awali. Hapo awali, kabla ya kuambisha kingami, silabi ya kwanza ya neno *mama* ndiyo iliyowekwa mkazo. Hii ina maana kuwa kiangami tamati kinapoambishwa kwa neno kuu, silabi asilia ya neno kuu iliyokazwa inabadilika kwani tunapata silabi ya ziada mwishoni mwa neno.

Uwekaji wa shadda unatokea mara ya kwanza katika neno ‘mama’ ambapo silabi ya kwanza ndiyo inayobeba shadda. Baadaye kiangami kinaongezwa kwa hiyo tunakuwa na ‘mamake’. Bado shadda ipo kwenye ‘ma’ ya kwanza. Kwa sababu ya mabadiliko haya, mzunguko wa pili wa sheria za kifonolojia unatokea. Shadda inawekwa tena au inahamishwa hadi silabi ya pili kutoka mwisho. Sasa shadda inawekwa kwenye ‘ma’ ya pili. Tazama Jedwali 4.1,

**Jedwali 4.1 Mabadiliko ya Shadda katika /mama+yake/**

| /máma + yáke/ | **Mabadiliko ya Shadda** |
|---|---|
| Shadda 1 | Máma + yáke |
| Mwambatano | Mámake |
| Shadda 2 | Mamáke |

Jedwali 4.1 limetumika kuonyesha mabadili ya shadda. Kiangami kinapoambishwa kwa neno *mama*, kunakuwa na mabadiliko ya shadda. Jedwali 4.2 limetumika kuonyesha ukiukaji wa mashartizuizi katika neno mamake. Maneno yote mawili, *mama* na *yake* yana shadda katika silabi ya pili kutoka mwisho. Baada ya kuunda kiangami –ke- kiangami hiki hakiwezi kupokea shadda. Kulingana na kanuni, shadda huwa katika silabi ya pili kutoka mwisho

**Jedwali 4.2: Ukiukaji wa Mashartizuizi katika Neno /mamake/**


| /máma+ke/ | **Shadda-kulia** | **NSarufi-NArudhi** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|
| (a) má.ma.ke | *! | | * |
| (b) ma.ma.ke | | *! | * |
| (c) ☞ma.má.ke | | | * |

Kulingana na Jedwali 4.2, washindani wote wana silabi tatu ambazo zina muundo wa KV. Mshindani wa kwanza (a) amevunja sharti muhimu la Shadda-kulia.

Katika neno hili, shadda imewekwa upande wa kushoto. Kulingana na sharti hili, vipashio vilivyo upande wa kulia ndivyo huamua mahali mkazo wa neno huwekwa. Mshindani wa pili (b) hana mkazo katika silabi yoyote ile. Hivyo basi amevunja sharti la Nsarufi-Narudhi. Kulingana na sharti hili, ni lazima neno la kisarufi lidhihirishe uwepo wa sifa za kiarudhi. Mshindani (c) amekiuka sharti moja la FIKI-UKO. Kulingana na nadharia ya umbo-upeo, sharti la FIKI-UKO huwa nyuma katika safu ya masharti ya uadilifu. Kulingana na sharti hili, hakuna kitamkwa ambacho kinafaa kuondolewa katika umboghafi. Hata hivyo, ukiukaji huu unavumilika kwani lugha ya Kiswahili inakubali udondoshaji na uambishaji. Dhana ya viangami inahusu kufupisha neno moja ili kupata kiangami. Hivyo basi mshindani c) amefikia upeo wa kukubalika.


Baada ya kuangazia mabadiliko ya shadda katika viangami tamati, hebu sasa tuangalie athari ya viangami awali katika shadda. Katika Mfano 74, tunatumia neno *bimkubwa.* Katika mfano huu, kiangami -bi- ni mfano wa kiangami awali kwani kimeambishwa mwanzoni mwa neno kuu *mkubwa.* Katika kirai *bibi mkubwa*, shadda inawekwa kama ifuatayo,

74.




Katika Mfano 74, kila neno linawekwa shadda kivyake. Katika kila neno, shadda inawekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho. Hii ni kwa mujibu wa sheria katika lugha ya Kiswahili. Neno kuu hapa litakuwa ‘mkubwa’, litakaloambishwa kiangami awali *–bi-* kinachotokana na neno ‘*bibi’*. Mfano 75 unaonyesha jinsi shadda inawekwa katika neno *bimkubwa*.

75.





Kwa vile kiangami hapa kinaambishwa mwanzoni mwa neno, silabi inayokazwa haibadiliki. Katika mfano huu, silabi –ku- ndiyo inayokazwa kwani ni silabi ya pili

kutoka mwisho. Silabi hii ndiyo pia inayokazwa hata kabla ya kuambisha neno kuu. Hii inaonyesha kuwa kunapokuwa na viangami awali, shadda nzito katika neno haibadiliki ikiwa neno kuu limeundwa na silabi mbili au zaidi.

Pia tuliangalia mkazo katika neno la silabi moja. Neno linapoundwa kwa silabi moja, mkazo huwekwa kwenye silabi hiyo moja kama ilivyo katika neno kanushi ‘si’. Neno ‘si’ ni aina ya kitenzi. Linaambishwa kiangami -*ye*- kinachotokana na kiwakilishi cha nafsi *yeye*. Tunapata neno *siye*. Mkazo unabaki katika silabi asili *si* kwani sasa neno limepata silabi ya pili. Kwa kurejelea sheria za lugha ya Kiswahili, shadda huwekwa kwenye silabi ya pili kutoka mwisho.

76




Kutokana na utafiti huu, tunaona kuwa viangami awali haviathiri pakubwa shadda katika neno kuu. Hii ni kwa sababu viangami hivi vinapachikwa mwanzoni mwa neno kuu upande wa kushoto. Viangami tamati navyo vinaathiri mkazo katika neno kuu kwani vinaambishwa mwishoni mwa neno upande wa kulia. Hii inatokana na sheria ya mkazo/shadda katika lugha ya Kiswahili kwani kama

tulivyoona ni kuwa, katika lugha ya Kiswahili mkazo unawekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho yaani upande wa kulia.

Shadda ni muhimu sana katika matumizi ya lugha. Sifa kuu ya mkazo ni kuweka nguvu kwenye silabi wakati wa utamkaji. Jambo hili husaidia katika kutamka maneno inavyofaa kulingana na lugha husika. Katika lugha ya Kiswahili, shadda isipowekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho, kuna uwezekano wa kutoeleweka kwa neno au kutoa maana ambayo haikukusudiwa. Nadharia ya umbo upeo inatumika hapa kuonyesha umuhimu wa kutamka maneno kwa kuweka shadda panapofaa.

**Jedwali 4.3: Ukiukaji wa Mashartizuizi kuhusu /ndu-gú-ye/**

| **/ndugu+yake/** | **Shadda-Kulia** | **Nsarufi-Narudhi** | **SHABI-JI** | **TEGE** | **FIKI-UKO** |
|---|---|---|---|---|---|
| (a) ☞ndu.gú.ye | | | | | * |
| (b) 'ndu.guy | | | * | | * |
| (c) ndu.gu.ye.e | | * | * | * | *! |
| (d) 'ndu.gu.ye | * | | * | | * |

Katika Jedwali 4.3, mshindani (a) ndiye mshindi kwani amekiuka shartizuizi moja ambalo limepangwa nyuma katika safu ya mashartizuizi ya uadilifu. Mshindani (b) amekiuka masharti mawili. Moja wapo ya masharti muhimu yaliyokiukwa ni sharti la FIKI-UKO na lile la SHABI-JI. Sharti la FIKI-UKO linasisitiza kuwepo kwa kila kitamkwa cha umboghafi. Mshindani (c) amekiuka masharti manne. Sharti

moja alilokiuka ni la TEGE. TEGE husisitiza kwamba kila kitamkwa cha umbotokeo kitegemee sauti zilizomo katika umboghafi. Katika umboghafi, sauti *e* ni moja tu lakini mshindani (c) na *e* mbili. Pia mshindani (c) amekiuka shartizuizi la SHABI-JI kwani kuna mabadiliko ya jinsi ya kutamka kati ya umboghafi na umbotokeo. Mshindani (c) amekiuka sharti la Nsarufi-Narudhi kwani neno hili halina shadda. Kulingana na sharti la Nsarufi-Narudhi, neno la kisarufi huwa pia ni neno la kiarudhi. Mshindani (d) amevunja sharti la Shadda-Kulia kwani mkazo umewekwa mwanzoni mwa neno. Kulingana na sharti hili la Shadda-Kulia, mkazo huwekwa upande wa kulia. Katika lugha ya Kiswahili, kulingana na sharti hili, mkazo huwekwa mwishoni mwa neno. Jedwali 4.2 linaonyesha mwingiliano wa shadda katika kiangami tamati.

Jedwali lifuatalo linaonyesha mwingiliano wa shadda katika kiangami awali. Hapa tulitumia neno *bimdogo*. Neno hili ni muungano wa *bibi mdogo*. Neno ‘bibi’ linafupishwa na kupata kiangami –bi-. Kiangami –bi- kinaambishwa mwanzoni mwa neno ‘mdogo’. Hivyo basi hiki ni kiangami awali. Tazama Jedwali 4.3.

**Jedwali 4.4 Ukiukaji wa Masharti kuhusu /bi-m-dó-go/**

| **F F**<br>**nz h h nz h**<br>**bi bi m dó go** | **SILABI-FUTI** | **Shadda-Kulia** | **Nsarufi-NArudhi** |
|---|---|---|---|
| (a)☞ bi.m.dó.go | | | |
| (b) bi.m.do.go | * | * | *! |
| (c) bí.m.do.go | | * | |
| (d) bí.m.dó.gó | * | * | |

Kwa mijibu wa Jedwali 4.4, mshindani (a) ameibuka mshindi kwani amezingatia mashartizuizi yaliyowekwa. Mkazo umewekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho kama inavyofaa katika lugha ya Kiswahili. Kwa kukosa kuwa na shadda kwa silabi yoyote ile, mshindani (b) amekiuka masharti muhimu. Amekiuka sharti la Shadda-Kulia. Kulingana na sharti hili, kipashio kilicho upande wa kulia hutawala vipashio vingine. Kipashio hiki ndicho huamua mahali mkazo wa neno huwekwa. Pia amekiuka sharti la NSarufi-NArudhi. Kulingana na sharti hili, ni sharti neno la kisarufi liwe na sifa za kiarudhi. Kwa kukosa kuwa na shadda, neno hili linakosa sifa ya kiarudhi na hivyo kuvunja sharti muhimu. Mshindani (c) amekiuka sharti la uwekaji wa shadda katika upande wa kulia kwani badala yake, shadda imewekwa upande wa kushoto. Hatimaye mshindani (d) amekiuka masharti muhimu la Silabi-Futi. Kulingana na sharti hili, silabi hupambanuliwa kwa kuzingatia futi. Ni sharti kila silabi iwe na futi. Katika neno kuna wizani au mapigo. Huu ni mfuatano wa silabi nzito na silabi hafifu.

Lugha ya Kiswahili huwa na mwingiliano bayana. Katika mashartizuizi, uchopekaji wa sauti katika neno hupewa umuhimu wa kwanza kisha mkazo. Sheria za ruwaza ya mkazo katika lugha ya Kiswahili haziathiriwi na uambishaji wa vipashio. Lugha zilizo na uchopekaji na zinatiwa mkazo wakati mmoja, kama vile lugha ya Kiswahili, mashartizuizi ya uziada katika lugha hiyo yanazidi nguvu kwa cheo mashartizuizi ya uadilifu. Katika lugha ya Kiswahili, ni wazi kuwa mkazo huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho na pia lugha ya Kiswahili inakubali uambishaji wa vipashio ili kuzuia uwepo kwa koda.

Katika sehemu hii, tutatumia neno *walani*. Hili ni neno lililoambishwa kiangami. Neno kuu hapa ni *wala*. Neno hili ni aina ya kitenzi. Neno *wala* limeambishwa kiangami *ni* kinachotokana na kiulizi *nini*. Mashartizuizi yaliyotumika hapa ni, HKODA, PWDHD, Shadda-Kulia na pia Sarufi-NArudhi.

Tazama Jedwali 4.5,

**Jedwali 4.5 Ukiukaji wa Mashartizuizi kuhusu /wala+nini/**

| **/Wala+nini/** | HKODA | Silabi-Futi | Shadda-Kulia | NSarufi-NArudhi |
|---|---|---|---|---|
| ☞(a) wa.lá.ni | | | | |
| (b) wa.la.ni | | * | * | * |
| (c) wá.la.n | * | * | * | |

Kulingana na Jedwali 4.5, mshindani a) anaibuka mshindi kwani anazingatia mashartizuizi yaliyopo. Mshindani b) anakiuka masharti muhimu. Mshindani huyu anakiuka sharti la Silabi-Futi kwani neno hili linakosa futi. Neno hili halina mkazo katika silabi yoyote ile. Hivyo linakosa sifa za kiarudhi na kuvunja sharti la NSarufi-NArudhi. Mshindani c) pia amekiuka masharti muhimu. Kwanza anavunja sharti muhimu la HKODA kwani neno hili linaishia kwa konsonanti badala ya irabu. Hata kama mshindani c) ana mkazo, mkazo umewekwa upande wa kushoto badala ya upande wa kulia.

Katika sehemu inayofuata, mtafiti aliangazia mwingiliano wa viangami na kiimbo katika lugha ya Kiswahili. Nadharia ya umboupeo ilitumika.

### 4.2.2 Kiimbo katika Viangami

Kwa mujibu wa Mgullu (2001), kiimbo ni umbile la jumla la uzungumzaji wa mtu au kundi la watu. Uwepo wa kiimbo husaidia kuwabainisha watu mbalimbali wanapoongea. Kiimbo hushughulikia hali ya kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji wa neno au maneno. Kiimbo ni muhimu katika lugha za kibantu. Katika lugha ya Kiswahili, kiimbo husaidia kuleta maana kamili ya sentensi kama ilivyokusudiwa. Kwa kutamka sentensi fulani kwa kutumia kiimbo kifaacho, ni rahisi kubainisha kauli za kutolea taarifa, kuuliza swali na pia kuonyesha hisia.

Kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti kunategemea mtetemo wa nyuzi za sauti ndani ya glota. Ikiwa mtetemo ni wa kasi, mawimbi ya sauti hupanda na

mtetemo ukiwa wa polepole, basi kiimbo cha sauti kinashuka. Katika utafiti huu, mtafiti aliangazia namna sauti moja inavyopaa ikilinganishwa na sauti nyingine katika neno lililoambishwa kiangami. Viangami vinapoambishwa kwa neno kuu, neno linalopatikana huwa na dhana mbalimbali. Kwa mfano,

77. (a) Mamake

(b) Shangaziye

(c) Watakani?

Kiimbo hujitokeza katika viangami vya lugha ya Kiswahili. Baadhi ya maneno yanayoambishwa kiangami huwa ni aina ya kirai. Hivyo basi ni sawa kusema neno lililoambishwa kiangami ni aina ya kirai kinachoundwa na neno moja. Tazama mifano ifuatayo,

| 78 | **Neno lenye Kiangami** | | **Aina ya Kirai** |
|---|---|---|---|
| | (a) nduguye | **(**ndugu yake**)** | kirai nomino |
| | (b) walani? | (wala nini) | kirai kitenzi |
| | (c) chajio | (cha jioni) | kirai kihusishi |

Kulingana na mifano hii ni wazi kuwa maneno yaliyoambishwa viangami ni aina ya virai. Mifano hii ilisaidia kuonyesha mwingiliano wa kiimbo katika viangami. Mifano iliyotumika katika utafiti huu, inaonyesha kauli za kuulizia, kuonyesha hisia na pia kuafiki. Viwango vya kiimbo ni vya aina tatu. Kuna kiwango cha juu (JU), kiwango cha kati (KA) na cha tatu ni kiwango cha chini (CH) (Mwihaki, 2006). Katika kauli za kuuliza, kiimbo cha chini huanza na kuzidi kupanda. Nazo kauli za kuafiki huanza kwa kiimbo cha juu kinachozidi kushuka. Katika kauli

zinazoonyesha hisia kama vile mshangao, kiimbo cha chini huanza na kuzidi kupanda.

Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya kauli zilizo na viangami na zinatumika kupitisha dhana mbalimbali. Katika Mfano 79, sentensi zinaonekana kufanana lakini kuwepo kwa tofauti katika kiimbo kunazifanya sentensi zinazofanana kuwa na maana tofauti.

| | | |
|---|---|---|
| 79. | (a) *Bimkubwa* amewasili. | Tamko la kawaida. |
| | (b) *Bimkubwa* amewasili! | Tamko la mshangao. |
| | (c) *Bimkubwa* amewasili? | Swali. |
| | (d) *Watakani ?* | Swali la kawaida |
| | **(e)** *Watakani!* | Swali lenye hisia kama vile hasira au mshangao. |
| | (f) *Siye* | Tamko la kawaida. |
| | (g) *Siye?* | Swali. |
| | (h) *Siye?* | Shaka |
| | (i) *Siye.* | Hakika |

Mifano hii inadhihirisha matumizi ya kiimbo katika maneno yaliyoambishwa viangami. Kila kundi la maneno yaliyoambishwa viangami lina maneno yanayoendelezwa sawa ila dhana inayopitishwa ni tofauti kwa kila neno. Kinacholeta tofauti hizi katika maneno ni vile kuna tofauti ya kiimbo katika

matamshi. Katika utafiti huu, tulibaini kuwa kiimbo katika lugha ya Kiswahili hujitokeza kwa namna tatu.

1. Kiimbo cha kushuka
2. Kiimbo cha kupanda
3. Kiimbo cha kupanda na kushuka.

#### 4.2.2.1 Kiimbo cha Kushuka

Kiimbo cha kushuka kinaeleza jinsi sauti hushuka hadi kwa silabi ya mwisho inayotiliwa mkazo. Kiimbo cha kushuka hupatikana kwenye maswali yanayohusu 'lini?' na 'wapi?', kauli zinazoonyesha uhakika wa jambo na pia mzungumzaji anapoweka wazi jambo fulani. Baadhi ya mifano ya sentensi zenye kiimbo cha kushuka ni:

80. (a) Shangaziye yu wapi? (kuuliza swali)

(b) Mamake atapika pilau. (kauli yenye uhakika)

Mfano 80 unahusu sentensi zilizo na kiangami. Kulingana na sentensi hizi, mawimbi ya sauti yanapanda mwanzoni huku yakishuka. Kiangami kinapoambishwa kwenye neno kuu, utamkaji wa sentensi huwa tofauti ikilinganishwa na sentensi iliyo na maneno kamili. Kwa mfano,

81 (a) Yu wapi shangaziye? Pilau imepikwa na mamake.

(a) Yu wapi shangazi yake? Pilau imepikwa na mama yake.

Kila jozi ya sentensi hizi inapitisha ujumbe sawa ila utamkaji wake ni tofauti. Mfano a) unahusu sentensi zilizoambishwa kiangami. Kutokana na utafiti huu ni

kuwa, mawimbi ya sauti yanaanza juu na kisha kushuka. Yanaposhuka, neno lenye kiambishi linalotamatisha sentensi linatamkwa kwa sauti ya chini. Maneno haya ni *shangaziye* na *mamake.* Katika mfano b) neno la mwisho peke yake ndilo linaliathiriwa na kiimbo. Katika mfano b) maneno *shangazi* na *mama* hayaathiri matamshi. Kivumishi *yake* ndicho kinasikika kikishuka.

#### 4.2.2.2 Kiimbo cha Kupanda

Kiimbo cha kupanda hueleza jinsi sauti hupanda mwishoni mwa sentensi. Kiimbo cha kupanda hupatikana katika maswali yanayohitaji majibu ya ‘ndio’ au ‘la’. Kwa mfano,

82. (a) Shangaziye amekuja?

    (b) Mamake amepika?

Katika sentensi hizi mbili, mawimbi ya sauti yanasikika yakipanda katika neno la mwisho. Ikiwa neno la mwisho limefupishwa na kuambishwa kwa neno lililotangulia basi mawimbi ya sauti yatapanda katika neno lililoambishwa. Kwa mfano,

83 (a) Umempata binti yake?

(b) Umempata bintiye?

Katika sentensi ya kwanza, (a) tunapotamka kivumishi ‘yake’ mawimbi ya sauti yanasikika yakipanda. Neno binti linatamkwa kwa kawaida. Katika sentensi b), kivumishi ‘yake’ kimefupishwa na kuambishwa kwa neno ‘binti’. Wakati wa

utamkaji wa sentensi hii, neno ‘bintiye’ linatamkwa kwa nguvu. Hii ina maana ya kuwa ikiwa neno kuu linaunganishwa na neno linalostahili kupanda, neno kuu pia litaathiriwa.

#### 4.2.2.3 Kiimbo cha Kupanda na Kushuka

Kiimbo cha kupanda na kushuka hueleza jinsi sauti inavyopanda na kushuka. Kiimbo hiki hutumika ikiwa mzungumzaji hana uhakika wa anachosema. Kiimbo cha kupanda na kushuka pia hupatikana katika maswali yanayoonyesha unyenyekevu. Kwa mfano:

(a) Nilimwona mamake. (kuonyesha shaka)

(b) Ungetaka nikuitie shangaziye? (swali lenye unyeyekevu)

Katika mifano hii, neno moja linashuka na kupanda kwa wakati mmoja. Sentensi hizi mbili zinapitisha dhana tofauti. Katika sentensi ya kwanza, mzungumzaji anaonekana kutokuwa na uhakika wa anachosema. Nayo sentensi ya pili inaonyesha kuwa mzungumzaji anauliza swali kwa unyenyekevu. Ikiwa neno linalohusika limeambishwa kwa neno kuu au liwe limetumika kama kiangami basi matamshi yatatofautiana. Mifano inayofuata ya *bimkubwa na bibi mkubwa inadhihirisha haya.*

(a) Anayekuja ni bimkubwa.

(b) Anayekuja ni bibi mkubwa.

Sentensi hizi mbili zinatumika kuonyesha shaka. Sentensi zote mbili zinaonyesha kuwa anayesema hivi hana uhakika kuwa bimkubwa ndiye anayewasili. Kulingana

na sentensi (a) neno ‘bimkubwa’ lina kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti. Yaani, katika neno hilo ambalo liko na *bibi* na *mkubwa* kwa wakati huo mmoja linakuwa na shadda ya kupanda na kushuka. Lakini katika sentensi b) neno lililo na mawimbi ya kupanda na kushuka ni ‘mkubwa’ peke yake. Katika sentensi hii, neno *bibi* haliathiriki katika kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti kwani halijaunganishwa na neno mkubwa.

Kutokana na utafiti huu, viangami vinaathiri kiimbo katika sentensi. Ikiwa neno linalofaa kutamkwa kwa nguvu katika sentensi linakuwa neno moja kivyake, jinsi sentensi hiyo itavyotamkwa ni tofauti na ikiwa neno hilo linalohitaji kutamkwa kwa nguvu litakuwa neno kuu na kisha kuambishwa kiangami. Basi kwa kuambisha kiangami katika neno matamshi ya hiyo sentensi yatabadilika. Hivyo basi kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti kunaathiriwa na uambishaji.

Jedwali lifuatalo linaonyesha jinsi maneno yaliyoambishwa viangami yanavyotamkwa. Maneno yaliyotumika ni,

| | | | |
|---|---|---|---|
| Bibi | + | mkubwa | = bimkubwa |
| Wataka+ | | nini | = watakani |
| Si | + | yeye | = siye |

**Jedwali 4.6 Mwingiliano wa Kidatu katika Viangami**

| **Neno lenye Kiangami** | **Kidatu** | **Dhana inayopitishwa** |
|---|---|---|
| Bimkubwa | KACHJUCH | Tamko la kawaida |
| Bimkubwa | CHCHJUJU | Mshangao |
| Watakani? | KACHKAJU | Swali la kawaida. |
| Watakani? | CHKAJUJU | Hasira |
| Siye? | CHJU | Swali la kawaida |
| Siye? | KAJU | Swali lenye shaka |
| Siye | KACH | Hakika |

Kwa mujibu wa Jedwali 4.6, neno moja huweza kutamkwa kwa kiimbo tofauti. Matumizi ya kiimbo katika jedwali hili yanatumika kutofautisha kauli mbalimbali kama vile, kauli za kawaida zinazotolea taarifa, kauli za kuulizia na pia kauli za kuonyesha hisia. Hii ni wazi kuwa maneno yaliyoambishwa viangami huweza kuathiriwa na kiimbo. Tulitumia mashartizuizi ya umboupeo kuonyesha mwingiliano wa kiimbo na viangami katika lugha ya Kiswahili.

**Jedwali 4.7 Mashartizuizi katika Kipashio *watakani***

| /Wataka + nini/ | SHABI-JI | II |
|---|---|---|
| ☞ a) Watakani?<br>KACHKAJU | | |
| b) Watakanii?<br>KAKACHJU | | *! |
| c) Watakani?<br>JUJUKACH | * | |

Kulingana na Jedwali 4.7, washindani wote wamekiuka sharti la kwanza la SHABI-SI. Hii kwa sababu katika kila mshindani kuna vitamkwa vinavyodondoshwa. a) ndiye mshindi kwani amevunja sharti moja tu ambalo linavumilika katika dhana ya viangami. Mshindani b) amekiuka sharti muhimu la *II linalokataza mfuatano wa irabu mbili. Naye mshindani c) amevunja sharti la SHABI-JI kwani kuna mabadiliko ya matamshi.

Kwa mujibu wa mifano iliyotumika katika sehemu hii pamoja na mejedwali, ni wazi kuwa, kiimbo kinaathiriwa na uwepo wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Ikiwa mawimbi yanafaaa kupanda au kushuka katika neno fulani katika sentensi kisha hilo neno liambishwe kiangami, basi kutakuwa na mabadiliko ya kiimbo katika sentensi hiyo.

## 4.3 Hitimisho

Sura ya hii nne ilishughulikia mwingiliano wa sifa za kiarudhi katika viangami vya lugha ya Kiswahili. Mtafiti alianza kwa kutolea fasili ya sifa za arudhi kwa muhtasari tu. Sifa za kiarudhi ambazo zimeshughulikiwa katika sura hii ni shadda na kidatu. Katika kila sifa ya kiarudhi iliyoshughulikiwa, mtafiti ameonyesha mwingiliano wake na viangami. Lengo la utafiti katika sura hii lilikuwa ni kuonyesha fonolojia katika viangami. Sura ya nne imeweza kudhihirisha kuwa kiangami cha Kiswahili kinapoambishwa kwenye neno kuu, umbotokeo linalopatokana huwa ni neno, kirai na pia sentensi.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura zilizotangulia zimeshughulikia dhana ya viangami katika lugha ya Kiswahili. Kila sura imeshughulikia dhana moja muhimu kwa kuongozwa na maswali ya utafiti. Sura hii ya tano ndiyo ya mwisho katika utafiti huu. Katika sura hii, mtafiti ametamatisha kwa kutoa muhtasari wa utafiti, mapendekezo ya utafiti na pia changamoto za utafiti.

## 5.2 Muhtasari

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua viangami katika lugha ya Kiswahili kimofosintaksia. Kwa jumla, madhumuni ya kazi hii yalikuwa ni: kubainisha tofauti zilizopo katika kuambisha viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili. Pili ni kuchunguza sheria zinazofuatwa katika uundaji wa viangami mwafaka katika lugha ya Kiswahili na mwisho ilikuwa ni kuweka wazi mwingiliano uliopo baina ya sifa za kiarudhi na viangami vya Kiswahili.

Sura ya kwanza ni kitangulizi cha kazi nzima na pia ni muhtasari wa utafiti mzima. Sura ya kwanza ilishughulikia mambo yafuatayo: usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada,  nadharia na hatimaye mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilishughulikia uambishaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti alifanya hivyo kwa kulinganisha uambishaji wa viangami na ule wa viambishi katika lugha ya Kiswahili. Kwanza, mtafiti alishushughulikia mofolojia ya Kiswahili kwa muhtasari tu. Mtafiti alishughulikia maumbo mbalimbali ya viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili. Maumbo haya yalielezewa kwa kuongozwa na nadharia ya umbo upeo. Sura ya pili inaonyesha aina mbalimbali za viangami. Kunavyo viangami kulingana na mahali vinamotokea. Hivi ni viangami awali na viangami tamati. Pia kuna aina ya viangami kwa kuzingatia uamilifu wake wa kisarufi kama vile kumilikisha, kuashiria, kuyakinisha, kukanusha na kuulizia. Sura hii ilimalizia kwa kuweka wazi tofauti kati ya viangami na viambishi katika lugha ya Kiswahili.

Sura ya tatu ilishughulikia utaratibu wa uundaji wa viangami katika lugha ya Kiswahili. Lengo la sura hii lilikuwa kutambua sheria za kisarufi zilizozingatiwa ili kupata viangami vinavyokubalika na wanajamii na wanaisimu wa lugha ya Kiswahili. Kiangami kilishughulikiwa kama mojawapo wa vipashio katika lugha ya Kiswahili. Baadhi ya kanuni za uundaji wa viangami zilizoshughulikiwa ni kama vile: viangami vinachukua muundo wa silabi wazi, viangami vinaundwa na irabu moja, maana halisi inabaki katika kiangami, neno linaloambishwa lifuatane na kiangami moja kwa moja katika sentensi na pia hakuna viangami vya konsonanti pekee.

Sura ya nne ilishughulikia mwingiliano wa sifa za kiarudhi na viangami katika lugha ya Kiswahili. Sifa za kiarudhi ni sifa za kifonolojia ambazo zinahusu

mabadiliko ya mkazo, kiimbo na toni katika vipashio mbalimbali. Katika sura ya nne, mtafiti alishughulikia sifa nne za kiarudhi. Kwanza mtafiti alishughulikia shadda. Hiki ni kiwango cha nguvu inayotumiwa wakati wa kutamka silabi. Pili, mtafiti alishughulikia kiimbo. Huku ni kupaa kwa silabi moja ikilinganishwa na sauti nyingine ambata.

Data iliyotumika katika utafiti huu ilikusanywa kwa kusoma vitabu, makala na tasnifu zilizoshughulikia mada. Data hii ilipatikana maktabani. Data iliyochanganuliwa iliwasilishwa kwa maelezo huku mtafiti akiongozwa na nadharia ya umbo upeo. Kando na maelezo yaliyotolewa, mtafiti alitumia majedwali na michoro kuwasilisha data.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu umethibitisha kuwepo kwa viangami katika lugha ya Kiswahili. Viangami hutokea baada ya kudondosha baadhi ya vitamkwa katika neno moja na kuviambisha kwa neno kuu, yaani neno linalotangulia au kufuata. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa kiangami ni kipashio katika lugha ya Kiswahili. Kiangami ni kipashio ambacho kinaambishwa kwa kipashio kingine yaani neno kuu. Viangami huambishwa mwanzoni au mwishoni mwa neno kuu. Hivyo basi kuna viangami awali na viangami tamati. Viangami katika lugha ya Kiswahili huwa na dhima ya kisarufi. Baadhi ya viangami katika lugha ya Kiswahili huwa na dhima ya kumilikisha, kuashiria, kuulizia, kukanusha, kuyakinisha na kuonyesha nafsi.

Viangami katika lugha ya Kiswahili vinaundwa kwa kuongozwa na sheria za kisarufi kama ilivyo katika vipashio hivyo vingine. Kanuni zilizotumika katika uundaji wa viangami zilikuwa kadha. Kwanza viangami vya Kiswahili vinachukua muundo wa silabi wazi. Sheria ya pili ni kuwa viangami katika lugha ya Kiswahili vinaundwa kwa irabu moja pekee. Hii ina maana kuwa hakuna viangami vya zaidi ya irabu moja.

Sheria nyingine ni kuwa baada ya neno kufupishwa na kuwa kiangami, maana halisi ya neno asili hubaki. Ili neno liambishwe kiangami, ni sharti kuwe na mfuatano wa maneno yale mawili katika sentensi. Pia lazima kiangami kihusiane na neno kuu kisarufi. Hivyo basi kiangami na neno kuu ni aina ya kirai. Sheria nyingine ni kuwa katika lugha ya Kiswahili, neno moja kamili huambishwa kiangami kimoja tu. Hatimaye, utafiti huu ulionyesha kuwa hakuna viangami vya konsonanti moja.

Kutokana na utafiti huu, viangami vya Kiswahili ni vipashio vikubwa kuliko foni. Kiangami ni silabi. Kiangami kinapoambishwa neno kuu, tunapata neno, kirai na pia sentensi. Kwa sababu hii, tuliweza kuangalia mwingiliano kwa sifa za kiarudhi na viangami vya lugha ya Kiswahili.

Kilicho wazi ni kuwa katika lugha ya Kiswahili, mkazo huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho. Hata neno linapoambishwa kiangami, bado silabi ya pili kutoka mwisho ndiyo inayowekwa shadda. Utafiti huu ulionyesha kuwa ikiwa neno kuu lina zaidi ya silabi mbili, kiangami awali hakiathiri silabi inayowekwa

shadda. Kiangami tamati kinapoambishwa kwa neno kuu, silabi inayowekwa shadda katika neno kuu inabadilika.

Maneno yanayoambishwa viangami huleta dhana mbalimbali na kwa hivyo hutamkwa kwa njia tofauti. Kwa mfano, kitenzi *wataka* kinapoambishwa kiangami *ni* tunapata *watakani?* Kipashio hiki kinaweza kuwa sentensi ya kuuliza swali la kawaida na hata kuonyesha mshangao. Hivyo basi kiimbo katika sentesi hii kinabadilika kutegemea dhana inayopitishwa.

## 5.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa viangami katika lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu unachangia pakubwa katika kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Viangami si suala geni katika lugha zingine ulimwenguni, hivyo basi kulikuwa na haja ya kushughulikia viangami katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia sheria za kisarufi za lugha ya Kiswahili. Utafiti huu utasaidia wanaisimu kuelewa viangami katika lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu utawafaidi wanaotumia lugha ya Kiswahili kimaandishi na kimaongezi katika shughuli zao za kila siku. Hawa ni kama vile waandishi wa vitabu mbalimbali vya Kiswahili, wanahabari na pia wanajamii. Wataweza kutofautisha maneno yaliyoambishwa viangami na yale yasiyoambishwa.

Utafiti huu utawanufaisha wanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Wataweza kutambua njia mbalimbali za kutumia misamiati iliyo kamili na ile ambayo imefupishwa na kuambishwa kwa maneno mengine. Hawatakanganyika wanapoyaona maneno

yaliyoambishwa na yale yasiyoambishwa. Kwa mfano, wakiona maneno kama vile *twenzetu* na *twende zetu,* wataweza kutambua kuwa maana ni sawa hata kama muundo ni tofauti. Hii itawasaidia kutambua maneno ambayo yamefupishwa na kuwa viangami na hivyo kuwasaidia wasikanganyike haswa wanapohitajika kuunda sentensi ili kuainisha maneno ya Kiswahili.

Wengine watakaonufaika kutokana na utafiti huu ni waandishi wa vitabu vya Kiswahili pamoja na wanafunzi wa somo la Kiswahili wanaovitumia vitabu hivyo. Utafiti huu utawasidia wanafunzi kutofautisha maneno yaliyoambishwa na yale ambayo yana viangami. Mara nyingi wanafunzi hutunga sentensi ambazo zinawatatiza kuainisha. Kunao waandishi wa vitabu vya kiada wanaochanganya viangami na viambishi. Jambo hili hukanganya wanafunzi hasa wa shule za upili. Kwa mfano, kwa maoni ya Ipara na wengine (2010), kuna viambishi viulizi. Baadhi ya mifano iliyotolewa ni kama vile, *wendapi*. Hapa waandishi wanaainisha kipashio -pi- kama kiambishi kiulizi ilhali -pi- ni kiangami kinachotokana na neno kamili *wapi.* Jambo hili linawakanganya wanafunzi wanaokitumia kitabu hiki katika kudurusu au hata kujifunza upya mada hii ya viambishi. Inatarajiwa kuwa data itakayowasilishwa katika utafiti huu itasaidia pakubwa katika kuendeleza sarufi ya Kiswahili na ambayo itatumika na wanaisimu kuchanganua na kufasiri zaidi matumizi ya viangami katika lugha ya Kiswahili.

## 5.5 Changamoto

Utafiti huu umekuwa na manufaa mengi kwa watafiti waliohusika. Hata hivyo watafiti walikumbana na matatizo hapa na pale. Tatizo la fedha za kufanyia utafiti lilikuwepo. Safari za kwenda nyanjani na maktabani zilimgharimu mtafiti kiasi kikubwa cha pesa. Vitabu kadha vilihitajika ila si vyote vilivyokuwa maktabani. Mtafiti alitumia fedha nyingi kununua vitabu muhimu alivyohitaji ili kukamilisha utafiti wake. Mtandao ulikuwa muhimu katika utafiti huu kwani mtafiti alipakua makala muhimu kutoka mtandaoni. Pesa nyingi zilitumika wakati wa kwenda mtandaoni.

## 5.6 Hitimisho

Sura hii imeangazia muhtasari wa matokeo ya utafiti. Umuhimu wa utafiti umepitiwa kwa muhtasari tu. Mtafiti pia ametaja baadhi ya changamoto alizokumbana nazo wakati wa utafiti.

## MAREJELEO

Alotaiby, F., Foda, S. and Alkharashi, I. (2010). *Clitics in Arabic Language:A Statistical Study.* Saudi Arabia: King Saud University.

Anderson, S.T. (2010) *Clitics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Baker, M., Johnson, K. and Roberts, I. (1989). 'Passive argument raised', *Linguistic Inquiry.*Vol. 20, No.2 pp. 219-251.

Bakita, (2015). *Kamusi kuu ya Kiswahili (KKK).* Dar es Salaam: Longhorn Publishers Limited.

Buckwalter, T (2004). *Buckwalter Arabic Morphological Analyzer Version 2.0.* Philadelphia: Linguistic Data Consortium (LDC).

Buliba, A. Gwachi, M. and Matinde, R. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Chisia, M. (2019). *Sarufi Kuntu ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: Rinny Education and Technical Piblishing Servises.

Chomsky, N. and Halle, M. (1968). *The Sound Pattern of English.* New York: Harper and Row.

Denham, K. and Lobeck, A. (2010). *Linguistics for Everyone: An Introduction. 2nd Edition.* Boston, Wadsworth.

Dictionary. com. www.dictionary.com. 22 January 2018

Donna, B. (2003). The Morphosyntax of Halkomelem Lexical suffixes. *International Journal of American Linguistics. 69(4): 345-356*

Elfner, E. (n.d.) *Stress-Epenthesis Interactions in Harminic Serialism.* Amherst: University of Massachusetts.

Franks, S. and King, T. (2000). *A Handbook of Slavic Clitics.* Oxford: Oxford University.

Fromkin, V., Rodman, R. and Hyams, N. (2003). *Language: An Introduction to Language.* 79 (4), 768-771.

Habwe, J. and Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Halpern (2001). *Clitics and Clouse Structure.* CA: Stanford University

Hartmann, R. and Stork, F. (1972). *Dictionary of Language and Linguistics.* London. Applied Science.

Ipara, I. Burudi, J. and Wakio, N. (2010).*Upeo wa Sarufi: kwa Shule za Upili.* Nairobi:Oxford.

Kager, R. (1999). *Optimality Theory.* Cambridge. Cambridge University Press.

Kari, E.E. (2002a). *African Study Monographs, 23 (3): 91-115.* Tokyo: University of Foreign Studies.

Kari, E.E. (2002b). *Distinguishing between Clitics and Affixes in Degema , Nigeria.* Tokyo. Textversion.

Kihore, M.Y. Masamba, D.P.B. na Msanjila, Y.P. (1999). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. (*SAMAKISA*): Sekondari na vyuo.* Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Kombo, D. and Tromp, L. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi: Paulines.

Lebman, W.P. (1973). *Descriptive Linguistics.* New York: Random House.

Massamba, D., Kihore, Y. and Hokororo, J. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu.*Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia.* Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Massamba, D. P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na falsafa ya lugha: Toleo la pili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Matthews, P. (1974). *Morphology: Second Edition.* Cambridge. Cambridge University Press.

Matundura, B. (2016). *Mbinu za uundaji wa Istilahi katika Kiswahili.* Imepakuliwa kutoka kwa Swahilihub-Thursday, January 7 2016 at 10:38.

Mgullu, R. (2001). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn.

Mugenda, O. M., and Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods: Qualitative and Quantitative Approaches.* Nairobi: Acts press.

Muguti, E. (1989). *Uundaji wa Nomino katika Kiswahili*. Nairobi: University of Nairobi Library.

Mulokozi, M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Muthooka, P. (2016). AKS 300 *Morphologhy and Syntax: Kenyatta University, Institute of Open Learning.* Idara ya Kiswahili na lugha za kiafrika. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwihaki, A. (2006). *Kiswahili Phonetic and Phonology*. Nairobi: Kenyatta University Institute of Open Learning.

Njogu, K. Mwihaki, A na Buliba, A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili; Uchunguzi na Matumizi*. The Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.

Polyglossia (2013). *Multilingualism: Language Policy.* Georgetown University Press.

Prince, A. and Smolensky, P. (1993). *Optimality Theory: Constraints Interaction in Generative Grammar.* Rutgers Center for Cognitive Science: Rutgers University.

Quinion, M. (2008). Affixes: *The Building Blocks of English*. Retrieved from http://www.affixes.org/type 2017.

Radford, A. (1981). *Transformational Syntax.* Cambridge: Cambridge University Press

Robert, S. (1967). *Utenzi wa Uhuru.* Nairobi. Oxford University Press

Runder, M. (2007). *English Dictionary for Advanced Learners: Second Edition.* New York Macmillan Education Publishers.

Spencer, A. and Luis, A. (2012). *Clitics: An Introduction.* Cambridge: Cambridge University Press.

TATAKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Tatu.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI. (2012). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la Pili*. Nairobi: Oxford University Press.

Varlokosta, S., Balletti, A., Veenstra, A., Weston, J., Yachini, M. and Yatsushiro, K. (2015). *Cross-Linguistic Study of the Acquisition of Clitics and Pronoun Production.*Taylor & Francis Group, LLC. Online.

Yule, G. (1996). *The study of language.* Cambridge: Cambridge University Press.

**KIAMBATISHO A:**

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 454462

Date of Issue: 17/November/2020

**RESEARCH LICENSE**



This is to Certify that Ms.. Naomi Ndumba Kimonye of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: UCHANGANUZI WA KIMOFOSINTAKSIA WA VIANGAMI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI for the period ending : 17/November/2021.

License No: BAHAMAS ABS/P/20/7722

454462

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commission for Science, Technology and Innovation -

## KIAMBATISHO B:

**KENYATTA UNIVERSITY**
**GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57530

Our Ref: C50/CE/25010/2014

DATE: 10th July, 2018

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
**NAIROBI**

Dear Sir/Madam,

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR KIMONYE NAOMI NDUMBA REG. NO. C50/CE/25010/2014.**

I write to introduce Kimonye Naomi Ndumba who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the Department of Kiswahili.

Kimonye intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, "Uchanganuzi wa Kimofosintaksia wa Viangami Katika Lugha ya Kiswahili".

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

MRS. LUCY N. MBAABU
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

EM/lnn

**KIAMBATISHO C:**

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 10th July, 2018

TO: Kimonye Naomi Ndumba
C/o Kiswahili Dept.

REF: C50/CE/25010/2014

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 4th July, 2018 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, "Uchanganuzi wa Kimofosintaksia wa Viangami Katika Lugha ya Kiswahili".

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking Forms per semester. The form has been developed to replace the Progress Report Forms. The Supervision Tracking Forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

ELIJAH MUTUA
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili Department

Supervisors:

1. Daktari Leonard Chacha Mwita
   C/o Department of Kiswahili
   Kenyatta University

2. Daktari Jacktone Onyango
   C/o Department of Kiswahili
   Kenyatta University